# Nipashe

Alhamisi Desemba 26, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580111

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US





UKURASA 13



## Waziri Mpina amaliza mgogoro wa miaka 15 wa Narco, wafugaji

UKURASA 24

# Lissu aanika mbinu 5 za kuing'oa CCM 2020

UKURASA 4





"Uchu wa madaraka na tamaa ya utajiri vinahatarisha amani ya nchi na kuchochea mauaji ya watu wenye ualbino na wazee.

ASKOFU SANGU



"Mke anapokosea, mume hupaswi kumnyanyasa, badala yake mweleweshe.

KINYAIYA



"Kuwe na mtazamo kwamba ushindani wa kisiasa si uadui bali ni ulinganisho wa sera.

ASKOFU SHAO



"Watanzania hawapaswi kuwatesa wala kufurahia kuwatesa wenzao wasio na hatia.

DK. DK. SHOO




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


# Maaskofu watoa ujumbe mzito

• **Ruwa'ichi** ataka amani ilindwe, Dk. Shoo akemea kutesana, mwingine aona shida siasa Zanzibar... *Uk. 2,3,5,11 na 23*

## Mjamzito, mtoto wafa kusombwa na maji

UKURASA 4

MICHEZO SIMBA SC YANOGESHA KRISMASI UK.32

MAONI, KATUNI UK.6

UJUMBE WA KRISMASI

# Uchu madaraka, utajiri 'vyamliza' Askofu Sangu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

ASKOFU wa Jimbo la Katoliki Shinyanga, Liberatus Sangu, amekemea vitendo vya watu kuwa na uchu wa madaraka na tamaa ya kuwa matajiri, akieleza kuwa vinachochea mifarakano ndani ya familia na mauaji ya watu wasio na hatia, wakiwamo watu wenye ualbino na wazee.

Askofu Sangu aliyasema hayo juzi usiku wakati wa misa ya mkesha wa sikukuu ya Krismasi iliyofanyika katika Kanisa Kuu la Mama Mwenye Huruma Ngokolo mjini Shinyanga.

Alisema uchu wa madaraka na tamaa ya kuwa tajiri ni vitu vibaya nchini na vimekuwa vikihatarisha amani ya nchi.

Alisema mtu anapokuwa na uchu wa madaraka au tamaa ya kutaka utajiri wa mali, yuko radhi kusababisha mauaji ya watu wasio na hatia, hasa kutokana na imani potofu aliyojengewa kwa kuwatoa kafara watu wenye ualbino na wazee ili apate vitu hivyo.

"Leo napenda kuhubiri vitu viwili tu uchu wa madaraka na tamaa ya utajiri wa mali, vitu hivi ni vibaya sana hapa nchini kwetu kwa sasa, vimekuwa vikihatarisha amani na hata kusababisha mauaji ya watu wasio na hatia, wakiwamo wenye ualbino na wazee," alisema.

"Natoa wito kwa Watanzania wote, tukatae dhambi pamoja na tamaa za kidunia, bali tumkabidhi Yesu Kristo atawale maisha yetu na yeye ndio mtoa riziki.

"Tukifanya hivyo amani nchini itaendelea kutawala, na wala hakutakuwa na mauaji ya aina yoyote ya watu wasio na hatia, tutaishi kwa upendo na amani," alishauri.

Kiongozi huyo wa kanisa pia aliwataka Watanzania kuendelea kuiombea nchi amani, umoja, mshikamano na kuepukana na aina yoyote ya ubaguzi na kupinga vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto ili Tanzania iwe sehemu salama pa kuishi.

Baadhi ya waumini waliohudhuria mkesha huo, walipongeza Jeshi la Polisi kwa kuimarisha ulinzi na usalama kanisani hapo, hivyo kuwawezesha kusali bila ya kuwa na hofu yoyote ya uvunjifu wa amani.

# Askofu Shoo aonya kutesana

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Fredrick Shoo, ameonya kuhusu kile alichokiita kutesana, akisema Watanzania hawapaswi kutesa wala kufurahia kuwatesa wenzao wasio na hatia.

"Tuache kuwatesa wanadamu wenzetu, tuache kufurahia kuwatesa wengine wasio na hatia, iwe ni katika nyumba zetu, kuna watu wanateka sana katika nyumba zao na ukisikiliza mashauri ya nyumba, mpaka saa nyingine 'unasema ee Mungu wewe, tunakuomba uingilie kati katika nyumba zetu', maana kuna watu wanatesana, kuna watu wanateswa, watoto, wake na waume wanateswa," alisema.

Askofu Shoo alikuwa akihubiri jana katika ibada ya kwanza ya sikukuu ya Krismasi iliyofanyika Kanisa Kuu la Usharika wa Moshi Mjini.

"Tunaambiwa baraka ya Krismasi, baraka ya kuzaliwa Yesu Kristo ni ili atuletee amani. Najiuliza amani hii iko katika nyumba zetu, iko katika jamii yetu?

"Tumeadhimisha Siku 16 za Kupinga Ukatili, ukatili wa aina yoyote na katika siku zile tulisikia mengi kuhusu ukatili unaofanyika kwa njia mbalimbali.

"Amani ya Kristo ituongoze, itutangulie, tusiwatese wenzetu wala tusifurahie kuwatesa wenzetu. Unajua ilikuwa ni nini? Ni kwa sababu huyu Yesu aliyepewa jina hili anajua maana ya kuteswa.

"Tunapotesa wengine, tujue kwamba Yesu anapata uchungu. Ndiyo maana kumtesa mwanadamu mwenzetu kwa namna yoyote ile tunamtesa Mungu. Hivyo, anasema ninasikia uchungu, hebu tukawe wajumbe wa amani ndugu zangu.

"Kwa wale mlio katika mateso, kuzaliwa kwa Yesu kukawaletee matumaini na kutambua kwamba Mungu anazijua shida zetu. Katika kuteseka kwetu kwa namna yeyote ile iwe ni kwa magonjwa iwe ni shida mbalimbali na kutesa wengine bila hatia, tujue kwamba Mungu yu pamoja nasi.

"Mpendwa unayemwamini Yesu Kristo, jua uko upande wa amani, usikate tamaa wala kuondoa imani na weka tumaini lako kwa Mungu. Saa zote na wakati wote jua kwamba Mungu yu nawe, Mungu hajakusahau na kwa ajili hiyo usiogope. Mateso haya, mateso unayokutana nayo katika maisha haya, tujue yatapita, yana mwisho wake.

"Nilipokuwa mdogo kule mlimani Machame, mzee mmoja alikuwa anamtesa sana mke wake, nakumbuka hata siku moja, tena ilikuwa kipindi cha mvua, alitoka kwenye pombe zake na ameshakula nyama za kuchoma, alipofika alikuta chakula hakijaiva na mama yuko jikoni na watoto wamezunguka pale, akamwambia 'bado chakula hakijaiva mvivu kabisa wewe'.

"Akasahau kwamba yule mama alikuwa amechoka, ametoka kutafuta chakula cha mifugo, ameandaa watoto huyu mama,

INAENDELEA UK. 8




Mwendesha guta akipewa msaada wa kuvutiwa mkokoteni wake baada ya kuharibika na kushindwa kutembea eneo la Manzese hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Viongozi wawe na hofu ya Mungu'

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

ASKOFU Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki Arusha, Mhashamu Isaac Amani, amewataka wakristo kuombea viongozi watambue uwapo wa Mungu ili waongoze nchi kwa kufuata sheria, haki, ukweli na kuondoa hofu, woga na unafiki.

Wito huo ulitolewa kupitia waraka maalumu wa salamu za Krismasi wa mwaka huu 2019 uliotiwa saini na Askofu Amani na Askofu Msaidizi Prosper Lyimo wa jimbo hilo na kusomwa mbele ya waumini wa Kanisa la Utatu Mtakatifu Kwa Murombo na Padri Rethinasamy Amaldoss.

"Tuiombee nchi yetu Tanzania, viongozi na raia tujaliwe kuongozwa na sheria, haki na ukweli tukiondokana na hofu, woga na unafiki, ubaguzi wowote wa matamshi au mipango kwani ni tishio kubwa kwa amani na ustawi wa watu," alisema.

Alisema kuzaliwa kwa Emanueli ambaye ni mfalme wa amani, kupokewe kwa kila familiya na watu wote ili aliombee taifa umoja, uzalendo na amani.

"Emanueli abariki familia na jumuiya zetu kwa zawadi zake za kimungu, umoja, dawa ya upweke, dawa ya ubinafsi na utoshelevu wa nafsi na dawa ya mahangaiko, kwani Mungu asipoijenga nyumba, waijengao wanajisumbua bure," alisema wakati akisoma waraka huo.

Alisema ni vyema kila muumini akajitahidi kuepuka kuwa na malezi ya mzazi mmoja ambayo yana athari kiroho, kisaikolojia na kijamii, kwa kuwa hata Yesu alilelewa na Yosefu na Maria.

"Kama mwana wa Mungu alilelewa na kulindwa na walezi wawili, vivyo hivyo nasi tuwalinde na kuwalea watoto wetu," alisema.

Pia, aliomba sikukuu hiyo ikawe mwisho wa matukio ya ukatili dhidi ya watoto katika mikono ya jamaa, wazazi, walezi na walimu na mauaji ya vichanga kwa njia ya utoaji mimba, ili kuleta amani kwa kila mmoja.

Katika waraka wake huo, Askofu Amani pia alisisitiza kukomesha ukatili kati ya wanandoa na utelekezaji wa familia na migogoro isiyoisha kati ya wanandoa.

## UJUMBE WA KRISMASI



Muuza samaki katika soko kuu la mjini Iringa, Zakaria Haule, akisubiria wateja ambapo alisema biashara katika sikukuu ya Krismasi sio nzuri kwake kutokana na watu wengi kununua nyama ya ng'ombe. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Askofu akemea ukatili wanandoa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

ASKOFU Mkuu Jimbo Kuu Katoliki Dodoma, Beatus Kinyaiya, amewataka wanaume walioko kwenye ndoa kuacha kuwanyanyasa wanawake kijinsia, akieleza kuchoshwa na malalamiko anayoyaona mara kwa mara kwenye vyombo vya habari.

Ameitaka jamii kutumia sikukuu ya Krismasi kufanya mabadiliko ya mienendo ili kuendeleza amani iliopo nchini.

Askofu Kinyaiya aliyasema hayo katika misa ya mkesha wa Krismasi iliyofanyika katika Kanisa Kuu Katoliki la Paulo wa Msalaba jijini Dodoma.

Alisema amekuwa akisikia malalamiko mengi juu ya unyanyasaji wa wanawake katika ndoa, jambo ambalo si zuri kwa mkristo aliyekamilika na jamii kwa ujumla, hivyo wanaofanya ukatili huo wanapaswa kuacha.

"Hivi kwanini umnyanyase mkeo wa ndoa wakati uliapa kuishi naye katika shida na raha? Nawaomba wenye tabia hiyo, tumieni sikukuu hii kufanya mabadiliko ndani ya mioyo yenu na tabia kwa ujumla," alisema.

Kiongozi huyo wa kiroho alisema si jambo zuri kiimani kumnyanyasa mke, akishauri kuwa mume anapaswa kumwelewesha mkewe pale anapokosea. Askofu Kinyaiya pia aliwataka viongozi wenzake wa dini kuendelea kutangaza neno la Mungu na kutangaza injili kwa jamii nzima.

Alisema wasikubali kukatishwa tamaa au kurudi nyuma kutokana na vikwazo mbalimbali, bali watekeleze wajibu wao kueneza neno la Mungu ili jamii ielewe makusudi ya Mungu.

Askofu Kinyaiya pia aliwataka waumini wa kanisa hilo na jamii kwa ujumla kuendelea kuiombea amani ya nchi, akisisitiza kuwa kupitia sikukuu hiyo, watu wanapaswa kujitakasa na kujisafisha ndani ya mioyo yao ili kuanza upya.

# Askofu awamulika wanasiasa waenda kwa waganga kienyeji

**Na Waandishi Wetu, DODOMA**

ASKOFU wa Kanisa la Angalikani Dayosisi ya Kati, Dk. Dickson Chilongani, amesema anachukizwa na tabia ya wanasiasa wanaokimbilia kwa waganga wa kienyeji kipindi cha uchaguzi.

Amesema kitendo hicho kamwe hakiwezi kusaidia kupata viongozi wenye maadili ya uongozi na wenye hofu ya Mungu.

Dk. Chilongani aliyasema hayo alipokuwa akihubiri kwenye ibada ya sikukuu ya Krismasi iliyofanyika katika Kanisa Kuu la Angalikani Tanzania Dayosisi ya Dodoma.

Bila kutaja majina ya wanasiasa hao, kiongozi huyo wa kanisa alidai anachukizwa na tabia hiyo na kuwataka viongozi hao kwenda kanisani kuombewa badala ya kukimbilia kwa waganga wa kienyeji.

"Kiongozi mzuri ni yule anayetokana na Mungu mwenyewe na siyo anayetokana na nguvu za giza, hivyo ni vema wanasiasa wakapeleka shida zao kwenye nyumba za ibada na si vinginevyo," alisema.

Askofu huyo pia aliwataka wakristo kuitumia sikukuu hiyo kutangaza upendo na amani badala ya kuigeuza kuwa ya machafuko yanayoharibu hata dhana ya Krismasi.

Alisema kumekuwa na tabia kwa baadhi ya watu inapofikia kipindi cha sikukuu, kuigeuza siku hiyo kuwa ya kuchafua amani ambayo Mungu amewatunuku wanadamu.

"Kwenye kipindi hiki cha sikukuu ya Krismasi siyo cha kuhatarisha amani, bali ni cha kudumisha amani na kujiepusha na vitendo vilivyo viovu," alisema.

Hoja hiyo pia ilisisitizwa na Askofu wa Dayosisi ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKKT) Jimbo la Dodoma, Amon Kinyunyu, ambaye katika mahubiri yake aliwataka Watanzania kusherehekea sikukuu hiyo kwa malengo yaliyokusudiwa na si vinginevyo.

Askofu Kinyunyu alisema watu wengi wamekuwa wakijisahau na kufanya mambo ambayo yapo nje ya maana halisi ya sikukuu ya Krismasi.

"Tumpokea Yesu katika mioyo yetu ili atusaidie kwenye maisha yetu, yeye ndiye mponyaji wa magonjwa, anayetoa baraka kwa kila mtu, hivyo tusherehekee kwa sababu tunajua kuhani wa milele amezaliwa," alisema.

***Imeandikwa na Peter Mkwavila na Renatha Msungu, DODOMA.**



# Lissu aanika mbinu 5 za kuing'oa CCM 2020

**Na Enock Charles**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Tundu Lissu, ametaja mambo matano anayoamini yakifanyika, yatakiwezesha chama hicho kikuu cha upinzani nchini kuingia madarakani mwakani.

Katika taarifa yake ya salamu za Krismasi kwa wananchi na wanachama wa Chadema, Lissu ambaye yuko nje ya nchi, alisema kudai tume huru ya uchaguzi ni miongoni mwa mambo hayo matano.

Alisema ni muhimu kwa chama hicho kuwa na harakati za kudai mabadiliko ya mfumo wa uchaguzi ili kupata tume huru itakayosimamia uchaguzi, kauli ambayo pia ilitolewa na Katibu Mkuu wa chama hicho, John Mnyika wiki iliyopita.

"Tuamshe harakati na vuguvugu kubwa nchi nzima, itakayoshirikisha vyama vingine vya upinzani, taasisi za kijamii, taasisi za kidini, vyama vya wafanyakazi, vyama vya kitaaluma na wananchi wa kawaida, kauli mbiu yetu iwe bila tume huru hakuna uchaguzi," Lissu alishauri.

Lissu alisema bila kufanya hivyo, anaamini itakuwa ngumu kwa upinzani kukiangusha Chama Cha Mapinduzi (CCM), akirejea uchaguzi uliofanyika mwezi uliopita wa serikali za mitaa ambao hata hivyo vyama vya upinzani vilijitoa kwa madai ya kuchezewa rafu ya kuenguliwa kwa wagombea wake.

Alidai uchaguzi huo ni uthibitisho tosha ya kuwa sasa inahitajika tume huru ya uchaguzi nchini ili iwatendee haki katika uchaguzi mkuu wa mwakani.

Lissu alitaja mkakati mwingine kuwa ni kuandaa wagombea udiwani, ubunge na urais mapema na wagombea hao wawe ni watu walio imara kwa mafunzo na vitendea kazi katika hatua zote za uchaguzi. Aliwataka wanachama wa Chadema kuepuka ugomvi na migongano ya kujitakia katika kipindi cha uchaguzi, akiamini kuwa itasababisha chama hicho kushindwa katika uchaguzi.

Mtaalamu huyo wa sheria alisema jambo la nne ni kuimarisha ushirikiano katika Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa) ambao alisema unapaswa kuwa mpya kwa kuzingatia maslahi ya kila chama katika uchaguzi ili kuepuka misuguano baina ya vyama hivyo.

Akifafanua kuhusu suala hilo, Lissu alirejea yaliyotokea mwaka 2015, pale vyama vilivyounda Ukawa viliposhindwa kuafikiana katika baadhi ya majimbo na kujikuta vinasimamisha wagombea wawili na kuirahisishia kazi CCM kushinda kutokana na vyenyewe kugawana kura.

"Katika ushirikiano wowote wa aina hii, kuna 'give and take' (toa na chukua) tusijiangalie sisi na maslahi yetu pekee, tuwaangalie

INAENDELEA UK. 8



Mkazi wa jijini akiondoa taka kwenye mtaro eneo la Mbezi Masana jijini Dar es Salaam, jana, zilizosababisha kuziba mtaro huo, kutokana na mvua zinazoendelea kuonyesha. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mjamzito, mtoto wafa kwa kusombwa na maji

**Na Gurian Adolf,** KALAMBO

MJAMZITO aliyefahamika kwa jina la Maria Kalunde (42) pamoja na mtoto wake, Magreth Lui (9), wamekufa maji baada ya kutumbukia katika Mto Kalambo mkoani Rukwa.

Mama na mtoto huyo walikutwa na mauti baada ya kutelekezwa katika kivuko cha miguu cha mto huo.

Tukio hilo lilitokea Jumatatu katika kijiji cha Kasitu, Kata ya Sopa wilayani Kalambo wakati watu hao wakivuka katika mto huo.

Mmoja wa wakazi wa kijiji hicho, Nobert Mwanawima, aliyeshuhudia tukio hilo, alisema mwanamke huyo na mtoto wake walikufa maji kutokana na eneo hilo kutokuwa na daraja la kuvukia kitendo kilichosababisha wananchi wa kijiji hicho kutengeneza kivuko cha miguu kinachokatisha mto kwa kutumia miti. Alisema mwanamke huyo alipokuwa akipita katika kivuko hicho na mwanawe, waliteleza na kutumbukia mtoni na kisha walianza kupiga kelele za kuomba msaada, lakini kwa kuwa watu walikuwa mbali hawakufika kwa wakati kuwasaidia.

"Siku mbili baadaye tulipata taarifa kuwa miili yao imepatikana katika kijiji jirani na baada ya kuona kuwa watu hao hawafahamiki waliamua kufanya maziko, ndipo walipoamua kuchukua msiba na kuusafirisha hadi kijiji cha Katete walipokuwa wakiishi," alisema.

Naye Jeremiah Shigoma, mkazi wa kijiji cha Kasitu, alisema kutokana na kutokuwa na daraja katika eneo hilo, watu wamekuwa wakifa maji kwa kusombwa na maji.

Alisema hali hiyo imekuwa ikijitokeza mara kwa mara hasa katika nyakati za masika kwa kuwa mto huo hujaa maji.

Shigoma aliiomba serikali kuwajengea daraja katika eneo hilo ili kuepukana na vifo vinavyotokea mara kwa mara kwa kuwa wamekuwa hawajisikii vizuri kushuhudia watu wakipoteza maisha kila nyakati za masika.

Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, Gasper Kateka, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kuongeza kuwa awali hali ilikuwa mbaya zaidi kwa kuwa hakukuwa na hata hicho kivuko lakini kilipatikana baada ya wananchi kujichangisha Sh. 10,000 kila mmoja kwa ajili ya kuwalipa mafundi waliokitengeneza. Diwani wa kata hiyo, Richad Kamagari, alisema tatizo la vifo kutokana na kutumbukia watu mtoni limekuwa likijitokeza mara nyingi na yeye amekwisha toa taarifa katika Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo.

Kwa upande wake Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya ya Kalambo, Mahmood Shauri, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusema kuwa serikali itajitahidi kutatua changamoto hiyo inayowakumba wakazi wa kijiji hicho.

# Wakosoa vifurushi vipya bima ya afya

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WANANCHI mkoani Manyara wamekosoa vifurushi vilivyotangazwa hivi karibuni na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kwa madai kwamba gharama hizo hazijazingatia hali za wananchi wa chini.

Kutokana na hali hiyo, wameiomba serikali kuwalipia wananchi kwa kuwa gharama zilizoainishwa zitawafanya wananchi wengi wa chini kushindwa kuzimudu.

Walitoa kasoro za vifurushi hivyo juzi mjini Babati wakati wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti juu ya maoni yao kuhusu vifurushi hivyo.

Mkazi wa Babati, Musa Rehani, alisema gharama ya chini ya Sh. 192,000 kwa mtu mmoja ambacho ni kifurushi cha 'Najali Afya' ni kubwa kwa mwananchi wa kawaida na gharama hiyo haina uhalisia.

Rehani ambaye ni mstaafu, alishauri kuwa bima hiyo wananchi wa chini walipie Sh. 5,000 kila mwezi ili kukamilisha kiwango cha fedha kinachotakiwa.

"Hiyo fedha ya Sh. 192,000 labda ikilipwa na mtu iwe ni ya bima ya maisha, lakini si kumlipisha mtu kila mwaka," alisema Rehani.

Pia alisema siku hizi afya na elimu nchini imekuwa biashara badala ya huduma kama ilivyokuwa zamani kwa mtu akiugua anatibiwa bure hata kama ameokotwa anatibiwa bila shida.

"Serikali iangalie watu wa hali ya chini iwalipie hiyo bima watu wote hao iwe kama enzi za Nyerere ambapo tulipata huduma bure mfano tulifanyiwa operesheni bure si kama siku hizi," alisema.

Mstaafu huyo alisema serikali ina vyanzo vingi vya mapato hivyo ingebeba mzigo wa kuwalipia watu wake gharama za bima kwa kuwa wako wafanyabiashara wakubwa wanalipa kodi wangezifidia.

Kuhusu wazee kutibiwa bure, alisema hakuna kitu kama hicho labda wanachoambulia ni kutopanga foleni na kuambulia kupewa paracetamol tu.

Katibu wa Baraza Kuu la Waislam Tanzania (Bakwata) Mkoa wa Manyara, Juma Mkola, akizungumzia vifurushi hivyo, alisema wananchi

INAENDELEA UK. 8

# Ruwa'ichi ataka amani ilindwe

**Na Mwandishi Wetu**

ASKOFU Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki Dar es Salaam, Thadeus Ruwa'ichi, amesema amani ya nchi inatakiwa kuambatana na utoaji haki, usawa na utekelezaji wa majukumu yote kwa usawa.

Akizungumza baada ya misa ya Krismasi iliyofanyika katika Kanisa la Mtakatifu Joseph jijini Dar es Salaam, Askofu Ruwa'ichi, alisema amani ni zawadi iliyotolewa na Mungu, hivyo jukumu la kila Mtanzania kuitunza.

Pia alisema kuna haja taifa kuombewa kwa taifa kuelekea uchaguzi mkuu wa mwakani.

Katika salamu zake, Askofu huyo alisema wakati taifa lilisherehekea kuzaliwa kwa Masia, Yesu Kristo, Watanzania wanatakiwa kuhimiza na kuombea haki, amani na upendo kuelekea uchaguzi huo.

Alisema ujumbe mkuu wa sikukuu ya kuzaliwa Kristo, yaani Krismasi kama ulivyosambazwa na malaika wakati wa kutangaza kuzaliwa kwake, ulikuwa 'amani na upendo' duniani, mambo ambayo msingi wake ni uwapo wa haki.

Alisema wakati Watanzania wakimaliza mwaka huu salama, suala la muhimu ni kuhakikisha kila mmoja anavuka salama kwa kuangalia umuhimu wa mapatano, ambapo kwa wale waliokoseana, wanatakiwa kuangalia namna ya kuombeana na kila mmoja kumjali mwenzake.

"Mambo haya ni muhimu na tunavuka mwaka na kuingia mwaka 2020, ambao tunaelekea kwenye uchaguzi mkuu kama taifa. Suala la muhimu ni kuliombea taifa, tuhakikishe tunafuata misingi ya haki, nina uhakika tutavuka salama.

"Ninachowasihi Watanzania, tusikiuke sheria, kila mmoja awe mtulivu. Kanuni zipo, asiwapo wa kupenda kupata madaraka kwa nguvu, tufuate kanuni na kusimamia haki. Nchi yetu ni nzuri na tukiweka mbele upendo, tutavuka salama," alisema.

Alisema ni jukumu la Watanzania na watu wenye mapenzi mema kuombea taifa na kuombea amani duniani na kwamba ni vyema kuchukuliana kwa upole, kwa kila mmoja kumjali na kumwombea mwenzake, hata pale anapopungukiwa kidogo.

Alisisitiza kuwa maisha yaliyo bora ni yale yanayoheshimu na kulinda amani na kujenga upendo, katika misingi ya kusimamia haki, ili kujenga furaha kuanzia katika ngazi ya familia.

"Lakini, ili kuwa na mafanikio na kushuhudia uwapo wa Mungu, yote haya, ya haki, amani na upendo yanatakiwa kuanzia kwa mtu mmoja mmoja, kuonyesha juhudi katika kutafuta amani. Hii amani ikiwapo ndiyo inayotupatia furaha kuanzia kwa mtu mmoja, familia na hatimaye taifa," alisema.

Askofu Ruwa'ichi pia alisema Watanzania wanatakiwa kutunza mazingira yanayowazunguka ili kuepuka majanga yanayoweza kujitokeza.

"Tunapoelekea kuhitimisha mwaka huu na kuanza mwaka ujao 2020, itakuwa ni fursa ya kijitathmini tulivyoenenda 2019 na kujitahidi kupambanua malengo, mipango na vipaumbele vyetu ili tupige hatua katika maisha yetu," alisema.



Wafanyabiashara ndogo maarufu Machinga wakiendelea na biashara zao zilizopangwa kwenye mbao juu ya mtaro wa maji ya mvua, eneo la Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Malasusa awapa dawa wenye huzuni

**Na Mwandishi Wetu**

ASKOFU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Dk. Alex Malasusa, amewataka Watanzania kuendelea kutafakari nuru na amani inayoangazwa na Yesu Kristo, akieleza kuwa dunia imebaki kuwa ya shaka na wengi wamebaki kuwa na huzuni ya mara kwa mara.

Askofu Malasusa aliyasema hayo jijini Dar es Salaam jana wakati wa ibada ya Krismasi iliyofanyika katika Kanisa la Azania Front.

Alisema kila wakati, wengi wamebaki na huzuni ya mara kwa mara, lakini ipo nuru inayoletwa na Yesu Kristo ambayo inatakiwa kuendelea kuiangaza.

Alisema kutokana na hali hiyo, maombi yake katika Sikukuu ya Krismasi mwaka huu iwe ya kipekee katika maisha ya kiroho na wala isiwe tu ya kupita, bali iwe ya kuenziwa na kila mtu.

"Dunia imebaki kuwa ya mashaka kila wakati, wengi wamebaki na huzuni mara kwa mara, lakini ipo nuru tuendelee kuiangaza. Hivyo, maombi yangu Krismasi ya mwaka huu iwe ya kipekee katika maisha ya kiroho, isiwe tu ya kupita," alisema.

Alisema Mungu anapozaliwa katika maisha yao, giza linaondoka, kwa kuwa yeye ni nuru ya ulimwengu, hivyo kama unahitaji pendo na amani ya kweli, ni lazima kukabidhi maisha yako kwa Mungu.

Aliongeza kuwa kuna hatua muhimu ya kurekebisha maisha ya mwanadamu ikiwa ni pamoja na kujikomboa na kwamba ukombozi ni wa kuondokana na vifungo vya shetani.

Pia, alisema dunia imejawa na mambo mengi, lakini Yesu ndiyo njia na jibu la uzima na yeyote anayetaka kuishi njia yake yenye mwanga na nuru, ni lazima kumpenda.

## Aonya wanaoshabikia utoaji mimba, 'unga'

**Na Elizabeth Faustine,** MWANZA

UTOAJI wa mimba, matumizi ya njia za kudhibiti mimba, dawa za kulevya na mafarakano katika ndoa, yametajwa kuwa baadhi ya matendo ambayo watu wanayashabikia bila kujua kuwa wanatenda dhambi.

Kauli hiyo ilitolewa na Paroko wa Parokia ya Familia Takatifu Nundu, Jimbo Kuu la Mwanza, Padri Moses Mapela, wakati wa misa ya mkesha wa Krismasi.

Alisema vijana wa sasa pia wanatumia vilevi vinavyowafanya washindwe kufanya kazi huku wengine wakiona kutoa mimba ni jambo la kawaida.

"Leo watu tunashabikia utoaji wa mimba, tunaua watoto wachanga wasio na hatia, tena kwa kukusudia, tunatumia dawa za kudhibiti mimba mradi tuwe huru na bado tunafika hatua tunasema ni haki ya msingi ya mwanamke, haya ni matendo ya giza," alikemea.

Padri Mapela alisema katika zama hizi, watu wanadhulumiana, wanauana, wanatesana na kuoneana vijicho, katika familia amani hakuna, ugomvi kila wakati, na muda mwingine wazazi wanagombona mbele ya watoto.

Alisema katika zama hizi, wazazi pia hawawafundishi watoto wao maadili mema na kuongeza kuwa matendo hayo ndiyo yanarudisha watu kwenye giza totoro.

"Wanandoa wakati mwingine tunaishi familia moja, hatuongeleshani, hatusemeshani, na wakati mwingine baba au mama anapofika nyumbani, anajisikia na kujiona kana kwamba sasa amejikabidhi tena katika Gereza la Butimba au Segerea ama la Keko, kwa sababu ndani hakuna upendo, furaha, maelewano. Sasa hii utaiita ni familia, au ndoa ama ndoana?" Alihoji.

Alisema katika familia zinapaswa kuishi kwa amani, furaha na kufurahia uwapo wa mwanafamilia, huku baba na mama wanapowaona watoto wawapende, wawathamini na kuwajali na kuwapa mafundisho yatakayowatoa gizani na kuwapeleka kwenye mwanga.

"Kuzaliwa kwa mwokozi, kuzaliwa kwa masihi, kutufundishe sasa kuishi kwa amani, upendo na mshikamano kama ambavyo tunavyoiona familia takatifu ya Yesu, Maria na Yosefu," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uanzishaji madawati ya jinsia elimu ya juu utekelezwe haraka

**UNYANYASAJI** wa kijinsia ikiwamo rushwa ya ngono katika vyuo vya elimu ya juu, vimekuwa vikiripotiwa mara kwa mara nchini na hata kusababisha taswira na hadhi ya taasisi hizo kuporomoka.

Hivi karibuni, mathalan, kumekuwapo na taarifa za kukithiri kwa vitendo hivyo katika baadhi ya vyuo, hatua ambayo iliwafanya wanaharakati kuingilia kati na kutaka uchunguzi ufanyike na wale wanaobainika kujihusisha na vitendo hivyo wachukuliwe hatua.

Miongoni mwa vyuo ambavyo vilitajwa hivi karibuni kuwa vinara wa vitendo hivyo ni Mtakatifu Augustino (Saut), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE). Katika taasisi hizi na nyinginezo, ilidaiwa kuwa baadhi ya wanataaluma wamekuwa wakiwataka wanafunzi wa kike kufanya nao mapenzi ili wawasaidie kufaulu mitihani ya vyuo.

Kutokana na kuwapo kwa tuhuma hizo, serikali iliingilia kati na kukemea kwa juhudi zote huku ikionya kuwa haitakuwa na msalie mtume na watu wote watakaobainika kujihusisha na aina hiyo ya rushwa ambayo ni sehemu ya ukatili wa kijinsia. Tunasema ni ukatili wa kijinsia kwa sababu mhusika (mwanafunzi) analazimishwa kufanya tendo la ndoa bila ridhaa yake na matokeo yake ni kumwondolea utu wake.

Hivi karibuni, wakati wa mkutano wa wakuu wa taasisi za elimu ya juu uliofanyika jijini Dodoma, serikali ilikunjua tena makucha yake na kukemea kwa nguvu zote kuandelea kukithiri kwa vitendo hivyo.

Katika ufunguzi wa mkutano huo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto anayeshughulikia Maendeleo ya Jamii, Dk. John Jingu, aliwapasha bayana wakuu hao juu ya vitendo hivyo vya aibu.

Bila kuuma maneno, Dk. Jingu ambaye kabla ya kushika wadhifa huo alikuwa mhadhiri UDSM, alisema vitendo hivyo vimeitia nchi doa baya na kuifanya sekta ya elimu hasa ngazi ya elimu ya juu kudharauliwa na kuchafuliwa.

Licha ya taasisi hizo hadhi yake kuporomoka, alisema rushwa ya ngono inasababisha kushuka kwa elimu kwa sababu ya kuzalisha wasomi ambao hawana sifa wala uwezo wa kushindana katika soko la ajira.


Sambamba na hilo, kiongozi huyo alisisitiza kwamba rushwa hiyo inasababisha hata kuporomoka kwa uchumi, hivyo kwa kuzingatia hayo, vitendo hivyo vya aibu havina budi kukomeshwa.

Hata hivyo, akifunga mkutano huo juzi, Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Francis Michael, alitoa sehemu ya suluhisho la kuimaliza kashfa hiyo kwenye ngazi hiyo ya juu ya elimu nchini. Katika hotuba yake, Dk. Michael alisema njia mojawapo ya kukabiliana na vitendo hivyo ni kuanzishwa madawati ya jinsia katika taasisi hizo.

Wazo hilo ni mwafaka kwa sababu litasaidia kwa kiasi kikubwa kupambana na vitendo hivyo kwa sababu wale watakaonyanyaswa, watakuwa na nafasi ya kuripoti matukio hayo ya aibu na hatimaye hatua kuchukuliwa.

Suala hilo halina budi kutekelezwa kwa haraka kwani ni imani yetu kwamba licha ya kupunguza vitendo hivyo, litasaidia kuwafichua wale wote wanaoendeleza uovu huo na kuchukuliwa hatua stahiki.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Staili hii enyi Machinga ni hatari kwa usalama wenu

**BAADHI** ya wafanyabiashara wadogo wa Kimara Mwisho, Dar es Salaam wako katika hatari kutokana na kufanya shughuli zao, chini ya nyaya kubwa za umeme wakati wa usiku.

Muda mrefu, Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco), lilishaweka tangazo la kupiga marufuku wafanyabiashara wadogo kufanya shughuli zao eneo hilo, kwa vile ni hatari kwa usalama wao.

Kuanzia asubuhi hadi jioni huwa hawaonekani kwenye eneo hilo, lakini inapofika usiku ndio wanamiminika kwa wingi wakiendelea na biashara kama kawaida, kana kwamba muda huo hakuna hatari inayoweza kuwapata.

Hatua zilizochukuliwa na Tanesco, inalenga kuwaondoa mahali hapo na kuwaacha wafanye salama, kwani ukweli unabaki palepale, kwamba eneo hilo ni hatarishi. Mtindo wa kuvizia hadi usiku ni sawa na kudanganya usalama binafsi.

Ndugu zangu hawa, pamoja na kutambua ukweli wanatafuta maisha, bado wangepaswa kuzingatia usalama wao kwanza. Ukweli usiopingika, uhai ni zaidi ya biashara zao, kwani walioamua kuwaondoa kwenye eneo hilo wanajua madhara yake na vyema wakazingatia maoni yao kwa ajili ya usalama wao, sasa na baadaye.

Yapo mengine ya kupuuzia kuliko hilo, ambalo linagusa uhai wao na hivyo suala la visingizio kwamba 'wakafanye biashara wapi' lisiwe na nafasi vichwani mwao, kwani mchana huwa wako wapi?

Ninasema hivyo, kwa sababu imekuwa kawaida kwa baadhi ya wajasiriamali na wachuuzi wadogo, wanaojenga tabia ya kuhoji swali kama hilo, mara wanapotakiwa kuhama kwenye maeneo ambayo siyo rasmi kwa shughuli zao.

Wapo waliokwishawahi kuhoji kwamba 'wakafanyie biashara zao wapi' baada ya kuondolewa chini ya nyaya za umeme eneo la Ubungo, bila ya kuhoji upande wa pili kuhusu hatari iliyowakabili.

Hatari inayowanyemelea ni kubwa zaidi, ingawa zipo nyingine kama za kufanya biashara kando ya barabara na kutupa taka ovyo kwenye maeneo mbalimbali na kuchafua mazingira. Umefika wakati, wafanyabiashara wenyewe wajiongeze na kuchukua hatua haraka kabla ya kukumbwa na madhara na kuanza kulalamika kwamba 'serikali imewaacha' na kumbe tatizo liko kwao wenyewe.

Watambue kwamba, eneo hilo chini uya nyaya ni hatari zaidi kwa usalama wao wakati wote, siyo kwamba halifai mchana na kisha usiku linafaa, hapa wenye mawazo hayo watakuwa wanajidanganya.

Ni vyema wakaogopa hatari inayoweza kuwapata kuliko kuiogopa Tanesco, ilikwishaamuru watoke katika eneo hilo, kwa ajili ya usalama wao na wakawekewa bango linaloonyesha hatari inayoweza kuwapata.

Kitendo cha wao kufanya biashara usiku, kinaonyesha kwamba wanahofu hatua za watumishi wa Tanesco kuwakuta na inapotimia usiku, wanajua kuwa siyo muda wa kazi hivyo watumishi hao hawawezi kufika eneo hilo.

Hapa jambo la msingi ni kuepuka hatari inayoweza kusababishwa na nyaya hizo, siyo watumishi wa Tanesco, hivyo wamachinga watafakari na kuchukua hatua haraka za kutorudi kwenye eneo hilo hatarishi. Vilevile, wenye jukumu la kuboresha masoko ya wafanyabiashara wadogo, waharakishe kufanya kazi hiyo, ili kusaidia kuepusha hatari inayonyemelea wale wanafanyia biashara kwenye maeneo ya hatari.

Ucheleweshaji wa kuboresha masoko hayo, pia unaweza kuchangia kuinyima serikali mapato yanayotokana kodi au ushuru kutoka kwa wafanyabiashara, ambao wamekuwa wakilalamikia ubovu wa masoko yao.

Kimsingi, kuna hatari zinazoweza kusababishwa na mambo matatu niliyoyataja awali. Hivyo, suala la kuwapo masoko rasmi ya wamachinga ni jambo la msingi.

Pia usafi wa mazingira kwenye maeneo yanakofanyia biashara, ikizingatiwa kuna baadhi ya wafanyabiashara wanadiriki kujisaidia haja ndogo katika chupa za plastiki na kuzitupa ovyo mitaroni.

Wengine wanapanga biashara zao kwenye mitaro au kuchimba kingo za barabara na kuweka vibanda kwa ajili ya kuweka bidhaa wanazouza.|

Ni mtindo unaochukua nafasi kwa biashara za kando ya barabara, ambayo nayo siyo salama, kwani ni jirani na mazingira ya ajali. Gari linaweza kupata tatizo na kumshinda dereva, matokeo yake ni kuwavaa wafanyabiashara walioko hapo.

Hivyo, ni vyema ndugu hao wajitahidi kufanya shughuli zao kwenye mazingira salama, badala ya kulzimisha hata pale pasipofaa na mwisho wa siku wanaangukia kwenye matatizo na kulalamika kwamba hawasaidiwi.

# HABARI KATIKA PICHA



Mchungaji Emmanuel Masoud wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Zanzibar, akimbatiza mtoto wakati ya ibada ya mkesha wa Krismasi iliyofanyika kwenye Kanisa la Anglikana Mkunazini Zanzibar juzi. **PICHA: MARTIN KABEMBA**



Msaidizi wa Askofu Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi Dodoma, Mchungaji Christian Ndossa, akiwatakia baraka waumini wa kanisa hilo, Mtaa wa Kisasa jana, baada ya ibada ya Krismasi iliyofanyika katika kanisa hilo jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Baadhi ya waumini wa Kikristo Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Mtaa wa Kisasa wakishiriki ibada ya Krismasi ambayo husherehekewa kila mwaka Desemba 25, ikiwa ni kumbukumbu ya kuzaliwa kwa Yesu Kristo zaidi ya miaka 2000 iliyopita. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Askofu wa Kanisa la Angalikana Dayosisi ya Central Tanganyika, Dk. Dickson Chilongani (aliyeshika fimbo), akisalimiana na Balozi mstaafu Job Lusinde, baada ya kumalizika kwa ibada ya Krismasi iliyofanyika jana, Dodoma. **PICHA: PETER MKWAVILA**



Waumini wa Kanisa Katoliki wakifuatilia ibada ya mkesha katika Kanisa la Mt. Joseph mjini Zanzibar, jana. **PICHA: MARTIN KABEMBA**



Wanafunzi wanaosomea utawa wakiwa kwenye mkesha wa sikukuu ya kuzaliwa Yesu Kristo (Krismasi), iliyofanyika katika Kanisa Katoliki la Mama Mwenye Huruma, Ngokolo, Shinyanga Mjini. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Watalii 450 kutoka Israel watua nchini

**Na Mwandishi Wetu**

WATALII zaidi ya 450 kutoka Israel wamewasili nchini mwezi huu kutembelea vivutio vya kitalii vilivyoko kaskazini mwa Tanzania, wakitumia ndege binafsi na za kawaida.

Imeelezwa kuwa kundi la kwanza la watalii 150 liliwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro (KIA) Desemba 21 na kupokewa na Bodi ya Utalii (TTB) na baadaye kwenda katika vivutio vya utalii vilivyoko mkoani Arusha.

Kundi la pili na la tatu lililokuwa na watalii 305 liliwasili nchini kupitia uwanja huo juzi.

Watalii hao wako nchini kwa ajili ya kusherehekea sikukuu za Krismasi na mwaka mpya na wanatembelea Hifadhi za Taifa za Serengeti, Tarangire, Ziwa Manyara, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorogoro na Bonde la Eyasi.

Ubalozi wa Tanzania nchini Israel umetoa viza zaidi ya 500 kwa Waisrael ambao wamepanga kuwasili nchini kwa kutumia Mashirika ya Ndege ya Ethiopia, Uturuki na Uswisi katika kipindi hiki cha siku kuu za mwisho wa mwaka huku ukiendelea kuratibu ziara nyingine ya watalii zaidi ya 800 ambao mchakato wa safari yao upo katika hatua za mwisho.

Ujio wa watalii hao unatokana na jitihada za kuvutia watalii zinazofanywa na Ofisi ya Ubalozi nchini Israel kwa kushirikiana na kampuni ya wakala wa utalii ya ndani na nje ya nchi ili kuunga mkono harakati za serikali za kukuza pato la taifa kupitia utalii na hivyo kuiletea nchi maendeleo.



Gari likipita karibu na shimo lililowekewa alama ya tairi kama tahadhari Mtaa wa Sokoine jijini Dar es Salaam jana.
**PICHA: JUMANNE JUMA**

# Lissu aanika mbinu 5 za kuing'oa CCM 2020

INATOKA UK. 4

na wenzetu na maslahi yao vilevile," Lissu alitahadharisha.

Vilevile, alisema ni muhimu kwa chama hicho kuimarisha diplomasia ya kimataifa itakayowawezesha kuwa na ushirikiano na vyama kutoka mataifa mengine katika kujifunza mbinu za kisiasa kutoka katika vyama hivyo kwa kuzingatia kuwa Sheria ya Vyama vya Siasa nchini haijakataza ushirikiano baina ya vyama na asasi za kimataifa, hivyo si sahihi kuita ushirikiano huo kuwa ni usaliti ilhali umeruhusiwa kisheria.

Katika kutekeleza hilo, Lissu aliwataka viongozi wenzake ndani ya chama hicho kujiandaa kushiriki katika mijadala na mabaraza ya kimataifa ili kupata uzoefu na kujiimarisha kusiasa sambamba na kuimarisha diplomasia ya chama hicho katika kiwango cha kimataifa.

Vilevile, mbunge huyo wa zamani wa Singida Mashariki, alisema ni muhimu kujiendaa kifedha kukabiliana na uchaguzi mkuu wa mwakani ili kufanikisha ushindi wa chama, akiwaomba wanachama wa chama hicho kukichangia kama mojawapo ya mikakati ya kufanikisha ushindi. Alisema uchaguzi ni gharama na kuna haja chama hicho kufanya kampeni ya kukichangia ili kiwe vizuri kifedha kuelekea uchaguzi huo.

Lissu (51), amekuwa nje ya mipaka ya Tanzania kwa takribani miaka miwili sasa baada ya kushambuliwa kwa kupigwa risasi na watu wasiojulikana wakati akijiandaa kushuka kwenye gari nyumbani kwake Area D jijini Dodoma muda mfupi baada ya kumalizika kwa kikao cha mchana cha Bunge, ambacho alichangia hoja.

# Askofu Shoo aonya kutesana

INATOKA UK. 2

akachelewa kwa ajili hiyo na wakati huo mvua ilikuwa inanyesha. Basi yule baba kwa hasira akampiga yule mama teke, chakula kikamwagika kilikuwa kwenye chungu na wakalala njaa usiku ule," alisema.

Dk. Shoo ambaye ni Askofu wa Dayosisi ya Kaskazini, alisema kwa watu ambao wamempokea Yesu moyoni, kiburi hakipo na hawana sababu ya kuwa na kiburi, wala hakuna sababu ya kujivuna.

"Mali ina nafasi katika jamii, kwa hiyo inaweza ukajifanya ukajisifu, ukawa na kiburi. Yesu aliyezaliwa kwenu akajinyenyekesha Krismasi hii, ndugu yangu mwambie Mungu akusamehe pale ulipokuwa na kiburi.

"Usitafute yaliyo makuu zaidi ya uwezo wako, utaweza kujua maana ya kukaa ndani ya neema ya Mungu. Na hapa kipekee napenda kutoa ujumbe kwa ndugu zetu wale ambao wanahusika kwenye kupeleleza kesi za watu na mahakimu na majaji simamieni ukweli.

"Vilio vya watu wanaobambikwa kesi na familia zao, vilio hivi ndugu zangu, wako waliohukumiwa pasipo ukweli wa kutenda kosa, vilio hivi ndugu zangu Mungu anavisikia kama alivyosikia vilio vya wana wa Israel kule utumwani.

"Ninyi mliopewa mamlaka ni lazima mjue kwamba ni wajibu wenu kusimamia haki, kwa maana tunaambiwa na maneno matakatifu kwamba tutawajibika kwake kujiridhisha kweli na mtoa hukumu zisizo za haki," alionya.

# Wakosoa vifurushi vipya bima ya afya

INATOKA UK. 4

wanawasumbua tu ili wapate fedha watu wa NHIF maana hata wanaolipia bima hawapati dawa.

"Wanatuambia eti dawa zipo ni maneno tu. Kama wanataka kutusaidia kwa nini wasiwaambie watu hiyo fedha wakaitoa kwa awamu tofauti," alisema Mkola.

Alisema bado kuna udanganyifu mkubwa kwenye upatikanaji wa dawa na dawa nyingi zinatoroshwa na madaktari kwenda kuziuza kwenye maduka yao ndiyo maana wanawaambia wagonjwa waende kununua dawa duka fulani.

Kiongozi huyo wa dini anamshauri Rais kuwatuma wasaidizi wake kama wakuu wa mikoa na mawaziri kulifuatilia jambo hilo kwa siri ili wabaini madaktari wanaohujumu dawa.

Akizungumzia vifurushi hivyo, Meneja wa NHIF Mkoa wa Manyara, Hance Mwankenja, alisema vifurushi hivyo vimeanzishwa kwa nia ya kuwasaidia wananchi.

Mwankenja alivitaja vifurushi hivyo kuwa ni 'Najali Afya' ambacho ni Sh. 192,000 ambacho kinamhusu mtu mwenye miaka 18 hadi 35 kwa kulipa mwaka mzima, 'Wekeza Afya' ambacho ni Sh. 384,000 kwa mwaka na kinamhusu mtu wa miaka 36 hadi 59 na kingine ni 'Timiza Afya' ambacho ni Sh. 516,000 kwa mwaka kinawahusu watu wa miaka 60 na kuendelea.

Mwankenja alisema watu wanachagua kifurushi kulingana na uwezo na kupata vifurushi hivi zimepigwa hesabu za kitaalamu kwa kuangalia makundi tofauti ya watu.

Aliongeza kuwa wananchi wasiangalie gharama za vifurushi bali waangalie huduma zinazopatikana na wakumbuke matibabu ni gharama sana.

## HABARI KITAIFA

# DC apiga 'stop' unyago, sherehe la saba

**Na Stevie Chindiye,**
TUNDURU

MKUU wa Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma, Julius Mtatiro, amepiga marufuku shughuli za unyago pamoja na kuwafanyia sherehe watoto wanaomaliza darasa la saba.

Mtatiro alitoa amri hiyo juzi wakati akizungumza na viongozi wa vyama vya msingi vya wakulima (Amcos) wilayani hapa katika kikao kilichofanyika katika ukumbi wa Klasta ya Walimu wa Tarafa ya Mlingoti mjini hapa.

Alisema marufuku hiyo ni kuanzia mwakani na endapo mzazi au mlezi atakiuka amri hiyo, atakutana na mkono wa sheria.

Ili kudhibiti hali hiyo Mtatiro alimwagiza Mkuu wa Polisi Wilaya ya Tunduru kusambaza polisi katika maeneo ya tarafa, kata na vijiji vyote ili kuwakamata wananchi ambao watakaidi agizo hilo.

Alisema kufanya sherehe za aina hiyo ni kuukaribisha umaskini ndani ya nyumba na familia kwa ujumla.

"Mtoto amemaliza darasa la saba ni sawa na ziro, ni mzigo pia, lakini cha kushangaza wazazi na walezi huenda kurundikana shuleni na kuwasubiri watoke na kuwafanyia sherehe na kupiga ngoma. Tabia hizo huwabweteesha watoto na kuwafanya wasiwe na uwezo wa kufikiria hatima ya maisha yao," alisema.

"Haiwezekana serikali iendelee kufumbia macho vitendo vya aina hiyo ambavyo wazazi wamekuwa wakivifanya kwa makusudi ikiwamo kuwafundisha watoto wadogo wa kike mafunzo ya utayari wa kuwahudumia wanaume," alisisitiza Mtatiro.

Alisema shughuli hizo ambazo wananchi wamekuwa wakisingizia mila za asili ya makabila yao, zinatakiwa kutolewa kwa watoto wa kike ambao wamepevuka na ambao hawasomi lakini kufanywa kwa vitoto ni vya ukatili wa kijinsia unaokiuka haki za watoto.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, baadhi ya washiriki wa mkutano huo walikiri kuwapo kwa vitendo hivyo miongoni mwao na kwamba marufuku hiyo itasaidia watoto kusoma.

Walisema ufumbiaji macho wa matukio ya aina hiyo pamoja na maelekezo ya kuwataka watoto wao wasifanye vizuri katika mitihani ya kumaliza darasa la saba kutoka kwa wazazi na walezi, umekuwa ukiharibu mwenendo wa masomo ya watoto wao jambo ambalo limekuwa likisababisha watoto kukithiri kwa mimba za utotoni.



Waziri wa Mambo ya Nje mstaafu, Bernard Membe (kushoto), akisalimiana na Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Yuda Thadeus Ruaichi, baada ya ibada ya Krismasi iliyofanyika jana katika Kanisa Kuu la Mtakatifu Joseph, Dar es Salaam jana. **PICHA NA JUMANNE JUMA**

# Upungufu damu wajawazito wapungua

**Na Happy Severine,** BARIADI

IDADI ya kinamama waliokuwa na upungufu wa damu wakati wa kujifungua umepungua kwa kiwango kikubwa kutokana na ongezeko la matumizi sahihi ya virutubisho vya madini chuma.

Idadi hiyo imepungua kutokana na uhamasishaji na elimu ya mara kwa mara inayotolewa kwao pindi wahudhuriapo kliniki kupitia mpango wa 'Right Start' unaoendesha na Shirika la Utafiti wa Afya Afrika (Amref).

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Masewa, Dk. Elina Julius, alisema hayo juzi alipotembelewa na uongozi wa Amref pamoja na wadau mbalimbali kutoka Ofisi ya Rais (Tamisemi), afya, elimu na wenyeviti wa halmashauri kutoka mikoa ya Mwanza na Simiyu kwa lengo la kujionea hali halisi.

Alisema awali walikuwa wakipata matukio mengi ya kinamama kupungukiwa na damu hasa wakati wa kujifungua hali ambayo ilikuwa ikisababishwa na matumizi hafifu ya madini chuma.

"Hapo awali tulikuwa tukipata shida, kinamama wengi walikuwa wanapungukiwa na damu nyingi kutokana na kutotumia lishe bora na madini chuma, lakini kwa sasa hilo tatizo halipo," alisema.

Dk. Julius aliongeza kuwa kwa sasa kati ya wajawazito 90 wanaojifungua kila mwezi katika kituo hicho ni wawili tu ndio wanaokutwa na upungufu wa damu na kukiri kufanikiwa kupunguza tatizo hilo.

Naye Ofisa Lishe Mkoa wa Simiyu, Chacha Magige, alisema katika kutekeleza mpango wa 'Right Start' wanakutana na changamoto ya mila potofu zilizoko miongoni mwa wazazi wengi mkoani hapa ambao wanakataa watoto wao kupatiwa madini hayo.

Alisema wazazi wengi wametawaliwa na mila potofu juu ya utumiaji wa madini chuma, huku wakidai endapo watatumia, watakuja kukosa watoto pindi watakapohitaji kuzaa.

"Tumekuwa tukikumbana na mila potofu juu ya matumizi ya madini chuma kwa watoto wa kike. Wengi wanadai watoto wao watakuja kukosa watoto baadaye, hivyo wanawazuia kutumia," alisema Magige.

Alisema sababu ya kuanzishwa kwa programu ya utoaji virutubisho vya madini chuma kwa watoto wa kike kupitia mradi huo ni kutokana na mabadiliko ya mfumo wa ulaji ambao umesababisha upungufu wa damu kwa wasichana ambao muda mwingi hupoteza damu nyingi wakati wa hedhi.

# Walalamikia wingi wa taka

**Na Neema Hussein,**
MPANDA

WAKAZI wa Kata ya Makanyagio Manispaa ya Mpanda, mkoani Katavi, wameulalamikia uongozi wa manispaa hiyo kwa kushindwa kupeleka gari la uzoaji taka kwa takribani miezi mitatu sasa.

Hatua hiyo, kwa mujibu wa wananchi hao, imesababisha kukithiri kwa uchafu katika eneo hilo, hivyo kutishia usalama wa afya zao.

Wakizungumza na Nipashe juzi, wakazi hao walisema hali hiyo husababisha hata kuziba kwa mitaro ya maji wakati wa mvua kutokana na baadhi ya watu kutupa taka kwenye mitaro hiyo.

"Gari la taka siku hizi halipiti kabisa, ni zaidi ya miezi 3 sasa. Taka zimekithiri kwa kweli wenye maeneo makubwa wanaamua kuchimba chini wanazifukia wengine wanazimwaga kwenye mitaro na mitaro inaziba, mvua ikija maji hayapiti," alisema mmoja wa wakazi hao ambaye hakutaka kutajwa jina lake.

Augustino Chambala, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mpadeko, alisema hali hiyo inatokana na kuwapo kwa gari moja tu manispaa nzima la kubeba taka, hivyo wameuomba uongozi uwape kibali cha kukodi gari binafsi kwa pesa zilizotolewa na wananchi Oktoba, mwaka huu, ili kunusuru tatizo hilo.

"Sisi baada ya kuona hali hii tulikaa kikao na viongozi wenzangu tukaamua kuomba kibali kwa viongozi wa juu ili tukodi gari binafsi kuja kubeba hizi taka. Kuna pesa iliyobaki ambayo walichanga wananchi mara ya mwisho kwa ajili ya kuja kubebewa taka," alisema Chambala.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Mpanda, Michael Zyungu, alipotafutwa kwa njia ya simu, alisema yuko nje ya mkoa na hana taarifa hizo, hivyo kuahidi kulifanyia kazi suala hilo.

Hata hivyo, Zyungu alikiri kuwa gari lililopo halitoshi kukidhi uwezo wa kuzoa takataka zinazozalishwa kwa siku huku akisema wana mpango wa kuongeza magari na kujenga dampo la kisasa kwa ajili ya kuhifadhi taka hizo.

# Tughe yalia na ada ya leseni

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

CHAMA cha Wafanyakazi wa Serikali Kuu na Afya (Tughe) kimelalamikia ongezeko la ada ya leseni kwa madaktari, wauguzi na wafamasia ambayo imekuwa kubwa na kuchukua thamani ya zaidi ya utaalamu walio nao.

Mwenyekiti wa Tughe Taifa, Archie Mntambo, alisema hayo juzi wakati wa Mkutano Mkuu wa chama hicho, uliomalizika mjini Morogoro.

Alisema licha ya kuunga mkono jitihada zinazofanywa na Rais John Magufuli na Waziri mwenye dhamana ya Afya, Ummy Mwalimu, kushughulikia changamoto na kuboresha mambo mbalimbali katika sekta hiyo, bado wanaamini wako watu wachache wanaowakwamisha kwa maslahi yao binafsi.

"Hatupingi uwapo wa leseni zinazotolewa na mabaraza haya ya kitaalamu yanayosimamia hawa wataalamu, lakini hii ada ni kubwa mno kulingana na utaalamu wanaoutoa hawa madaktari, wauguzi na mafamasia," alisema.

Mntambo alisema mkutano huo ambao hufanyika mara moja baada ya miaka mitatu, ulipitia pamoja na mambo mengine, malalamiko ya migogoro kati ya wauguzi na baraza la wauguzi na madaktari wa afya na wafamasia na mabaraza yanayowasimamia inayohusu ongezeko hilo la ada ya leseni wanayopata wataalamu hao baada ya kuhitimu mafunzo yao.

Alisema kinachoshangaza ni kuona mabaraza hayo yanaweka ada kubwa wakati yanajua kwamba mfanyakazi wa Tanzania mshahara wake haujapandishwa hali inayofanya wailaumu serikali wakati si uamuzi wake.

"Tuna imani kubwa na serikali na Rais wetu na waziri anayesimamia sekta ya afya. Lakini tunajua jambo hili linafanywa kwa maslahi ya wachache, hivyo hatutanyamaza kimya. Tunatoa rai kwa wote waliopewa mamlaka wanapofanya uamuzi unapogusa maslahi ya mtumishi, ni vyema watushirikishe," alisema.

Naye Katibu Mkuu wa Tughe, Henry Mkunda, alisema bado kuna mazingira mbalimbali katika sekta ya afya yanayofanya watumishi kukosa furaha ya huduma kutoka kwa wajiri wao, ikiwamo kufanya kazi katika mazingira magumu, kukosa likizo na malipo ya muda wa ziada.

Alisema ni vyema waajiri wakaruhusu kuwapo kwa vyama vya wafanyakazi maeneo ya kazi kwa kuwa baadhi wamekuwa wakizuia uwapo kwa vyama hivyo katika maeneo yao.

# RPC aapa kula na madereva walevi

**Na Hamisi Nasiri,** MTWARA

JESHI la Polisi mkoani Mtwara limewaonya madereva wa vyombo vya moto kuacha kutumia kilevi ili kuepusha ajali zisizotarajiwa hasa kipindi hiki cha sikukuu za mwisho wa mwaka.

Pia limeahidi kuimarisha maeneo yote ya mipakani kati ya Tanzania na Msumbiji ili kudhibiti watu wanaokusudia kuingia nchini kwa lengo la kufanya uhalifu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Blasius Chatanda, alitoa onyo hilo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kuelekea kipindi hiki cha sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya.

Alisema jeshi hilo halitawavumilia madereva wa vyombo vya moto ambao wataendesha huku wakiwa wamelewa.

Kamanda Chatanda alisema kumekuwa na tatizo la baadhi ya madereva mkoani Mtwara katika kipindi cha sikukuu kuendesha vyombo vya moto wakiwa wamelewa, hivyo kuonya kuwa jeshi hilo litawakamata.

Alisema Jeshi la Polisi limejipanga kufanya operesheni kabambe ya kuhakikisha katika kipindi hiki hakuna matukio ya ajali na uhalifu yatakayojitokeza.

"Tunaimarisha usalama wa raia na ajali za barabarani, lakini tunatoa onyo kwa madereva walevi kuacha kutumia vyombo vya moto wakiwa wametumia kilevi chochote," alisema.

Kwa mujibu wa Chatanda, katika kusherehekea Krismasi na Mwaka Mpya ni wakati wa kufurahi na si kupata ulemavu au umauti, hivyo madereva wanapaswa kutumia vyombo vya moto kwa uangalifu.

Chatanda alisema Jeshi la Polisi limeamua kujipanga kwa kuimarisha mipaka ya Tanzania na Msumbiji ili kudhibiti watu wenye nia ya kufanya uhalifu.

Alisema watahakikisha mipaka hiyo inakuwa salama na hakuna wahalifu wowote ambao watainngia kutoka Msumbiji kwa lengo la kufanya vitendo hivyo.

Kamanda huyo alisema jeshi hilo linawahakikishia wananchi kuwa na amani na kusherehekea sikukuu bila hofu ya aina yoyote.

Alisema katika kuhakikisha kunakuwa na amani na utulivu, doria itafanywa usiku na mchana huku akipiga marufuku disko toto kwenye kumbi za starehe kwa kuwa si salama kwa watoto.




Kiongozi wa kiroho wa Waislamu Shia Ithnasheriya Maulana, Sheikh Hemed Jalala, akitoa mkono wa baraka, fanaka na kheri kwa Wakristo kwa kusherehekea sikukuu ya Krismasi na Mwaka Mpya, leo, Masjid Ghadir, Kigogo Post Dar es Salaam, wakati akiongea na waandishi wa habari. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Achaguliwa mwenyekiti UVCCM Tunduru

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

MKUTANO Mkuu Maalum wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) wilayani Tunduru, umemchagua Hussein Mkuiya kuwa mwenyekiti wa jumuiya hiyo.

Akitangaza matokeo hayo, Msimamizi wa Uchaguzi huo, Abiniel Nzagule, alisema kuwa Mkuiya ameibuka mshindi kwa kupata kura 181. Nzagule alisema katika uchaguzi huo uliofanyika juzi, Mkuiya aliwabwaga wapinzani wake Amos Fusi aliyepata kura 64 na Innocent Mmole aliyapata kura 37.

Alisema katika uchaguzi huo ambao ulifanyika katika Klasta ya Walimu Tarafa ya Mlingoti mjini hapa, kura 313 zilipigwa huku kura halali zikiwa 292 na 10 ziliharibika.

Nzagule, ambaye ni Katibu wa CCM Wilaya ya Songea Vijijini, akitoa maelekezo ya uchaguzi huo, aliwataka wajumbe kuchagua kiongozi ambaye hatakuwa na makundi ndani ya jumuiya yao.

Naye Katibu wa CCM Wilaya ya Tunduru, Kite Mfilinge, aliwataka wajumbe wa mkutano hao kuchagua kiongozi bora ili kukisaidia chama katika uchaguzi mkuu ujao wa Rais, wabunge na madiwani.

Huseini Mkuiya amechukua nafasi hiyo ambayo iliachwa wazi na Mbemba Matola Mbemba ambaye kwa sasa ameajiriwa kuwa Mtendaji wa Kata ya Sisi kwa Sisi wilayani hapa.

# Askofu Massangwa: Maadui watatu bado tatizo Tanzania

**Na Allan Isack,** ARUSHA

ASKOFU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Kaskazini Kati, Dk. Solomon Massangwa, amesema bado wananchi wanakabiliwa na matatizo ya ujinga, maradhi na umaskini.

Matatizo hayo yalitajwa na Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere takribani miongo mitano iliyopita.

Askofu huyo aliyasema jana wakati wa ibada ya sikukuu ya Krismasi katika Kanisa la KKKT, Mtaa wa Mjini Kati Usharika wa Mjini Kati.

Alisema kutokana na matatizo hayo, wananchi wamepoteza tumaini la maisha, hivyo aliwataka kuwa na matumaini mapya kwa kuwa mkombozi amezaliwa upya katika maisha yao.

"Ujinga ni adui kwetu kwa kuwa anayejua kesho yake na mazingira tunayoishi wananchi, na Wakristo wanapenda kudanganywa kwa mambo yasiyowezekana.

"Mfano wa ujinga tunaouzungumzia, kwa sasa wamezuka manabii wa uongo ambao wanawadanganya watu, wawapelekee vitu vya thamani ili wawafanyie maombi na kuwatatulia shida zao," alionya.

Alisema tatizo lingine linalowasumbua wananchi ni umaskini na kuwa na kipato kidogo ambacho hakiwezi kukidhi mahitaji ya maisha yao.

"Umaskini ni tatizo kubwa kwa wananchi na wakristo wetu, mfano kuna mashirika yamekuja kutoka nje ya nchi yanawaambia watu wanaotaka kupata fedha, wanyooshe mikono na kuangalia juu halafu hela zitakuja na yote haya wanafanya kutokana na umaskini na ujinga," alisema.

Alisema wananchi pia wanakabiliwa na tatizo la kuwa na maradhi mbalimbali na wengi wao wameshakata tamaa, hivyo akawataka kuwa na tumaini la uponyaji. "Mwokozi wetu Yesu Kristo amezaliwa na wakristo tumefundishwa kumcha na kumsujudia kwa kuwa yeye ndiye mkombozi wa dhambi zetu.

"Mtume Paulo katika maandiko matakatifu, anasema tushukuru kwa kila jambo kwa kuwa ni mapenzi ya Mungu, ukipata kazi, msiba, mke, mume au ugonjwa tushukuru kwa kila jambo. "Yesu amezaliwa ili sisi tumwone Mungu, lakini tunapaswa kumsifu bwana aliyezaliwa katika maisha yetu na kutuletea ukombozi ambao haukuja kwa dhahabu bali ni kwa damu," alisema.



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, Dk. Maulid Madeni (kulia), jana, akimshika mkono Ofisa Elimu Sekondari wa Halmashauri ya Jiji hilo, Valentine Makuka, kama ishara ya kumkabidhi madawati na meza 3,900 vyenye thamani ya Sh. milioni 105 yaliotengenezwa na jiji kwa ajili ya kukalia wanafunzi wa kidato cha kwanza mwakani 2020. **PICHA : CYNTHIA MWILOLEZI**

# Aiomba serikali kuongeza madaktari kituo cha afya

**Na Mwandishi Wetu,** BABATI

BAADA ya kuboresha huduma za upatikanaji wa vipimo vikiwamo vya upasuaji katika Kituo cha Afya cha Magugu, Mganga Mfawidhi wa kituo hicho, Dk. Costa Ndunguru, ameiomba serikali kuongeza wafanyakazi ili kukabiliana na ongezeko la wagonjwa wanaojitokeza kupata huduma.

Akizungumza wakati wa ziara ya kutembelea kituo hicho ambacho ni miongoni mwa vilivyopata Sh. milioni 400 kwa ajili ya maboresho, Dk. Ndunguru alisema kwa sasa wanapokea wagonjwa 100 hadi 150 kwa siku, na muda mwingine wanazidiwa na wagonjwa kutokana na uchache wa watumishi.

Alisema kabla kituo hicho hakijafanyiwa maboresho ya huduma za afya, walikuwa wanapokea wagonjwa wasiozidi 500 kwa siku na walikuwa na uwezo wa kuwahudumia wote, tofauti na ilivyo kwa sasa.

Aliiomba serikali kuongeza idadi ya watumishi ili kukabiliana na ongezeko la wagonjwa ambao wanatoka katika vijiji saba vilivyopo ndani ya kata hiyo, na vijiji vingine vya jirani.

"Tunashukuru Mungu wagonjwa wetu wanapata huduma nzuri na bora, lakini watumishi wakiongezeka, huduma zitazidi kuimarika zaidi kwa wakazi wa kata hii ya Magugu na maeneo jirani," alisema.

Alibainisha kuwa dawa kwa saa si tatizo kwa kuwa wamekuwa wakipata dawa zinazohitajika kwa ajili ya matibabu ya wagonjwa wanaohudhuria katika kituo hicho.

Hata hivyo, alisema tatizo linalowakabili ni upungufu wa watumishi kulingana na ukubwa wa kituo hicho na ongezeko la idadi ya wagonjwa wanajitokeza kupata huduma za afya.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Babati, Hamisi Malinga, alisema serikali imetoa fedha kwa ajili ya kufanya maboresho ya kituo hicho na kuongeza baadhi ya majengo ambayo yamefanya huduma zao kuwa bora na kuvutia. Alisema kwa sasa wakazi wa eneo hilo hawapati shida ya matibabu kutokana na huduma zote za matibabu kupatikana.

"Tunaendelea kukiboresha kituo hiki kwa kujenga jengo la upasuaji ambalo lipo tayari kwa ajili ya kuanza kutoa huduma," alisema.

Mkazi wa Kata ya Magugu, Salum Omary, aliishukuru serikali kwa kuwekeza katika sekta ya afya nchini, akieleza kuwa kuboreshwa kwa kituo hicho kumesaidia kuokoa maisha ya watu wa vijijini.

Alisema awali walikuwa wakipata shida ya upatikanaji wa huduma za afya, hususani za mama na mtoto, lakini kwa sasa huduma hizo zinapatikana kwa urahisi na ukaribu.

Aliiomba serikali kuendelea kutoa kipaumbele katika sekta ya afya maeneo yote nchini, hasa vijijini.

# Wakazi 15,000 wanufaika na ujenzi wa zahanati

**Na Mwandishi Wetu,** BABATI

ZAIDI ya wakazi 15,000 wa vijiji vitatu vya Kata ya Ayalagaya, Halmashauri ya Wilaya ya Babati, wameondokana na tatizo la kutembea umbali wa zaidi ya kilomita 20 kutafuta huduma ya afya baada ya kujengewa zahanati ya kisasa na serikali kwa kushirikiana na Shirika lisilo la kiserikali la Karimu International Foundation.

Shirika hilo pia limesema linatarajia kutoa Sh. milioni 250 kwa ajili ya upanuzi wa zahanati hiyo ili iwe kituo cha afya.

Ujenzi wa zahanati hiyo umegharimu Sh. milioni 147 na itatoa huduma mbalimbali za afya kwa wakazi wa eneo hilo.

Akizungumza wakati wa ziara ya kutembelea miradi katika Halmashauri ya Babati, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Babati, Hamisi Malinga, alisema kabla ya ujenzi wa zahanati hiyo, wananchi walilazimika kusafiri hadi Babati mjini kufuata huduma ya matibabu katika hospitali ya misheni Dareda, hali ambayo iliwagharimu kinamama wajawazito na watoto hasa wakati wa msimu wa mvua.

Malinga alisema baada ya kuona hali hiyo, Shirika la Karimu International Foundation kupitia mradi wa ustawishaji afya ya jamii (Kaheso), lilitoa fedha hizo kwa kushirikiana na serikali kujenga zahanati hiyo.

Alisema kwa sasa wananchi wanapata huduma za matibabu katika zahanati hiyo badala ya kwenda Dareda misheni kama ilivyokuwa awali.

"Hivi sasa, kila kitu cha huduma ya afya kinapatikana hapa na tunatarajia kufanya upanuzi wa zahanati hii kuwa na kituo cha afya," alitamba.

Daktari wa zahanati hiyo, Anastazia Kisonga, alisema kila siku wanapokea idadi kubwa ya wagonjwa kutoka vijiji vitatu vya kata hiyo.

"Tunaishkuru serikali ya awamu ya tano kutokana na kuwekeza katika sekta ya afya kwa kuwa imewasaidia wananchi kupata huduma kwa karibu," alisifu.

Mkazi wa Kijiji cha Ayalagaya, Victoria Kachuchu, alisema anaishukuru serikali kwa kuwekeza katika sekta ya afya kwa kuwa imesaidia kuepuka vifo vya kinamama na watoto vilivyosababishwa na kutembea umbali mrefu kwa ajili ya kutafuta matibabu.

Alisema kwa sasa hawana shida yoyote kutokana na kuwa huduma zote zinapatikana ikiwamo huduma za kujifungua kwa wanawake pamoja na vipimo vya afya tofauti na awali.





# Askofu Shoo aridhia kusitisha michango ya kanisa mwakani

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Fedrick Shoo, ameridhia kusimamishwa kwa michango mingine ya miradi ya kikanisa kuanzia mwaka 2020 katika Dayosisi ya Kaskazini, ili kuruhusu fedha zitakazochangwa zitumike kuboresha Chuo Kikuu Kishiriki cha Kumbukumbu ya Askofu Stefano Moshi (SMMCo).

Dk. Shoo alitangaza uamuzi huo jana katika Kanisa Kuu la Usharika wa Moshi Mjini, wakati akitoa salam zake za Krismasi kwenye ibada ya kwanza.

"Wana dayosisi wote, naomba ujumbe huu uwafike popote pale walipo, kwamba kupitia vikao vya halmashauri kuu yetu na mkutano wa wachungaji wote, tumeamua kwa kauli moja kwamba Mungu akitujalia, kutuingiza katika mwaka mpya unaofuata, kama dayosisi, kwa hapa kwetu tuutangaze mwaka huo kuwa ni mwaka wa Chuo chetu Kikuu cha SMMUCo.

"Na hii pia, wachungaji wakaamua kwamba michango mingine kuondoa zile sadaka za kawaida, michango mingine yote isimame kwanza ili kwa mwaka huu unaokuja, Mungu akitujalia tuhakikishe tunasimamisha chuo chetu," alitangaza.

Kutokana na uamuzi huo, Dk. Shoo ambaye ni Askofu wa Dayosisi ya Kaskazini, aliwaomba waumini wa kanisa hilo kwa pamoja kujitolea kipekee kuhakikisha chuo hicho hakifungwi.

"Tujitolee kukisimamisha chuo chetu kiwapo, zimefanyika jitihada kubwa sana na za gharama kubwa katika kutimiza masharti tuliyopewa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), yale masharti yote tumetimiza na kozi zote zilizokuwa zimefungwa, zimefunguliwa," alisema.

Alibainisha kuwa chuo hicho kilikuwa kimefungiwa kozi kadhaa na hivyo kufanya idadi ya wanafunzi kupungua na kupunguza uwezo wa chuo kujiendesha na wakati huo huo walikuwa na kazi ya kujenga makao makuu ya chuo, hivyo ni vyema waumini wakatambua huo ni wajibu mkubwa na unahitaji nguvu ya pamoja.

"Kwa msharika yeyote wa Dayosisi ya Kaskazini katika mwaka unaokuja, tujiingize kwa moyo wa upendo, kwa moyo wa mshikamano katika kuitenda kazi hii.

"Kila usharika wamegawiwa uwiano wake, na kwa uwiano huo siyo uwiano mdogo sana, lakini tumeona kwamba tunaweza kama kweli kila mmoja atajitolea na kajitoa. Hapa katika Usharika wetu wa Moshi Mjini tumepewa kuchangia Sh. milioni 56 kwa mwaka mzima wa 2020," alisema. Aliomba kila msharika kutoa Sh. 2,000 kwa kila Jumapili, hivyo katika majuma 52 ya mwaka, watakuwa wametimiza wajibu wao na kwa ajili hiyo akawashauri mwaka ujao waifanye kazi hiyo kwa moyo.



Waumini wa Kanisa Katoliki Minara Miwili wakishiriki kuimba nyimbo kwenye mkesha wa sikukuu ya Krismasi uliofanyika kwenye Kanisa la Mt. Joseph mjini Zanzibar, jana. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Usafiri Moshi-Rombo wageuka lulu

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

UTITIRI wa abiria wanaosafiri kwenda katika Wilaya ya Rombo kwa ajili ya kusherehekea sikukuu za mwisho wa mwaka, jana ulisababisha Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (Latra) mkoani Kilimanjaro, kuruhusu mabasi makubwa ya abiria kuhama njia kwa muda ili kunusuru mamia ya wanaosotea usafiri.

Matangazo ya moja kwa moja yaliyokuwa yanatolewa na Latra kupitia vipaza sauti vya Halmashauri ya Manispaa ya Moshi katika eneo la kituo kikuu cha mabasi yaendayo mikoani, yalieleza kuwa uamuzi huo umefikiwa na mamlaka zinazohusika baada ya kujadiliana kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo.

Kaimu Meneja wa Latra mkoani Kilimanjaro aliyejitambulisha kwa jina moja la Masoud kwa kushirikiana na Kikosi cha Usalama Barabarani, walithibitisha kuridhia kuruhusiwa mabasi kuokoa jahazi kutokana na abiri kufurika kituo kikuu cha mabasi cha Moshi Mjini.

Licha ya Latra kuruhusu magari madogo ya abiria aina ya Coaster kubeba abiria kutoka Kituo Kikuu cha Mabasi Moshi Mjini kwenda Rombo, hali ya usafiri kituoni hapo bado ilikuwa ni mbaya.

Juzi, Mji wa Moshi ulikuwa umejaa idadi kubwa ya wageni kutoka mikoa mbalimbali nchini, huku ukitishiwa na msongamano wa magari madogo yanayoingia na kuelekea vijijini.

Msongamano huo ulitokana na utamaduni wa wenyeji wa Mkoa wa Kilimanjaro, kurejea makwao kila inapofika sherehe za mwisho wa mwaka za Krismasi na Mwaka Mpya.

Kuanzia majira ya 4:00 asubuhi hadi saa 3:00 usiku, katikati ya mji huo na kituo kikuu cha mabasi yaendayo mikoani, hali ilikuwa tete pia kutokana na idadi kubwa ya abiria kugombea mabasi madogo yanayofanya safari zake kati ya Moshi Mjini na maeneo ya Rombo, Marangu, Machame, Siha, Old Moshi na Uru.

Nipashe lilishuhudia askari polisi wa Kikosi cha Usalama Barabarani, wakiwa wamepangwa kila kona kudhibiti upakiaji wa hatari wa abiria hao.

Idadi kubwa ya wageni hao ni wale walioingia katika Mji wa Moshi kwa kutumia treni ya abiria na hivyo kufanya idadi ya wageni kuongezeka kwa kiwango kikubwa msimu huu wa sikukuu za mwisho wa mwaka.

Wiki iliyopita, Shirika la Reli Tanzania (TRC) lilitangaza kuongeza safari za Dar es Salaam-Moshi kutoka nne kwa wiki (mbili kwenda na mbili kurudi) hadi sita.

Hatua hiyo inatokana na mahitaji makubwa yaliopo tangu treni ya abiria irejee kufanya safari zake kutoka Dar es Salaam kwenda Moshi, Desemba 6 mwaka huu baada ya miaka 25 ya kusitishwa kwake, safari moja ikichukua zaidi ya abiria 600.

## Huduma za waliofanyiwa ukatili zaanzishiwa kituo

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

MCHAKATO wa uanzishwaji wa Kituo cha Huduma Jumuishi za Pamoja (One Stop Centre) ili kuwasaidia waathirika wa ukatili wa kijinsia katika Hospitali ya Wilaya ya Siha, umekamilika.

Kwa mujibu wa Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Peter Msaka, Mkurugenzi Mtendaji wa Siha amekubali kutoa chumba kimoja katika hospitali hiyo kwa ajili ya timu ya wataalamu wanaopaswa kushughulikia masuala ya ukatili.

"Kimsingi, mchakato huu ni kama sasa umekamilika, tayari mkurugenzi wetu ameridhia kutoa chumba kimojawapo katika hospitali ya wilaya kwa ajili ya kuwa One Stop Centre. Tunamshukuru sana kwa ajili ya mpango huo," alisifu.

Siku chache zilizopita, Ofisa Ustawi wa Jamii wa Mkoa wa Kilimanjaro, Flora Betwel, alisema huduma za uchunguzi kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia wanaofikishwa kwenye vituo jumuishi vya pamoja katika muda usiozidi saa 72 baada ya tukio la ukatili, zinapaswa kutolewa bure.

Betwel alisisitiza uamuzi wa kutowalipisha fedha waathirika hao, ulishatolewa na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu.

Ofisa huyo alisisitiza kuwa mara nyingi serikali inakosa taarifa za waathirika wengi wanaokwenda kufanyiwa uchunguzi katika hospitali zao na wengi wanabaki majumbani kwa sababu wanadhani watakapofika hospitali ni lazima watoe fedha.

Mratibu wa Haki za Binadamu na Jinsia wa Shirika la Kiraia la Kwieco, Elizabeth Mushi, alisema mafanikio hayo ya uanzishwaji wa kituo jumuishi cha pamoja katika Wilaya ya Siha ni utekelezaji wa Mpangokazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (Mtakuwwa).

Tayari Kwieco imeshaanza kuwajengea uwezo wataalamu hao, kwa ufadhili wa Taasisi ya Friedrich Naumann Foundation for Freedom.

Mpango huo ulianza kutekelezwa nchini kote kuanzia mwaka 2017/18 na utaendelea hadi mwaka 2021/22 ikiwamo pia na mikakati ya kuanzisha vituo jumuishi vya pamoja katika mkoa wa Kilimanjaro.

ama
ALHAMISI DESEMBA 26, 2019
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 18

## Mlolongo wa mambo makubwa yanayowakuta wazazi wa njiti



Ukurasa 14

Ugali, mlo unaoliwa zaidi Afrika na unachangia nguvu kwa binadamu.



Ukurasa 16

## Mfumo mpya wa takwimu mtandaoni unavyoleta mapinduzi ya afya mitaani





### MIAKA MINNE YA JPM

# Dk. Mbwanji: Hospitali ya Rufani Mbeya tuna mafanikio makuu 11

Ukurasa 14



Ugali, mlo unaoliwa zaidi Afrika na unachangia nguvu kwa binadamu. **PICHA: MTANDAO.**

# Utafiti: Watu watakula mara mbili ya sasa

**Na Mark Kinver**

WANASAYANSI wa Chuo Kikuu cha Gottingen, Ujerumani, wametafiti na kubaini hadi kufikia mwisho wa karne iliyopo, hitaji la mlo kwa wanadamu litaongezeka kwa asilimia 80, kulinganisha na ilivyo leo.

Ni ubashiri unaokaribia wastani kuongezeka mara mbili ya namna ilivyo sasa, huku aina ya chakula kitakachohitajika zaidi katika mabadiliko hayo ni kinachotia nguvu mwilini, kwa ongezeko la asilimia 60.

Aina nyingine ya vyakula vinavyohitajika katika mwili wa mwanadamu ni vya kulinda na kujenga mwili.

Hata hivyo, taarifa zilizoko kupitia jarida la afya, ni kwamba mwelekeo uliopo sasa duniani, wakazi wa Afrika wako hatarini kubaki katika hali mbaya zaidi, wakiumizwa na mabadiliko hayo.

Makadirio ya kasi ya ongezeko la watu duniani yanayotolewa, ni kwamba hadi mwaka 2010 dunia ilikuwa na jumla ya watu bilioni saba na makadirio ni kwamba, hadi kufikia mwaka 2100 idadi itafika watu bilioni 11.

Kwa nini mlo wa kuongeza nguvu utakuwa zaidi? Inatajwa sababu mojawapo ni idadi ya watu kwa asilimia 18 wataongezeka kuwa na miili mikubwa na wanarefuka zaidi, umbile litakalowapa hitaji la mlo zaidi wa kuwatia nguvu ya kuwezesha kumudu shughuli zao.

AFYA

MIAKA MINNE YA JPM

# Dk. Mbwanji: Hospitali ya Rufani Mbeya tuna mafanikio makuu 11

• Kiwanda maji, mabingwa, huduma mionzi



Mtaalamu akionyesha namna ya kutengeneza maji tiba.

**Na Augusta Njoji, a**liyekuwa MBEYA

RAIS John Magufuli alipoingia madarakani Novemba 2015, moja ya vipaumbele vyake vikubwa ni uboreshaji huduma za afya kwa wananchi wake.

Lengo ni kuhakikisha hiyo inakuwa na mafanikio makubwa. Alimteua Ummy Mwalimu, kuwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, na fasi anayodumu hadi sasa.

Ni kweli ishara za mafanikio zinaonekana, katika sekta hiyo ya afya inayokutana na ushirikiano mtambuka na wizara kama Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa an Serikali ya Mitaa (Tamisemi).

Huduma za afya hospitalini na viwango vya chini vya kutolea huduma, zimeendelea kuimarika kwa kiwango kikubwa, huduma za afya za umma sasa zikipata heshima kubwa kiutendaji.

Aina na mustakabali wa mafanikio, unaelezeka zaidi katika sura ya mgawanyiko kimaeneo, kama mkoa na wilaya. Hapo ndipo eneo la mfano katika mafanikio, mkoa wa Mbeya, ambako pia ni makao makuu ya Nyanda za Juu Kusini mwa nchi, kunaweza kufanyiwa marejeo.

> Kwa wiki operesheni za koo 15 hadi 20 zinafanyika. Awali huduma hizi mgonjwa ilimlazimu kwenda Dar es Salaam

### MKUU WA MKOA

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, anasema serikali imeuwezesha mkoa huo kujenga miundombinu ya kisasa katika sekta zinazochangia kuleta ustawi kwa wananchi, ikiwamo afya.

Hapo ndipo Hospitali ya Kanda ya Rufani Mbeya (MZRH), inayochangia huduma kwa mkoa wa Mbeya na Kanda Nyanda za Juu Kusini, ambayo kwa kipindi cha miaka minne sasa inasema ina mafanikio lukuki.

Mkurugenzi wa Hospitali hiyo, Dk. Godlove Mbwanji ana orodha ya anayoyataja jumla yake 11 ambayo yanayowezesha utoaji huduma za afya kwa Kanda ya Nyanda za Juu.

### KIWANDA CHA MAJI TIBA

Dk. Mbwanji anasema, kuanzishwa kiwanda chenye uwezo wa kuzalisha maji tiba lita 3,840 kwa mwezi, ni miongoni mwa mafanikio ya hospitali, kutekeleza kwa vitendo Sera ya Viwanda, ambayo ni sehemu ya maagizo ya Rais John Magufuli.

Anasema kiwanda kilianzishwa Februari mwaka huu, kwa gharama ya Sh. milioni 120 kwa mapato ya ndani, kikizalisha dripu mita za mita ujazo 250 hadi 500 na zimeanza kutumika kuhudumia wagonjwa wahitaji.

Hali hii imesaidia kuondokana na adha ya ama kununua au kuagiza dripu nje ya nchi na kiwanda kina uwezo wa kutengeneza maji tiba lita 3,840 kwa mwezi, huku uhitaji wa hospitali ni lita 5,232, hivyo inakidhi kwa asilimia 73 uhitaji wa maji tiba kwa ajili ya hospitali, anasema.

Mkurugenzi huyo anasema, wamefanikiwa kupunguza gharama za ununuzi wa maji ya tiba nje nchi, wakiwa na uhakika wa upatikanaji wake, pia wameshatoa mafunzo ya utaalamu wa utengenezaji maji tiba na kuongeza ajira kwa wataalamu wake.

Mara baada ya kukidhi mahitaji ya ndani, tutaanza kuzalisha maji tiba ambayo yatauzwa katika hospitali zilizopo Nyanda za Juu Kusini, pia muda mfupi tutaanza kutengeneza dawa za macho eye drop mchakato umeshaanza, anasema.

Anaeleza kwamba, wanatarajia kuanza kutengeneza dawa ya macho na masikio kwenye kiwanda hicho mwaka 2020.

Dk. Mbwanji anasema, hospitali hiyo inahudumia mikoa saba ya Nyanda za juu Kusini ambayo ni Iringa, Njombe, Ruvuma, Katavi, Rukwa, Songwe na Mbeya na inaendelea kuboresha huduma, ili kutoa huduma bora za afya kwa wananchi.

### DAWA & DAKTARI BINGWA

Anasema hospitali kwa miaka minne ya serikali iliyopo, madarakani, imekuwa na ongezeko la upatikanaji dawa kutoka asilimia 70 hadi 95, baada ya kuanzishwa duka la dawa la bima na matarajio ni watakapoanzisha kitengo cha kansa, upatikanaji huo utafikia asilimia 98.

Katika orodha ya matabibu, imeongezeka kutoka madaktari bingwa 36 kati ya mwaka 2015 hadi 2019, hivyo kufanya idadi yao kufikia 53.

Dk. Mbwanji anaeleza madaktari hao wanatoa huduma katika idara mbalimbali, hivyo kuongezeka huduma za matibabu yanayohitaji upasuaji kwa siku sita za juma, pia huduma za dharura pia.

Vilevile, tumeanzisha huduma za kibingwa za masikio, koo, pua. Kwa wiki operesheni za koo 15 hadi 20 zinafanyika. Awali huduma hizi mgonjwa ilimlazimu kwenda Dar es Salaam, anafafanua na kuongeza;

Tumeanzisha huduma ya kisasa ya upimaji wa kiwango cha usikivu, huduma ambayo awali iliwalazimu wakazi wa Nyanda za Juu Kusini kuifuata jijini Dar es Salaam.

AFYA

# Dk. Mbwanji: Hospitali ya Rufani Mbeya tuna mafanikio makuu 11



Maji tiba yanayozalishwa katika hospitali Mbeya. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

Anasema kuwapo mashine hiyo, kumesaidia kujua kiwango cha kupoteza usikivu na kumwezesha mgonjwa kupatiwa matibabu halisi ya tatizo la usikivu.

"Zaidi ya wagonjwa 900 wanatarajiwa kupatiwa huduma hii kwa mwaka 2019. Pia, tumeboreshwa kwa huduma za tiba ya figo hasa katika kusafisha figo.

"Waliowengi wanaopata huduma hii, ni wale wenye tatizo la kudumu . Kwa sasa, tunahudumia wagonjwa 21 wa kudumu kwa mwezi na wale wa muda mfupi ni wanane kwa mwezi," anasema.

**HUDUMA MIONZI**

Dk. Mbwanji anasema, upatikanaji wa huduma za mionzi kama 'CT Scan' hadi sasa wagonjwa 1,532 wamepatiwa huduma, pia kwa mashine za kidigitali za X ray, Fluoroscopy, Mammography na Ultrasound.

"Hii imemwezesha mwananchi wa kipato cha chini kuweza kumudu vipimo hivi, kutokana na gharama za vipimo tajwa kuwa na bei nafuu. Awali, mwananchi alikuwa wanasafiri umbali mrefu kufuata huduma hizi ambapo zilikuwa zikipatikana jijini Dar es Salaam," anasema.

**KUPANUA MIUNDOMBINU**

Dk. Mbwanji anasema, hadi sasa wameshaongeza uwezo wa kulaza wagonjwa, kutoka vitanda 477 hadi 553 baada ya kukamilika jengo la watoto na hivi karibuni serikali imetenga Sh. bilioni 7.5 kwa ajili ya kupanua jengo la wazazi litakalokuwa na ghorofa tano.

"Matarajio baada ya kumalizika kwa mradi huu, kutakuwa na ongezeko la huduma za kulaza wagonjwa idadi ikiwa vitanda 200, vitanda 40 'grade one' (daraja la kwanza) na vitanda 160 kawaida."

" Vilevile kutakuwapo na vyumba vitatu vya upasuaji mkubwa, pamoja na chumba maalumu cha huduma za watoto wadogo ndani ya mwezi mmoja," anasema.

Anasema serikali imeshatoa kiasi cha Sh. bilioni tatu za kujenga jengo la radiolojia, lenye idadi ya vyumba 37 vikiwamo vya madaktari, ukumbi, darasa la mafunzo na kununua vifaa vya mionzi.

"Kukamilika kwa ujenzi huu kumeleta mafanikio katika utoaji huduma za mionzi, zikiwamo uanzishwaji huduma mpya za 'CT Scan,' mashine za kidigitali za X ray, Fluoroscopy, Mammography, Ultra Sound.

"Hii inamwezesha mwananchi wa kipato cha chini kumudu vipimo hivi kutoka na gharama za vipimo tajwa kuwa nafuu. Awali, mwananchi alikuwa anasafiri umbali mrefu kufuata huduma hizi, ambazo zilikuwa zikipatikana jijini Dar es Salaam," anasema.

**DAWA ZA KULEVYA**

Dk. Mbwanji anasema kuanzishwa kituo cha methadone kuhudumia waathirika wa dawa za kulevya na kinachotoa matibabu kwao, inaleta huduma hiyo karibu na wananchi.

> "Vilevile kutakuwapo na vyumba vitatu vya upasuaji mkubwa, pamoja na chumba maalumu cha huduma za watoto wadogo ndani ya mwezi mmoja.

"Takwimu zinaonyesha kuanzishwa kwa kituo hiki Julai 2017 kilikuwa kinahudumia warahibu 2 na kwa sasa kinahudumia warahibu 261, wakiwa wanaume 252 na wanawake tisa.

**TAALUMA & UKALIMANI**

Anasema, kuanzishwa tawi la Chuo Kikuu cha Afya na Tiba Dar es Salaam tawi la Mbeya, imetoa fursa kwa madaktari kuanza kutafiti na kutoa mafunzo kwa wanafunzi wao, ili kuwezesha kuzalisha wataalamu mbalimbali wa afya.

Pia ndani ya miaka minne iliyopita, inaelezwa wameanzisha huduma ya mkalimani wa lugha ya alama mwaka jana, ikiwa ni hospitali pekee nchini kuanzisha huduma hiyo.

Mkurugenzi huyo wa Hospitali ya Rufani Mbeya, anasema hatua hiyo baada ya kugundua kuna watu wengi wenye ulemavu wa kutokusikia washindwa kupata uhuduma stahiki za matibabu, kwa sababu ya kukosa mawasiliano mazuri kati ya mgonjwa, daktari na wahudumu wengine.

"Hadi sasa tunahudumia wagonjwa 22 wa kawaida kwa siku wenye ulemavu wa kusikia, 27 wanahudhuria kliniki ya dawa za kupunguza makali ya VVU; 12 wamefanyiwa upasuaji mdogo na mkubwa, ikiwamo uvimbe kinamama, 16 wamefanyiwa tohara na saba wanahudhuria kliniki ya wazazi," anaeleza Dk Mbwanji.



Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufani Kanda Mbeya, Dk. Godlove Mbwanji.

**WANANCHI NAO?**

Mmoja wa wakazi wa Mbeya, Joseph Masyani, anasema kuimarika huduma za afya kwenye hospitali za serikali, kumewasaidia wananchi kuondokana na gharama kubwa za matibabu katika hospitali za binafsi.

Pia anasema awali huduma za kibingwa hazikuwapo katika kanda hiyo na kusababisha wagonjwa kusafiri umbali mrefu kufuata huduma hizo, ikiwamo Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

**WIZARA AFYA**

Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano katika Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Gerald Chami, anatamka: "Tumeboresha sekta ya afya, itafanyika katika kanda tano nchini, kwa taasisi ambazo ziko chini ya wizara, ili kuwaeleza wananchi mafanikio ya miaka minne kwenye sekta hiyo, ambayo yamesaidia wananchi kupata huduma bora za afya."

MAZINGIRA

# Mfumo mpya wa takwimu mtandaoni unavyoleta mapinduzi ya afya mitaani

• Songwe mfano kupaa toka hali mbaya • Maofisa afya, wasomi wakiri mageuzi • Vyoo vibovu; 62% ya 2015 hadi 34 leo




Mifereji yenye maji machafu iliyoko Dar es Salaam. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Devota Mwachang'a,** DODOMA

MAOFISA afya wa mikoa na wilaya nchini, kimsingi ndio ngome tegemezi katika ukusanyaji na uwekaji taarifa na takwimu sahihi za afya, usafi wa mazingira, magonjwa na nyingine yanayohusu afya ya binadamu kwa ujumla.

Uwekaji huo wa taarifa, kwa sasa ni katika mifumo ya kielektroniki, kulingana na teknolojia iliyopo. Lengo ni kurahisisha upatikanaji wake kwa wahitaji, wakiwamo watafiti, waandishi habari, wafadhili na watendaji.

Jamii inahitaji elimu ya uelewa na upatikanaji wa taarifa sahihi zinazohusu masuala ya usafi, upatikanaji wa vyoo na majisafi na usafi wa mazingira, ili kujilinda dhidi ya magonjwa ya mlipuko, ikiwamo janga la kipindupindu.

Ripoti ya Hali ya Huduma ya Afya nchini, kwa kipindi cha mwaka 2018 iliyotolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, inaonyesha takwimu za wagonjwa wa kipindupindu imepungua.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, katika mwaka 2018 ilifika 4,706 ikilinganishwa na wagonjwa 4,626 kwa mwaka 2017 na idadi ya vifo imepungua kufikia 84 mwaka 2018, ikilinganishwa na 93 kwa mwaka 2017.

**OFISA AFYA MKUU**

Ofisa Afya Mkuu wa Ofisi ya Rais (Tamisemi), Juma Motoka, anasema maofisa afya wa mikoa, wanaongezewa ujuzi zaidi wa uingizaji takwimu zote kwenye mfumo unaotoa taarifa za usimamizi wa usafi nchini ujulikanao kama NSMIS, ulioboreshwa na Wizara ya Afya, lengo ni kutoa taarifa sahihi kwa umma, kupitia tovuti yake.

> **Hivi karibuni tumepita na kampeni yetu ya 'Nyumba ni Choo' na imefanya vibaya zaidi Morogoro, Tanga, Mbeya, Songwe, Geita, Mwanza, Mara, Shinyanga, Simiyu na Kagera.**



Mfumo wa majitaka jijini Mwanza.

Motoka anasema hayo katika mafunzo ya siku mbili yaliyoandaliwa na Wizara ya Afya, ili kuwakutanisha pamoja maofisa afya wa mikoa na wilaya zaidi ya 60 na wadau wa afya jijini Dodoma.

Katika mjumuiko huo hivi karibuni, lengo hasa ni kuwapa ujuzi katika uingizaji takwimu kwenye mfumo wa utoaji taarifa za uwepo wa maji, huduma ya kujisafi na usafi ujulikanao kama "Tanzania WASH Portal".



Vyoo katika baadhi ya shule.

Remidius Kakuru ni Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Afya na Mazingira, kutoka Wizara ya Afya, anasema mfumo wa NSMIS ni mzuri na umetengenezwa na wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Anasema, ni mfumo unaofuata msingi ya mifumo ya serikali kwenye masuala ya usalama, ambayo ni muhimu kwenye takwimu, pia umeunganishwa na mifumo ya serikali.

Kakuru anasema: "Uingizwaji takwimu sahihi katika mfumo, utatoa ripoti sahihi na unaongeza uonwaji wa taarifa. Watu wanaweza kuziona taarifa bila kutumia namba ya siri kuingia (password), hivyo tunaruhusu watu waweze kutukosoa, kwa hiyo tusiruhusu uwepo wa 'data' ambazo watu watahoji kuhusu ubora wake."

**MABORESHO VYOO**

Takwimu kutoka tovuti ya wizara hiyo inaonyesha idadi ya kaya zenye vyoo bora nchini imeongezeka hadi asilimia 62 kufikia Septemba mwaka huu, ikilinganishwa na asilimia 34 ya mwaka 2015.

Pia inaelezwa wizara inayohusika na afya, imewezesha wananchi kupata taarifa za afya, udhibiti wa wagonjwa, usalama wa chakula, usafi wa mazingira na uchafuzi wa hali ya hewa na maji.

**WATAALAMU MFUMO**

Tuzo Englibert ni mtengenezaji wa mfumo wa NSMIS kutoka UDSM, anasema kwenye matumizi ya mifumo ya kielektroniki, changamoto huwa hazikosekani, hivyo watendaji wanapoona wawe mabalozi wazuri wa kuisambaza mifumo hiyo, ili wengine wafuate matumizi yake.

"Mtakapopata mrejesho kutoka kwa wananchi waliopitia mfumo na kusoma taarifa, mchukue nafasi kama nyie ndiyo wizara kwa kuyachukua maoni yao kwa kuwa hawezi kutufikia moja kwa moja," anasema Englibert na kuongeza:

"Lakini kwa kutumia hiyo 'portal' iliyosambazwa chukua maoni ya wadau tuleteeni kule ili wanachotaka kifanyike tukifanyie kazi."

Mkuu wa kitengo cha Wash na Mratibu wa Kampeni ya Kitaifa ya Usafi (NSC) kutoka Wizara ya Afya, Anyitike Mwakitalima, anafafanua kwamba kwa sasa taarifa za usafi si siri tena, tofauti na awali ilikuwa ngumu kuipata taarifa hiyo."

Anasema, wahitaji wake walilazimika kuandika barua au kupiga simu wizarani kuomba taarifa kwa ajili ya masuala ya kitafiti, kiuandishi au kwa suala la mtu kutaka kujua nchi ipo wapi kwenye hali ya afya.

Mwakitalima anasema, kabla ya mfumo wa Portal, taarifa hazikuwekwa wazi na inawezekana ofisa husika alikaa nazo tu (ikiwa wilaya yake ya mwisho kwa utendaji wa masuala ya usafi), lakini sasa mkurugenzi au mkuu wa wilaya, ataona taarifa na kuchukua hatua inayostahili.

"Hivi karibuni tumepita na kampeni yetu ya 'Nyumba ni Choo' na imefanya vibaya zaidi Morogoro, Tanga, Mbeya, Songwe, Geita, Mwanza, Mara, Shinyanga, Simiyu na Kagera," anasema.

Mwakitalima anaenelea: "Ilikuwa inalegalega, lakini baada ya ushiriki wa viongozi kwenye kampeni na hamasa toka kwa msanii Mrisho Mpoto kuna mabadiliko sasa," anasema Mwakitalima.

Anaupongeza Mkoa wa Songwe uliokuwa wa mwisho sasa upo juu ya mikoa ya Lindi na Kigoma wenyewe umepanda upo katikati na mikoa ya Arusha na Mara ambayo tangu kampeni iliongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya wakazi wasio na vyoo.

Ofisa huo anaeleza mageuzo yaliyotokea ni kwamba hivi sasa, imepanda kwa asilimia 10, baada ya kuhamasika mkoa wa Mara ndani ya miezi miwili.

**WENYE MFUMO**

Kaimu Mkurugenzi wa Kinga wa Wizara ya Afya, Dk. Janeth Mghamba, anawaelekeza wafanyakazi wa afya wenye uzoefu na mfumo wa NSMIS kwenye ukusanyaji taarifa za magonjwa na masuala ya usafi, wautumie vyema mfumo ulioboreshwa wa Tanzania WashaASH Portal ili uwasaidie.

> **Lakini kwa kutumia hiyo 'portal' iliyosambazwa chukua maoni ya wadau tuleteeni kule ili wanachotaka kifanyike tukifanyie kazi.**

Anafafanua namna ya kutumia ni kuangalia maeneo yatakayoibua uwepo wa magonjwa ya kipindupindu au kuharisha, hali ya usafi, upatikanaji wa maji, vyoo ipoje kwenye maeneo hayo.

Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la WaterAid Tanzania, Dk. Ibrahim Kabole, anasema kinachofanyika kupitia mfumo wa Portal inafanana na kujiweka wazi na tayari kushirikiana na wadau katika kuboresha utendaji, kwa kushirikiana, kazi ambayo imeshafanyika na Wateraid Amerika na Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), kuunda mfumo wa sasa.

INAENDELEA UK.20

# Mkuranga yajipanga kukabili janga la lishe duni isiyoisha



Sherehe ya Siku ya Watoto, katika viwanja vya Shule ya Msingi, Mwanambaya, Mkuranga. Kundi hilo ndilo lenye waathirika wakubwa wa lishe duni. **PICHA: MTANDAO**

**Na Yasmine Protace**

IKO dhahiri kuna uhusiano wa moja kwa moja, kati ya lishe na ustawi wa afya ya mtu. Inapotokea aina yoyote ya ukiukwaji wake, unaangukia mtu kuwa na afya duni.

Matokeo ya kinachoshuhudiwa katika ukiukwaji huo, yanaangukia katika hali kama watoto kukonda, pia kupatwa na utapiamlo na makuzi duni, yanayokinzana na uhalisia.

Madhila hayo yanaenda mbali hata kwa wajawazito, wanaoangukia katika matatizo mengi ya hatari kiafya, ikiwamo upungufu wa damu.

Kiashiria hicho, kimsingi ni sehemu ya uhalisia wa yanayokabili maisha ya wakazi katika Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, ambayo sasa inaendelea kujipanga katika vita kukabili mapungufu hayo kijamii.

Dalmia Mikaya, ni Katibu Tawala wa Wilaya ya Mkuranga, anayekiri hali ya lishe kwa jamii yake hairidhishi na takwimu zinaonyesha, kuna tatizo katika lishe, hivyo anahimiza haja kuwapo darasa kuanzia ngazi ya familia, watendaji hadi viongozi.

Mikaya ametamka hayo kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya, wakati wa mafunzo ya maandalizi ya mipango na bajeti ya lishe katika halmashauri kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Katibu Tawala anafafanua takwimu zilizopo, kwamba hali ya lishe ya jamii Mkuranga sio ya kuridhisha, upungufu wa damu kwa watoto ni wastani wa asilimia 50.2 au sawa na nusu ya watoto wote.

Pia anataja robo yao, sawa na asilimia wana uzito pungufu; udumavu ni asilimia 16; waliokonda asilimia saba, huku rekodi ni sio ya kuridhisha kwamba asilimia 90 ya vifo vinavyotokana na matatizo ya uzazi mwaka juzi, vilitokana na upungufu wa damu.

Mikaya anaongeza kwamba, mikakati muhimu kwa jamii ya Mkuranga, ni kutoa elimu ya lishe kupitia mikutano ya hadhara ya serikali, maonyesho kwa sinema, michezo ya jadi, mashindano mbalimbali.

Anataja mengine ni mabango, vipeperushi na kuhimiza suala la lishe kuwa ajenda mtambuka katika vikao vyote vya Halmashauri ya Wilaya Mkuranga.

Kwa mujibu wa Katibu Tawala, kata zinazoongoza kwa kuwa na wagonjwa wengi wa utapiamlo ni: Kimanzichana, Vikindu, Mkuranga, Kisiju, Bupu, Tengelea, Njianne, Lukanga, Kiparang'anda, na Mwarusembe, ambazo zitapewa kipaumbele cha mradi wa kutokomeza maradhi hayo.

Mwezeshaji wa Mipango na Bajeti kutoka Ofisi ya Rais Tamisemi, Mkama Lugina, anasisitiza wadau wa masuala ya lishe, kuendelea kutoa elimu kwa jamii, hususani kuzingatia umuhimu wa lishe katika siku 1,000 za mtoto tangu kutungwa mimba), kwamba ni muhimu kumjenga kiafya na kiakili, ikimwepusha na udumavu.

"Tutaendelea kutoa elimu ya lishe kwa jamii hususani kuzingatia umuhimu wa lishe katika siku 1,000 za mtoto tangu siku ya kutungwa mimba, ndio muhimu zaidi kwa kumjenga mtoto," anasema.

Lugina anaeleza umuhimu wa kumnyonyesha mtoto katika miezi sita ya mwanzo baada ya kuzaliwa, upatikanaji chakula cha nyongeza kwa kinamama, utoaji matone ya vitamin A na kupambana na ongezeko la wanawake wenye uzito mkubwa na viriba tumbo.

Mengine anataja utumiaji ni madini joto, makuzi changamshi na kusisitiza umuhimu Fedha za Bajeti za Vituo (DHFF) kupelekwa moja kwa moja kwenye shughuli zenye matokeo makubwa.

Ofisa Lishe Wilaya ya Mkuranga, Pamela Meena, anachangia kwamba, changamoto kubwa ni kutokuwapo mikakati shirikishi kwa idara zote katika halmashauri hiyo, hivyo anaelekeza kila idara kupendekeza sampuli ya shughuli zitakazowekwa katika mipango na bajeti za lishe katika halmashauri hiyo.

AFYA

# Mlolongo wa mambo makubwa yanayowakuta wazazi wa njiti

NA CHRISTINA MWAKANGALE



Kinamama wenye watoto njiti walipotembelewa hospitalini. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

***ALHAMISI iliyopita ilikuwa sehemu ya kwanza ya ushuhuda kuhusiana na mzazi wa watoto wanne njiti na madhila aliyokutana nayo, sasa akihudumia watoto watatu wenye afya njema. Endelea na simulizi kutoka kwa mama mwenzake.***

**YALIYOMKUTA BRIGITA**

Mama Brigita, anayejitambulisha kwa jina moja, naye anatoa yaliyojiji katika simulizi ya watoto njiti. Ana simulizi ambayo si nzuri kiafya, kwamba ilianza kwa kupasuka chupa ya uzazi akiwa usingizini na alipompigia daktari wake, alimtaka afike hospitalini haraka.

"Nilitakiwa kujifungua mwezi wa pili, lakini chupa yangu ilipasuka mwezi wa 12. Nilikuwa nimelala wakati wa usiku, nikaamka kwenda kujisaidia nikashangaa," anasimulia na kuendelea:

"Baada ya muda kidogo nikampigia daktari wangu simu, ambaye nilikuwa namuona kwa kipindi chote cha ujauzito na kuniambia hilo ni tatizo na muda wa kujifungua bado."

Mama huyo mkazi wa Dar es Salaam, anasema baada ya kumuona daktari huyo, alishauriwa kwamba tatizo lake inabidi mtoto azaliwe kabla ya umri kutimia, ilhali umri wa mtoto tumboni bado mdogo.

Brigita anasema, baadaye katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) na baada ya kufika huko alifanyiwa uchunguzi, walibaini maji yaliyomo kwenye tumbo la uzazi yanaendelea kupungua na kuhatarisha uhai wa mtoto wao.

"Wakaniambia kuna mawili hapa, mtoto kuishi au kufariki. Tukashauriana na madaktari kwamba, kama nitaweza kukaa wiki moja 'bedrest' (kudumu kitandani) ili maji yasiendelee kuisha na angalau siku ziongezeke kidogo na nilitakiwa nile vizuri ili mtoto akizaliwa kilo ziwe zimeongezeka, kwa sababu alikuwa bado mdogo sana," anasimulia Brigita.

"Niliambiwa nilale tu nisihaingaike, walisikilizia mapigo ya moyo ya mtoto kila baada ya muda fulani, kwa sababu madaktari waliniambia niwe makini kusikiliza ili kama mapigo hayapo niweze kutoa taarifa mapema. Haikuwa rahisi kukaa wiki nzima sehemu moja tu.

"Ilipofika tarehe 29 nikaanza kuona tofauti, kwa sababu mapigo ya moyo yalikuwa hayasikiki, ikabidi niwakumbushe manesi tuangalie mapigo ya moyo kila wakati: "Ikabidi daktari apigiwe simu na aambiwe kuwa maji yameisha kabisa tumboni na hawezi kuvumilia, inabidi wamtoe mtoto haraka iwezekanavyo.

"Hali yangu ikawa sio nzuri, daktari akaniambia mtoto ana kilo moja tumboni, kwa hiyo akizaliwa uzito unaweza kupungua zaidi au wanifanyie operesheni, wamtoe mtoto kama atakuwa mzima au nijifungue kawaida".

> **Huduma ya mfuko inatolewa kulingana na uanachama na aina ya kifurushi, kwa bahati mbaya mama ambaye si mwanachama hawezi kupata huduma mfuko.**

"Nikaona ni bora wanizalishe kwa operesheni kama mtoto akizaliwa hai nitashukuru Mungu, lakini akizaliwa amefariki pia ni mipango ya Mungu. Namshukuru Mungu nikafanyiwa operesheni na kuna daktari mzuri sana wa watoto pale Muhimbili anaitwa daktari Robert akaja pembeni wakati nipo nafanyiwa operesheni ili kuangalia mtoto kama yuko sawa.

"Basi baada ya muda akamchukua mtoto haraka na kumpleka chumba maalumu cha watoto njiti kwa ajili ya kumuweka kwenye oksijeni..." anasimulia Brigita, mkasa wake.

**BAADA KUZALIWA**

Brigita anasema, mtoto huyo alizaliwa akiwa na uzito kilo moja na gramu 200 siku ya kwanza, lakini baada ya muda kidogo alipungua chini ya kilo moja, kwa maana ya gramu 800, jambo ambalo halikuwa zuri kiafya, hali iliyofanya ahamishiwe kwenye chumba cha njiti wenye hali mbaya (ICU), wanaohitaji uangalizi maalum.

Anaendelea: "Hali ilikuwa mbaya sana hata baba mtoto alipomuona naye akawa na wasiwasi. Nikakaa wodini siku mbili na nilikuwa sijamnyonyesha, wenzangu wanaenda kunyonyesha wakati wa kwangu hata kunyonya hawezi ni mdogo sana.

"Daktari akamuita nesi ili aje aniite nipewe maelekezo nilipofika pale akanielekeza nikamue maziwa kiasi fulani na kumpatia mtoto kupitia bomba la sindano hadi kwenye mrija kulingana na kiasi nilichoambiwa na daktari na kila siku kiasi kilikuwa kinaongezeka kadri uzito unavyoongezeka na kumbeba kifuani kwa mtindo wa kangaroo."



Dk. Julieth Magandi wa Hospitali ya Taifa Muhmbili (MNH) akiwasilisha hoja katika moja ya Siku ya Kuhudumia Watoto Njiti.

Anaeleza kwamba, baada ya mtoto kutoka ICU, alihamishiwa katika wodi ya kawaida ya watoto njiti, alikokaa kwa miezi mwili.

"Bili niliyokuja kudaiwa ni kama milioni nne, ambayo ni pamoja na operesheni, sindano, dawa za kumsaidia mtoto kupumua kwenye mapafu vizuri kwa wale waliokuwa hawana uwezo, waliambiwa walipe kama laki tatu na nusu, lakini wakawa wanaangalia kila mtu na uwezo wake.

"Wengine walitoa laki saba na kuna wengine hawakutoa kabisa kulingana na kutokuwa na uwezo na kama ulianzia hospitali labda ya Temeke na kupewa rufani kuja Muhimbili hao angalau walilipishwa hela kidogo," anasema.

"Kuna wengine hata 60,000 iliwashinda kulipa. Ukiambiwa ulipe na ukakataa kulipa, wanakukatalia kutoka hospitali na daktari hawezi kukusainia kabisa hadi ulipe. Kwa mtu ambae haletewi chakula, hana uwezo wa hiyo milioni nne anaitoa wapi?" Anasema Brigita.

Mama huyo anasema, ni jambo lililomfanya aanzishe kundi la mtandao wa 'whatsap' mahususi kwa kinamama njiti, washauriane kuhusu malezi ya watoto wao.

**MZAZI ACHANGIA**

Mama anayejitambulisha kwa jina la Aisha, anasema wakiwa wodini kwa muda wa miezi yote, watoto ndio wanaopewa chakula bure, huku mama anayelea anajihudumia, jambo lililomfanya kula mara mbili tu kwa siku kutokana na hali ya kipato chake.

"Tunakula asubuhi na jioni tu na maziwa usipokula vizuri hayatoki, sasa uzito utaongezekaje kwa mtoto?" Anahoji na kuongeza: "Tunaiomba serikali ituangalie sisi tunaohudumia hawa watoto kujinunulia chakula miezi mitatu ni mingi tupewe na sisi chakula."

Analalamika Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF), haujawa msaada mkubwa kwa wanaohitaji huduma katika mazingira hayo ya kuwa na mtoto njiti. Aisha anaeleza:

"Mfano, umejiunga na bima ya afya, unaambiwa Najali Sh. 504,000 kwa mwaka na kulazwa ni siku 30 tu, wakati watoto njiti tunalazwa nao zaidi ya mwezi au miezi miwili na nusu. Hiyo hela ya kulipia mwezi mwingine naitoa wapi? Serikali ituangalie jamani watoto hawa wahudumiwe bure."

Meneja Uhusiano wa NHIF, Angela Mziray, anajitetea kwamba wana-



chama wake wanapata huduma na wategemezi wao kulingana na utaratibu wa vifurushi vinavyotolewa.

Anainisha kwamba kuna kifurushi kinachojumuisha wanandoa wenye umri kati ya miaka 18 hadi 35 na mtoto mmoja, kwa ada ya Sh. 504,000 kwa mwaka, kinachotoa huduma ya kulazwa kwa siku 30 kwa mnufaika mmoja.

Pia anataja kifurushi cha mwanachama mwenye umri huohuo na mtoto mmoja kwa ada ya Sh. 924,000 na huduma ya kulazwa siku 45 kwa mwaka.

Kingine anasema, kuna huduma ya umri huo kwa wanandoa na mtoto, ada ni Sh.1, 272,000 na huduma ya kulazwa kwa mnufaika siku 60 kwa mwaka.

**BINGWA MUHIMBILI**

Takwimu zilitolewa na Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Upasuaji wa Hospitalini Muhimbili, Dk. Julieth Magandi, mwaka 2016 katika Siku ya Watoto Njiti Duniani, anasema Tanzania kupitia Mpango Namba Nne wa Millennia, imefanikiwa kupunguza vifo vya wachanga.

Mpango huo ulilenga kupunguza vifo chini ya umri wa miaka mitano kwa zaidi ya theluthi mbili, licha ya kuwapo ongezeko la watoto wanaozaliwa njiti walio hatarini kupoteza uhai, kutakapokosekana uangalizi maalum.

Dk. Magandi anabainisha huduma zinazotolewa kwenye kitengo cha 'Kangaroo' kilichopo hospitalini hapo, kimeimarisha usimamizi thabiti na utaalamu wa unyonyeshaji bora wa watoto wachanga, bila ya kuwapa chakula kingine.

Anasema mtindo wa 'Kangaroo' unamsaidia mama kutunza joto la mwili la asili na kujenga ukaribu kati yake na mtoto aliyezaliwa, pia kupata joto linalomsaidia mtoto kuishi na kukua.

"Watoto njiti hawana uwezo wa kupumua vizuri, kwa kuwa mapafu yao hayafunguki ipasavyo. Kwa mara ya kwanza dawa mpya ya kukomaza mapafu watoto hawa, tumeanza kuitumia, ingawa gharama yake ni kubwa hugharimu Sh. milioni moja kwa mgonjwa mmoja," anasema Dk. Julieth.

**MWAKILISHI UNICEF**

Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (Unicef), linaeleza kwamba huduma bora zinahitajika wakati wa kujifungua hususan kwa watoto wachanga wanaozaliwa na uzito mdogo (njiti) na walio wagonjwa.

Mwakilishi wa Unicef nchini, Dk. Jama Gulaid, anasema dakika ya kwanza baada ya mtoto anapozaliwa anataja kuwa ya 'dhahabu' kwa kila mtoto mchanga, hivyo wanahitaji huduma muhimu.

Dk. Gulaid, anasema kuna ushahidi wa uhakika unaoonyesha kutolewa huduma muhimu wakati wa ujauzito, wakati wa kujifungua na baada ya hapo bila ya kutumia gharama kubwa na uangalizi sahihi unaohusisha teknolojia ya juu, unaokoa maisha ya watoto.

Anasisitiza kwamba, watoto wengi wanaozaliwa kabla ya muda, wanaweza kukua na kuwa na afya nzuri bila ya ulemavu wa kudumu.

Taarifa ya Unicef mwaka 2014, iliyotolewa kwa kushirikiana na wadau, inasema vifo vya watoto



Madaktari mabingwa wa watoto, wakiwa pamoja baada ya kukutana ili kuongeza ujuzi kuhusu kuhudumia watoto njiti, hospitalini Muhimbili. **Chini;** wageni wanaowatembelea kinamama wenye watoto njiti hospitalini.

> **Iwapo huduma hii rahisi ya kusaidia watoto wachanga kupumua inapatikana kwa asilimia 90 ya watoto wanayoihitaji,basi takribani maisha ya watoto wachanga 2,000 yanaweza kuokolewa kila mwaka.**

wachanga kutokana na matatizo ya kuzaliwa njiti, vinaweza kupunguzwa kwa gharama nafuu.

Inataja dawa aina 'antenatal steroids' inapotolewa kwa kinamama wanapopata uchungu wa kujifungua kabla ya wakati katika ngazi za afya zinazostahili, inasaidia kukuza mapafu ya mtoto njiti ambayo hayajakomaa na kuzuia matatizo kwenye mfumo wa hewa ya watoto wachanga.

Pia huduma ya 'kangaroo' inayotolewa katika kitengo maalum hospitalini Muhimbili, inatajwa kuwa na nafasi ya kuepusha vifo vya watoto 5,000 wanaozaliwa kila mwaka nchini, ikiwamo msaada wa vifaa kusaidia matatizo ya kupumua.

"Iwapo huduma hii rahisi ya kusaidia watoto wachanga kupumua inapatikana kwa asilimia 90 ya watoto wanayoihitaji,basi takribani maisha ya watoto wachanga 2,000 yanaweza kuokolewa kila mwaka," anasema mwakilishi huyo wa Unicef.

Anataja njia nyingine ni kuzuia maambukizi kwa mama na mtoto, kwa kutolewa dawa za antibaiotiki kama vile 'amoxicillin' inayotbu maradhi kama niumonia, pia 'gentamicin' kwa kudhibiti maambukizi makubwa kwa watoto wachanga.

Kingine muhimu ni watoto wote wachanga wanahitaji kukaguliwa afya ndani ya saa 24 baada ya siku tatu ya kuzaliwa, ili kuzuia matatizo yanayotokea na yanayosababisha ulemavu katika maisha yao baadaye.

**SERIKALINI**

Sera ya Afya ya Mwaka 2007 inataka huduma za afya kwa wazee, wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano kupata huduma bure.

Waziri wa Katiba na Sheria, Balozi Dk. Augustine Mahiga, anashauri ni wakati sasa serikali kukutana na wadau mbalimbali, ikiwamo Wizara za Afya, Kazi na Sheria, pamoja na sekta binafsi, zijadili namna ya kuboresha sheria inayozingatia malezi ya watoto.

"Kwa kuwa suala hili linagusa sekta karibu tatu siwezi kutolea maamuzi haya sasa hivi, ila nimelichukua suala hili na nitawafikishia wadau na kulijadili," anasema Balozi Dk. Mahiga.

Meneja Uhusiano Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF),



Angela Mziray, anasema mwanachama yeyote aliyejiunga na mfuko huo atapata huduma na wategemezi wake kulingana na utaratibu wa vifurushi vinavyotolewa.

Anasema kifurushi cha 'Najali' kinachojumuisha wanandoa wenye umri kati ya miaka 18 hadi 35 na mtoto mmoja ada ni Sh. 504,000 kwa mwaka kinatoa huduma ya kulazwa kwa jumla ya siku 30 kwa mnufaika mmoja.

"Huduma ya mfuko inatolewa kulingana na uanachama na aina ya kifurushi, kwa bahati mbaya mama ambaye si mwanachama hawezi kupata huduma mfuko," anasema Mziray.

Pia kifurushi cha 'Wekeza' kwa mwanachama mwenye umri huohuo wanatoa na mtoto mmoja ada ya mwaka ni Sh. 924,000 na huduma ya kulazwa mnufaika siku 45 kwa mwaka.

Aidha, anataja kifurushi cha 'Timiza' kwa mwanachama mwenye umri wa miaka 18 hadi 35, wanandoa na mtoto, ada yake ni Sh. 1,272,000 na kutoa huduma ya kulazwa kwa mnufaika kwa siku 60 kwa mwaka.

**WANAHARAKATI**

Mkurugenzi wa Mtandao wa Jinsia (TGNP), Lilian Liundi, anaeleza hitaji la mabadiliko katika kinamama wanaojifungua njiti na kutozwa kiasi kikubwa cha pesa hospitalini.

"Suala la kupata watoto njiti bado linasumbua. Unasikitika sana na hapo unakuwa na uhakika kuwa mtoto wangu anaweza kuwa hai au hataweza.

"Kipindi cha miezi mitatu au miwili ni mingi sana kukaa hospitali na wewe kama mama kwa muda wote, shughuli zako zinasimama kwa muda wa miezi hiyo," anasema Lilian anayependekeza likizo ya ziada kwa wanaojifungua njiti, anaongeza:

"Sio waajiri wengi wanafikiria suala hili, kwa sababu ukae hospitali miezi mitatu bado 'maternity leave' (likizo ya uzazi) miezi mitatu, mwajiri anakuwa haelewi kabisa na mama unapata adhabu mara mbili au ufukuzwe kazi."

"Wengine unakuta wanajifungua hospitali zetu hizi kutokana na kipato na wengine wanatengwa kabisa. Wodi za watu kama hawa zilitakiwa ziboreshwe ili na wao wajisikie ni sehemu ya kujivunia na sio adhabu.

"Kiukweli hawa wanawake hawatakiwi kudaiwa huduma hata kama kajifungua mtoto njiti. Inatakiwa huduma hii iwe bure na igharamiwe na pesa za walipa kodi na ukisema uanze kumdai mama pesa na wakati kisaikolojia ameathirika kutokana na kujifungua mtoto njiti."

Balozi Getrude Mongella, aliyeongoza Bunge la Kinamama jijini Beijing China, miaka 25 iliyopita anasema ajenda kuu ya kumkomboa mwanamke na kumpunguzia changamoto za afya hususan uzazi, bado harakati zinahitajika kumkwamua.

AFYA

# Virusi, vimelea, njia za hewa ni chanzo cha mafindo, tezi

**Na Mwandishi Wetu**

TATIZO la kuvimba tezi za kooni au mafindofindo ambayo baadhi ya watu huyaita 'matonsesi' yana vyanzo mbalimbali, lakini kimojawapo ni virusi pamoja na bakteria.

Matezi au tezi ambalo ni sehemu ya kinga hushambuliwa na virusi ama vimelea vya magonjwa vinavyoingia mwilini kupitia kinywani.

Magonjwa hayo yanaweza kutibiwa hivyo ni vyema kuzitizama aina za matibabu ambayo ni ya kutumia dawa, lakini kuna matibabu yanayoweza kufanyika nyumbani bila kumeza dawa au kufanyiwa upasuaji.

**MATIBABU NYUMBANI**

Iwapo tatizo la kuvimba tezi limesababishwa na virusi au bakteria na zipo njia mbalimbali zinazoweza kufanyika nyumbani kumsaidia mgonjwa.

Iwapo chanzo cha kuvimba kwa tezi kumesababishwa na virusi, daktari anampangia dawa za kuua vimelea.

Mara nyingi kwa njia hii ya matibabu ya nyumbani mgonjwa hupata nafuu au kupona baada ya siku saba hadi 10.

Njia zinazoweza kutumika katika tiba mtu akiwa nyumbani, ni pale chanzo cha kuvimba kimebainika kuwa ni virusi. Moja inashauriwa mgonjwa apumzike na iwapo kama ni mtoto, mzazi wake anapaswa kumshawishi apate muda wa kutosha kulala kikamilifu.

Pia inalaezwa mtoto huyo asisahau kutumia maji ya kutosha, kwani hii nayo ni tiba. Mwangalizi au mzazi anapaswa kumpatia mtoto au mgonjwa maji kila mara, ili kusaidia kuzuia koo kubaki kavu, hali inayosababisha mara nyingine ajihisi vibaya.

Kusukutua kwa kutumia maji yenye chumvi, ni aina nyingine bora ya kumsaidia mgonjwa. Anapaswa kutumia maji yalichanganywa na chumvi, walau kijiko kimoja cha chai kwa glasi moja ya maji ya vuguvugu.



Ilivyo sura halisi ya tezi na inavyosumbua. **PICHA : MTANDAO.**

> **Pia, kula kwa kuepuka kushirikiana chakula, glasi za vinywaji kama maji, chupa za maji au vyombo vingine vya kulia chakula.**

Baada ya kuchanganya, mtumiaji atasukutua maji hayo hayo kwa muda mfupi, kisha anatema. Hiyo inamsaidia kuleta nafuu mgonjwa, kwani chumvi inaua vimelea.

Mafindofindo kwa kawaida huambatana na homa, hivyo mtu anapaswa kujadili na daktari kuhusu utumiaji dawa za kupunguza maumivu, ili kumsaidia kumaliza maumivu ya koo au kudhibiti homa.

Hata hivyo, homa zisizoambatana na maumivu ya koo hazihitaji matibabu. Katika hali zote hizo za matibabu, inashauriwa kutotumia dawa aina ya aspirini katika kipindi chochote cha kuugua uvimbaji tezi, kwani inaweza kuleta madhara mengine.

**DAWA**

Iwapo tatizo la kuvimba tezi limesababishwa na bakteria, daktari humpangia mgonjwa dawa za kutumia mara nyingi kundi la antibaiotiki. Wapo watu au watoto ambao wana mzio au 'aleji' na dawa hizo na hivyo daktari humpangia mgonjwa dawa nyingine tofauti.

Hata hivyo, ni muhimu sana kwa mgonjwa kumaliza dozi ya dawa hata kama dalili za ugonjwa zimekwishatokomea.

Kushindwa kumaliza dawa kutasababisha tatizo kuzidi kuwa kubwa kwa bakteria kusambaa na kuvamia sehemu nyingine za mwili. Ni hali ya kusambaa bakteria na kusababisha mtoto au mgonjwa kuwa kwenye hatari kubwa ya kupata tatizo la kuvimba figo.

**UPASUAJI**

Iwapo mtu anaandamwa na tatizo la kujirudia kwa kuvimba tezi na kusababisha dawa za kutibu bakteria kushindwa kufanya kazi vizuri, upasuaji wa kuondoa tezi waweza kuwa njia bora zaidi ya kumaliza tatizo.

Tezi zinazohitaji kufanyiwa upasuaji ni zile ambazo zina vigezo vifuatavyo: Mtu anapopata tatizo la kuvimba tezi zaidi ya mara saba katika kipindi cha mwaka mmoja.

Hivyo, iwapo uvimbaji tezi unamsababishia mgonjwa hali ya kuziba kwa njia ya hewa na hushindwa kupumua vizuri akiwa amelala.

Kadhalika, pale mgonjwa anapopata tatizo kubwa la kumeza chakula na inasababisha mgonjwa atoe usaha kwenye sehemu ya tezi na akitibiwa kwa dawa za bakteria hapati nafuu.

**JINSI YA KUZUIA**

Virusi na bakteria wanaosababisha tatizo la kuvimba kwa tezi huambukizwa kutoka kwa mtu mmoja kwenda mwingine. Kwa maana hiyo, njia pekee ya kuzuia ni kujiweka katika hali ya usafi kila wakati.

Kama mzazi, unapaswa kumfundisha mwanao mambo kadhaa kama kunawa mikono kila mara, hasa baada ya kutoka chooni na kabla ya kula.

Pia, kula kwa kuepuka kushirikiana chakula, glasi za vinywaji kama maji, chupa za maji au vyombo vingine vya kulia chakula.

Ili kuepuka mtoto kuwaambukiza wengine, mzazi anapaswa kumhimiza mtoto kubaki nyumbani kipindi chote anachougua na kumfundisha kupiga chafya kwa kujikinga, kwa kutumia kitambaa au kama hana atumie mkono.

Mtoto pia awe na tabia ya kunawa mikono kila mara baada ya kupiga chafya au kukohoa.

***Kwa mujibu wa mtandao wa afya***

# Mfumo mpya takwimu mtandaoni unavyoleta mapinduzi

**INATOKA UK.17**

Meneja Operesheni wa USAID kupitia Mradi wa Maji (WALIS), Alayne Potter, anasema shirika hilo linasaidia kuboresha mfumo wa afya, kwa kutumia njia ya teknolojia ya digitali kuboresha utoaji takwimu sahihi za afya.

Mfumo wa Portal unatajwa, nafasi yake ipo pale takwimu zake hazitatumika katika kuboresha usafi na kuleta mabadiliko.

**MTAALUMA MUHAS**

Mshiriki, ambaye ni Mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) katika kitivo cha Afya ya Mazingira na Kazi, Dk. Gloria Sakwari, anasema wahadhiri watanufaika na mfumo huo kwa kuwa mara nyingi wanapofundisha au kuandika machapisho au mapendekezo ya kufanya tafiti fulani taarifa ni muhimu kwaom, iliyokuwa ngumu kuzipata.

"Mimi kama mtafiti, naona naweza kupata taarifa nyingi ambazo kwa kipindi cha nyuma zilikuwa na matatizo kuzipata kwa urahisi na uhakika. Lakini, sasa taarifa zinazohusu usafi wa mazingira na vyoo na taarifa nyingi nitapata kupitia kompyuta mpakato yangu mezani kwangu," ameongeza Sakwari.

**OFISA AFYA**

Gaudence Haule, ni Ofisa Afya wa Halmashauri ya Mafinga, anabainisha kuwa mfumo huo ni msaada katika ukusanyaji na kuziingiza takwimu sahihi kutoka kwenye maeneo ya vijiji na mitaa na baadae kutumia viashiria kutengeneza, vigezo vitakavyotumika kuamua na kuimarisha hali ya afya na usafi wa mazingira.

Anasitiza kuwa Portal inaimarisha mfumo wa wazi na ufanisi na kila kilichofanyika kinaonekana, hivyo ni rahisi kwa ofisa kuchukua hatua za kudhibiti tatizo mwenyewe, pasipo kutegemea msaada toka ngazi za mbali.

Nelson Rumbeli, Ofisa Afya kutoka mkoa Kagera, anaeleza kwamba mafunzo yamewaongezea ujuzi na uwajibikaji zaidi katika ukusanyaji takwimu na mfumo utasaidia kujua taarifa bila kusubiri simu.

Anasema, ni fursa kwa watu kutambua takwimu za magonjwa yatokanayo na ukosefu wa usafi na uchafu wa mazingira mikoani. Rumbeli anaendelea:

"Takwimu zinazokusanya na kuwekwa kwenye mfumo huu, zinatusaidia katika kuandaa taarifa za vikao, mipango ya serikali na mikakati ya utekelezaji wa majukumu yetu kwa ngazi ya mkoa hadi wilaya," amesema Rumbeli.

Ofisa Afya wa Mkoa wa Dodoma, Carle Lyimo, anasema mfumo umeongeza uwajibikaji na kuwezesha mkoa wa Dodoma uliokuwa na viwango cha chini vya usafi kufanya vizuri.

Anasema, kwa sasa mkoa huo upo katika nafasi nzuri ya kuridhisha, hali iliyochangiwa na kujitoa kwa maofisa afya kutembelea na kukusanya taarifa kwa usahihi kutoka katika maeneo yote.



# Wazazi mbaroni kwa tuhuma kuua mtoto

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya linawashikilia watu wawili ambao ni mume na mke, wakazi wa Mtaa wa Pambogo, Kata ya Iyela jijini Mbeya, kwa tuhuma za mauaji ya mtoto wao kisha kumfukia.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake juzi, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alidai tukio hilo lilitokea Desemba 22, mwaka huu saa 12:30 alfajiri.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Ally Mbavu (23) na Sabina Alex (19), ambao wanadaiwa kusababisha kifo cha mtoto wao wa kiume, Ismail Mbavu (mwaka mmoja na miezi 11).

Kamanda Matei alidai watuhumiwa walitoa taarifa tangu Desemba 21 katika Kituo cha Polisi kuwa wamepotelewa na mtoto wao na hivyo wakashirikiana na wananchi wa eneo hilo kumtafuta na ndipo wakampata asubuhi akiwa amefariki dunia na kufukiwa kichwa, huku kiwiliwili kikiwa juu. "Hili tukio ni la kusikitisha na ni unyama mkubwa, hawa watu tunawahisi kuwa wanahusika na kifo cha mtoto huyo kutokana na mazingira ya tukio lenyewe," Kamanda Matei alidai.

Alidai watuhumiwa wanashikiliwa na jeshi hilo wakati upelelezi wa tukio hilo ukiendelea na kwamba baada ya uchunguzi huo kukamilika, watu hao watafikishwa mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria.

Aliwataka wananchi wa Mkoa wa Mbeya kuwa makini kuwalinda watoto wao dhidi ya wahalifu, akisisitiza watoto wadogo hawatakiwi waachwe peke yao.

Akizungumzia tukio hilo, Mwenyekiti wa Mtaa wa Pambogo, Mwaikambo Mwalwisi, alidai kuwa baada ya wazazi hao kutoa taarifa ya kupotelewa na mtoto, alipiga king'ora ili kuwataka wananchi wa eneo lake kushiriki kumtafuta.

Alidai walitafuta ikashindikana kumpata, wakaamua kwenda kulala ili baadaye wawahi asubuhi kuendelea na utafutaji na walipoamka, waliendelea kumtafuta ndipo wakamkuta akiwa amefukiwa jirani na nyumbani kwa wazazi wake.

"Nilipigiwa simu na wananchi wakidai wamemkuta mtoto akiwa amekufa na amefukiwa, nilipofika eneo la tukio, nilitoa taarifa kituo cha polisi ndipo wakaja kupima na kuondoka na mwili kwenda kuuhifadhi," alidai.

Alidai wanandoa hao walikuwa wanakaa kwenye nyumba ya kupanga, hivyo hakuna anayejua kilichotokea mpaka mtoto huyo akafariki dunia na hivyo suala hilo wanaliachia kwa Jeshi la Polisi.

Katika hatua nyingine, Kamanda Matei aliwataka wananchi wa Mkoa wa Mbeya kuwa makini wakati wa sikukuu za mwisho wa mwaka ili kuepuka matukio mbalimbali ya uhalifu.

Alisema Jeshi la Polisi litaimarisha ulinzi katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo yakiwamo maeneo ya makanisa na mitaani ili kuwashughulikia wanaojaribu kuvunja amani.

Alisema vijana wake wako imara kwa ajili ya kukabiliana na vikundi vyote vya uhalifu vitakavyojitokeza huku akizitaka Kamati za Ulinzi za Makanisa kuimarisha ulinzi ili kushirikiana na Jeshi la Polisi.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (wa tatu kulia), akiwakabidhi wakuu wa wilaya za mkoa huo, mabati 3000 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa 59 vinavyohitajika kwa ajili ya wanafunzi wanaotarajiwa kuanza kidato cha kwanza mwakani, lakini majina yao yamezuiliwa. **PICHA NA NEBART MSOKWA**

# TPA yafanya upembuzi bandari za Ziwa Nyasa

**Na Elizabeth Zaya,** KYELA

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari (TPA), imesema inafanya upembuzi yakinifu katika bandari zote za Ziwa Nyasa unaolenga kuboresha miundombinu na kuimarisha shughuli za kibiashara katika ziwa hilo.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Meneja wa Bandari za Ziwa hilo, Abedi Gallius, alipozungumza na waandishi wa habari katika Bandari ya Kiwira iliyopo wilayani Kyela mkoani Mbeya.

Alisema wameamua kuboresha miundombinu ya ziwa hilo ili kurahisisha usafirishaji kwa wananchi wanaozunguka maeneo hayo na kuimarisha shughuli za kibiashara na kukuza uchumi.

Alisema kwa miaka miwili iliyopita, hakukuwa na ongezeko la shehena kutokana na ukosefu wa meli na kwamba kufanyika kwa maboresho hayo, kutasaidia kukuza biashara kwa kasi kuanzia Januari mwakani.

Alisema wanatarajia kuanza kupitisha shehena za makaa ya mawe, tani 4,000 kila mwezi kuanzia mwakani.

"Mwezi wa kwanza (Januari) 2020, tutaanza kupitisha shehena za mkaa wa mawe, na baada ya hapo, tunatarajia kwamba biashara itakuwa nzuri zaidi, na tunaendelea na mikakati ya kimasoko ili watu waanze kutumia njia ya maji badala ya barabara," alisema.

Aliongeza kuwa miaka mitano iliyopita, walikuwa wakihudumia kati ya tani 5,000 hadi 10,000 kwa mwaka na mapato yalikuwa yanafikia Sh. milioni 300 kwa mwaka na kwamba kwa sasa baada ya kuboresha miundombinu na uwekezaji wa meli uliofanya, wanatarajia kuanza kusafirisha mizigo zaidi na kuzalisha faida kubwa.

"Lakini, kwa mipango tuliyonayo kwa sasa, tunatarajia kwamba tutafikia hadi kuhudumia tani 76,000 kwa mwaka na mapato kufikia Sh. bilioni tatu kwa mwaka.

"Mwanzoni shida iliyokuwa inachangia kutokusafirisha shehena nyingi, ni kukosekana kwa vyombo vya kusafirishia mizigo, bandari siku zote haiwezi kufanya kazi kama hakuna vyombo vya kusafirishia. Kwa hiyo, uwekezaji wa meli uliofanywa na serikali kwa sasa ndiyo unakwenda kuchagiza ongezeko hilo la shehena pamoja na mapato," alisema.

Alibainisha kuwa Ziwa Nyasa lina bandari rasmi 15, huku asilimia 90 ya mizigo inayosafirishwa katika bandari za ziwa hilo ikiwa ni makaa wa mawe.

Alitaja bandari hizo kuwa ni pamoja na Itungi, Kiwira, Matema, Lumbila, Ifungu, Nsisi, Makonde, Lupingu, Manda, Liuli na Mbamba Bay.

## Wanaume wapewa neno kuishi na mke

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANAUME wa Mkoa wa Mbeya wameshauriwa kushirikiana na wake zao katika kufuatilia afya za watoto wao ikiwa ni pamoja na kushiriki kuwapeleka kliniki ili kuhakikisha wanakua wakiwa na afya njema.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Mariam Mtunguja, wilayani Chunya wakati wa ziara ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, akieleza kuwa baadhi ya wanaume wamekuwa wakiacha jukumu hilo kwa wanawake peke yao.

Aliwataka wanaume kuwasindikiza wake zao kliniki wanapokuwa wajawazito ili wapewe elimu juu ya namna bora ya kuishi katika kipindi chote cha ujauzito ili kulinda afya ya mama na mtoto atakayezaliwa.

Mtunguja alisema kwa sasa, serikali imeimarisha huduma za afya, hivyo ni wajibu wa wananchi kuzitumia vizuri huduma ikiwa ni pamoja na kukabiliana na vifo vya mama wajawazito na watoto wachanga.

"Katika mkoa wetu wa Mbeya, Kijiji cha Bitimanyanga ndicho cha mfano kwa wanaume kushiriki kuwasindikiza wake zao kliniki na kuwapeleka watoto wao kuwapima, sasa nawashauri kinababa sehemu zote za mkoa huu kuiga mfano huo," alishauri.

Alisema elimu inayotolewa kwenye vituo vya afya inasaidia kukabiliana na udumavu ambao unawakabili watoto katika mkoa huo, licha ya kuwa miongoni mwa mikoa inayozalisha chakula kwa wingi.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, aliwataka wananchi wilayani Chunya kuzingatia njia za uzazi wa mpango ili kupunguza kasi ya kuzaliana pamoja na kulinda afya za wanawake.

Alisema baadhi ya wanaume hasa jamii za kifugaji, hawajali uzazi wa mpango na badala yake wao ni kuwazalisha wake zao kila mwaka hali ambayo inadhoofisha afya za wanawake, huku idadi ya watu ikiongezeka kwa kasi kubwa nchini.

"Nawaomba na ninyi kinamama, muwe mnawaelimisha waume zenu kuhusu uzazi wa mpango, siyo kila mwaka unazaa mtoto na matokeo yake kasi ya ongezeko la watu inakuwa kubwa na kuhatarisha hata misitu," alilalamika.

Baadhi ya wanawake wa Kijiji cha Bitimanyanga walisema wanashindwa kutumia njia za uzazi wa mpango kutokana na kulazimishwa na waume zao kuzaa watoto wengi.



# Vigogo wa ranchi wapewa siku 38 kuongeza mapato

**Na Paul Mabeja,** KONGWA

KATIBU Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Elisante Ole Gabriel, ametoa siku 38 kwa ranchi ya mifugo Kongwa kujenga duka la kuuza nyama kando ya barabarani kuu ya Dodoma-Morogoro ili kujiongezea mapato ya ndani.

Ole Gabriel alitoa agizo hilo jana alipotembelea shamba la mifugo la ranchi ya Kongwa kukagua miradi ya maendeleo hususani uchinjaji na uuzaji wa nyama ya ng'ombe.

Alisema kwa sasa wateja wamekuwa wakipata tabu kufuata nyama eneo la ndani ya ranchi hiyo kwa umbali wa zaidi ya kilomita mbili kutoka barabarani, hali inayosababisha idadi ya wateja kupungua na kukosekana kwa mapato ya kutosha.

"Nawaonyesha eneo hapo barabarani ifikapo Januari 31, mwakani, nataka Waziri Luhaga Mpina aje kuzindua duka hilo, kufuata nyama huku ndani imepitwa na wakati na haifai kwani biashara ya sasa wateja wanataka uwapelekee bidhaa jirani na eneo lao," aliagiza.

Vilevile, kiongozi huyo wa wizara alionya tabia ya baadhi ya watumishi wa ranchi hiyo kutumia lugha mbaya kwa wateja, akieleza kuwa inawapunguzia sifa na amekuwa akipokea malalamiko kutoka katika maeneo mbalimbali kuhusu suala hilo.

Meneja wa Ranchi ya Kongwa, Raymond Lutege, akisoma taarifa ya ranchi hiyo, alisema kituo chao kinazalisha nyama bora ambayo inauzwa katika maduka yao yaliyoko Dodoma Mjini, Morogoro, Kibaigwa na Kongwa.

Lutege alisema katika ranchi hiyo, wanao ng'ombe 9,919, mbuzi 1,336, kondoo 748, nguruwe 127 na farasi saba ambao ni wanyama wa kazi.

Pia, meneja huyo alisema bado wanakabiliwa na tatizo kukosa mtaji kwa ajili ya kuongeza uzalishaji kwenye soko la nyama.

Kaimu Meneja Mkuu wa Kampuni ya Ranchi za Taifa (Narco), Mipawa Masele, alisema wanalenga kuwekeza zaidi katika ranchi zote licha ya kukabiliwa na vikwazo vya uvamizi wa maeneo yao.

Masele alisema kwa mwaka wa fedha 2019/20, wanalenga kukusanya Sh. bilioni tisa na kwa Kongwa pekee, wameshakusanya Sh. bilioni 1.1 katika kipindi cha miezi mitano iliyopita.

"Lakini, pia katika kujiongezea mapato, tumepanga kuongeza uzalishaji ili kuondokana na utegemezi kwa hapa Kongwa kuongeza idadi ya ng'ombe kufikia 12,000.

"Pia kuweka utaratibu wa kununua ng'ombe kutoka kwa wadau wengine ili kuongeza uzalishaji wa nyama na kukidhi soko la nyama ndani na nje ya nchi," alitamba.

Ranchi ya Kongwa ilianzishwa na serikali ya kikoloni mwaka 1948 na kutangazwa rasmi na serikali mwaka 1974.



Msaidizi wa Askofu Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKKT) Dayosisi Dodoma, Mchungaji Christian Ndossa (kulia), wakitakiana heri ya sikukuu ya Krismas na Mchungaji Humphrey Sam wa kanisa hilo, Mtaa wa Kisasa jijini Dodoma, baada ya Ibada ya Sikukuu ya Krismasi iliyofanyika kanisani hapo jana. **PICHA: JOSEPH IBRAHIM**

# Spika awataka kuwekeza upandaji miti

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amewataka wakazi wa mikoa ya Kanda ya Kati kuanza kuwekeza katika upandaji miti badala ya kujikita katika kilimo pekee ili kuwasaidia kujikwamua kiuchumi kama ilivyo kwa mikoa ya Kilimanjaro, Kagera na Mtwara.

Kiongozi huyo wa Bunge aliyasema hayo wakati akizundua miradi wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) ya kuwawezesha wanawake kujikwamua kiuchumi inayotekelezwa katika Tarafa ya Zoisa wilayani Kongwa jijini Dodoma kupitia vikundi 52.

Alisema wananchi wa mikoa hiyo hawana budi kuachana na kilimo cha kutegemea mahindi peke yake, badala yake wajikite kwenye mazao ya miti ambayo ni ya muda mrefu na yanaweza kumtajirisha mtu na vizazi vyake vijavyo.

"Ukijiuliza kwanini sisi Kanda ya Kati ni maskini, jibu la haraka ni kwamba hali ya hewa na aina ya kilimo, miaka kadhaa kunakuwa hakuna mavuno na mwaka mwingine unakuwa mzuri.

"Shida yetu ni kuwa, tukivuna katika kipindi ambacho mikoa mingine yote pia imevuna, sasa mtu ukiwa na bidhaa ambayo wengine wanayo, huwezi kupata faida," alifafanua.

Alisema uwekezaji katika upandaji wa miti ni muhimu kwa sasa kwa mikoa hiyo kupiga hatua kiuchumi, akiitolea mfano mikoa ya Kiliminjaro, Iringa, Kagera na Mbeya ambayo alikiri iko tofauti kwa kiwango kikubwa na ya Kanda ya Kati.

Alisema maeneo yetu hayakubali kahawa, lakini kilimo cha korosho, zabibu vinakubali, kila mmoja anapaswa kusimamia kilimo hicho ili kuondokana na umaskini.

Alivitaka vikundi hivyo kuhakikisha miradi hiyo ya kanisa inatumika vyema kukuza uchumi wao, akiahidi kuunga mkono kwa kuelimisha jamii kuwa umaskini si mpango wa Mungu.

Katibu Mkuu wa CCT, Canon Moses Matonya, alisema wana wajibu wa kuhakikisha uchumi wa wananchi unakua hususani kupitia vikundi mbalimbali vya wanawake, hivyo ni lazima miradi hiyo isimamiwe ili ilete tija katika jamii.

Alisema lengo lao ni kuhakikisha wanatekeleza miradi hiyo Tanzania nzima, hivyo vikundi vya Dodoma vinatakiwa kuwa mfano wa kuigwa.

Mwakilishi wa vikundi hivyo, Talita Mazengo, alisema wanatekeleza miradi ya ufugaji nguruwe, kuku, mbuzi, ng'ombe, nyuki, samaki, kilimo cha alizeti, karanga pamoja na kilimo cha umwagiliaji.

Mazengo alisema wanakabiliwa na vikwazo kadhaa ikiwa ni pamoja na ukosefu wa dawa na kinga kwa magonjwa nyemelezi, upungufu wa fedha kwa ajili ya kumalizia bwawa la samaki Sh. 400,000, ukosefu wa mbegu za kilimo cha mboga.

Alisema malengo ni kuwa na miradi endelevu, makazi bora, ikiwamo kusomesha watoto na kuchangia huduma mbalimbali za kijamii.

# Waziri aanika fursa uwekezaji Dodoma

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Anthony Mavunde, amewataka wawekezaji kuwekeza shughuli mbalimbali za kiuchumi jijini Dodoma, kutokana na kukua kwa uchumi na mji huo.

Mbali na hilo, Mavunde pia amewataka wakazi wa Mkoa wa Dodoma kuchangamkia fursa hiyo ya uwekezaji ili wajiinue kiuchumi.

Mavunde alisema hayo juzi wakati wa uzinduzi wa hoteli ya kisasa ya Emirates jijini hapa alipokuwa akizungumza na wawekezaji pamoja na wananchi jijini hapa.

Alisema kutokana na kukua kwa uchumi kwa hivi sasa kulikochangiwa na uwapo wa makao makuu ya serikali, wawekezaji na wananchi wanatakiwa kuwekeza katika shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Aliwataka wawekezaji kuhakikisha wanatoa kipaumbele kwa wazawa katika kutoa ajira kulingana na uwezo na sifa za mwombaji.

"Tunawashukuru wawekezaji ambao wameamua kuwekeza na kuamua kuwaajiri vijana wetu ambao hivi sasa pia wameamua kuchangamkia fursa hizi," alisifu.

Mmiliki wa hoteli hiyo, Mahmoud Ali, alisema anaamini wawekezaji wengi watachangamkia fursa hizo na kinachotakiwa ni kupewa ushirikiana na watoa uamuzi ili kuondoa na urasimu unaokwamisha uwekezaji.

Shekhe wa Mkoa wa Dodoma, Mustapha Rajabu, aliwataka wakazi wa Dodoma kujishughulisha na biashara mbalimbali badala ya kusubiri watu wengine kuchangamkia fursa zilizoko jijini humo.

Alisema serikali imeamua kuweka makao yake jijini humo, hivyo ni muhimu wakazi wake wakakimbilia fursa hizo ili wajiongeze kipato.



## Wahimiza wanawake kujiandikisha daftari la kudumu la wapigakura

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UMOJA wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), umewataka wanawake kujitokeza kwa wingi kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura ili kujiweka sawa kwa maandalizi ya uchaguzi mkuu mwakani.

Naibu Katibu Mkuu wa (UWT) Zanzibar, Tunu Kondo, alisema jana kuwa kujiandikisha katika daftari hilo ni haki ya kila mwananchi mwenye sifa.

Alisema huwezi kupiga kura katika uchaguzi mkuu kama taarifa zako hazimo kwenye daftari hilo, hivyo akawataka wanawake wasikubali kukosa fursa hiyo muhimu.

"Wapo baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa wameanzisha vitisho kwa ajili ya kuwazuia baadhi ya wananchi kutumia haki yao kidemokrasia kupiga kura katika uchaguzi mkuu kwa malengo ya kisiasa," alidai.

Tunu pia aliwataka wanawake kujitokeza kuwania nafasi za uongozi katika majimbo ya uchaguzi kwa lengo la kutimiza azma ya kufikia asilimia 50 kwa 50 katika vyombo vya uamuzi.

Alisema hakuna majimbo ya uchaguzi ambayo ni haki miliki ya mtu binafsi, akisisitiza kuwa wanawake wanatakiwa kujitokeza kuwania nafasi hizo wakati ukifika.

"Wanawake tunataka kufikia asilimia 50 kwa 50 iliyowekwa kuingia katika vyombo vya uamuzi vya kutunga sheria na njia pekee ya kufikia malengo hayo ni kuwania nafasi za uongozi katika majimbo ya uchaguzi," alifafanua.

Mlezi wa Umoja wa Wanawake, Khadija Jabir, alisema wanawake ndiyo nguzo na mategemeo ya CCM katika ushindi wake.

Alisema kama wanawake watakaa nyuma, ni dhahiri kwamba ushindi kwa chama hicho utayumba na kuingia dosari kubwa.

"Huu ni wakati wa wanawake kushika nafasi za uongozi, hivyo msikubali kujiweka nyuma, nendeni katika daftari la kudumu la wapigakura kujiandikisha kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa mwakani," alihimiza.

# Askofu aipa neno CCM

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

ASKOFU wa Kanisa Katoliki Jimbo la Zanzibar, Augustine Ndeliakyama Shao, amekitaka Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuweka mtazamo kwamba ushindani wa kisiasa si uadui bali ni ulinganisho wa sera.

Askofu Shao alisema hayo jana wakati wa ibada ya Krismasi katika Kanisa Katoliki la Minara Miwili lililoko Shangani mjini Zanzibar.

Katika ibada hiyo, ujumbe maalum wa Krismasi ulikuwa ukisema haki, amani na usawa kwa wote.

Alisema kuanzishwa kwa siasa ya vyama vingi nchini ni kuwapa Watanzania nafasi ya kulinganisha sera, kuchagua viongozi, kupongeza, kuwajibisha, kukosoa na kufichua udhaifu wa serikali.

"Migogoro inayoendelea sasa katika baadhi ya vyama vya siasa inaashiria utata wa kukosekana haki, amani na usawa tunayotamani," alisema.

Askofu Shao pia alidai uchaguzi wa viongozi wa serikali za mitaa uliofanyika hivi karibuni ulikuwa na viashiria vya kutokuwa na picha nzuri. Kiongozi huyo wa kiroho pia alizungumzia kuwapo kwa matamko kwa baadhi ya viongozi wa siasa ambayo yamegeuka kama sheria, jambo ambalo alidai ni hatari katika kulinda haki na amani inayotakiwa.

"Kisheria mtuhumiwa huhesabiwa ana kosa au mhalifu ndani ya mahakama baada ya kupewa haki ya kujitetea, ni muhimu kwa viongozi wetu watafakari matamko yao, watambue wanachosema siyo sheria, bali ni maelekezo au maagizo," alishauri. Alisema haki na amani kwa wote ni chombo kinachowaleta pamoja hasa maskini, hivyo ni lazima kila mmoja ahusishwe kuleta mabadiliko ya maendeleo ya nchi.

Naye Askofu wa Kanisa la Anglikana Mkunazini Unguja, Dk. Michael Hafidh, aliipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuimarisha amani na utulivu katika kipindi chote.

Alitaka juhudi hizo za serikali inayoongozwa na Dk. Ali Mohamed Shein, kulindwa kwa nguvu zote wakati nchi inaelekea kwenye mchakato wa harakati za uchaguzi mkuu mwakani.

"Sisi Wakristo wa Zanzibar tunaridhishwa na uwapo wa amani na utulivu chini ya Rais Ali Mohamed Shein, tunataka waweke mkazo zaidi tunapoelekea kwenye uchaguzi mkuu wa mwakani," alishauri. Kiongozi huyo wa kiroho aliwataka wananchi wakiwamo waumini wa kanisa hilo, kutumia nafasi ya kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura ili kutumia haki yao ya kikatiba.

Alisema huwezi kupiga kura na kuchagua viongozi wakuu wa serikali kama utashindwa kuandikishwa katika daftari hilo.

"Huo ndiyo wito wetu, watu waliokuwa hawajaandikishwa katika daftari la kudumu la wapigakura, waitumie nafasi hiyo, ndiyo neema kutoka kwa Rais Shein," alisema.

"Pia nasikitishwa sana na wimbi la matukio ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia kwa jamii yetu huku watoto na wanawake chini ya umri wa miaka 18 wakiathirika vibaya," aliongeza.



Waumini wa Kanisa la Anglican Mkunazini Zanzibar, wakifuatilia ibada ya mkesha wa Krismasi kwenye kanisa hilo jana.
**PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Akosoa jamii watoto kulelewa vituo maalum

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JAMII imetakiwa kujihusisha na malezi ya watoto yatima na wanaoishi mazingira magumu, badala ya kuwapeleka katika vituo maalum vya kulelea watoto yatima.

Wito huo ulitolewa na mratibu wa mradi wa malezi mbadala unaosimamiwa na Shirika la SOS la Zanzibar, Nyezuma Simai, wakati akizungumza na waandishi wa habari jana.

Alisema watoto hao wanapolelewa katika familia zao, huwa katika malezi bora kuliko wanapoishi katika vituo vya kulea watoto yatima.

Alisema utaratibu huo wa kulea watoto katika vituo si mzuri kwa sababu hauleti suluhisho la mwisho. Alisema watoto 50 waliokuwa katika mradi huo katika Kisiwa cha Tumbatu, Mkoa wa Kaskazini Unguja, wamefaidika kwa kupata huduma za bima ya afya mara mbili.

Alisema mradi huo ambao unatekelezwa katika kisiwa hicho kidogo, una lengo la kuwawezesha watoto waliopoteza wazazi wao kuendelea kuishi chini ya wazazi na ndugu wa karibu.

"Mradi wa malezi mbadala lengo lake ni kuhakikisha watoto wanalelewa kutokana na ndugu wa karibu na kuwapatia huduma zote muhimu ikiwamo elimu," alisema. Baadhi ya wananchi walioshiriki katika mradi huo, walitaka kuwekwa mkazo zaidi katika suala la ufuatiliaji wa familia hizo katika maendeleo ya sekta elimu.

Sheha wa Tumbatu Gomani, Ussi Nyange, alisema bado familia nyingi katika kisiwa hicho hazina utamaduni wa kufuatilia nyendo za watoto wao wanapokuwa shuleni. Sheha wa Tumbatu Uvinze, Miza Ali, alilipongeza Shirika la SOS kwa kutekeleza mradi huo kisiwani humo na kuonyesha mafanikio makubwa.

"Tumeshuhudia mafanikio ya mradi wa malezi mbadala, tumeona jinsi ulivyobadilisha maisha ya watoto na malezi kubwa bora," alisema.

Fatuma Juma (61), mzazi anayeishi na watoto wawili wanaofaidika na mradi huo, alisema amefaidika na huduma zinazotolewa na taasisi hiyo na hivyo kuweza kuwamudu watoto hao katika kupata huduma muhimu ikiwamo elimu.

HABARI KITAIFA



Mbunge wa Musoma Vijijini mkoani Mara, Profesa Sospeter Muhongo (mwenye tisheti ya bluu) na wakazi wengine wa jimboni mwake, wakiwa na moja ya majembe ya kukokotwa na ng'ombe, ambayo aligawa kwa vikundi 20 vinavyojishughulisha na kilimo, ikiwa ni kampeni ya kupunguza matumizi ya jembe la mkono. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Serikali yamaliza mgogoro wa wananchi na wawekezaji

**Na Mwandishi Wetu,** KAGERA

SERIKALI imemaliza mgogoro wa ardhi baina ya wananchi na Kampuni ya Ranchi za Taifa (Narco) uliodumu kwa zaidi ya miaka 15.

Mgogoro huo umemalizwa baada ya Waziri ya Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, kuamua wakazi wa vijiji vilivyokuwa ndani ya ranchi hizo kubaki na kuendelea na shughuli za kilimo na ufugaji.

Uamuzi huo wa Waziri Mpina umekuja ikiwa ni utekeleza agizo la Rais John Magufuli la kumega maeneo ya serikali zikiwamo ranchi hizo na kugawia wananchi wa vijiji vilivyokuwamo ndani badala ya kutakiwa kuondoka .

Mpina alikuwa akizungumza na wananchi wa vijiji vilivyokuwa vinatakiwa kuhama kupisha wawekezaji walioko ndani ya ranchi hizo ambao wengi wao walimiliki maeneo makubwa na kushindwa kuyaendeleza kwa mujibu wa mikataba na kushindwa kulipa kodi stahiki za serikali.

Akiwa kwenye mikutano ya hadhara kwenye vijiji hivyo vinavyopakana na ranchi ya Misenyi na Rutolo kando ya Ranchi ya Kagoma, Mpina aliamuru vijiji vya Kankuyu, Bugango, Bweju, Gubal, Mishambya, Kiobuheke, Buyegelegele, Chobokwe na Rutolo visihamishwe na wananchi waendelee na shughuli zao.

Uamuzi huo ulipokewa kwa furaha na wananchi wa maeneo hayo na kumshukuru Rais Magufuli kwa kukubali mashamba hayo kugawiwa kwa wananchi. Kutokana na uamuzi huo, Mpina alimwagiza Kaimu Meneja Mkuu wa Narco, Masele Mipawa, kuweka mipaka mipya ndani ya mwezi mmoja ili kuwawezesha wananchi kuheshimu mipaka hiyo.

Pia aliiagiza Narco kufanya mapitio ya mikataba kwa wawekezaji wote wa ardhi na kwamba yule ambaye hajawekeza ipasavyo kwa mujibu wa mkataba, shamba lake likatwe na kugawa kwa Watanzania wengine wenye uhitaji wa ardhi.

Aidha, Waziri Mpina alielezea kukasirishwa kwake na kitendo cha wawekezaji wa muda mrefu kushindwa kulipa kodi stahiki za serikali sambamba na kushindwa kuweka mifugo kwa mujibu wa mikataba huku wananchi wengine wakikosa mahali pa kulisha mifugo yao.

"Tangu uingie mwaka 2007 mpaka leo unadaiwa kodi eti unaenda kuishtaki serikali mahakamani. Ni dharau gani hiyo kwa serikali? Yaani mmetudharau kwa kiwango gani badala ya wewe kujua wajibu wako? Lipa halafu dai haki yako," alisema.

Mpina alisema dharau hizo kwa serikali zimeshapitiliza na kuweka msimamo kuwa serikali tutakwenda nao mahakamani hata kama miaka 10 wakati ng'ombe wa wawekezaji hao wakiwa nje ya ranchi.

Alisema haiwezekani watu wanashikilia maeneo makubwa ambayo hawayafanyii kazi huku wananchi wengine wanahangaika kutafuta malisho na kutoa mwezi mmoja jambo ambalo kamwe serikali haiwezi kulikubali kuendelea.

Aidha, Waziri Mpina aliwapongeza wawekezaji wa muda mfupi kwa ulipaji mzuri wa kodi za serikali za kupanga maeneo hayo hakuna anayedaiwa huku akiwashukia vikali wawekezaji wa muda mrefu kwa kuzigeuza ranchi hizo kuwa mali zao na serikali ilipowataka kulipa malimbikizo ya kodi waliipeleka mahakamani.

Aliongeza kuwa wananchi wanakosa mahala pa kulima wanajinyima kwa sababu wanajua ni mali ya umma, hivyo serikali haiwezi kukubali wananchi kujinyima halafu ananufaika mtu mmoja.

"Unawanyanyasa wananchi kwa kukosa eneo la kulima, kukosa maeneo ya kuchungia unamfuga mtu mmoja ananufaika hata kodi halipi halafu anakutishia kwenda mahakamani na nitakuja kuendesha hiyo operesheni mwenyewe," alisema.

Waziri alisema ndani ya mwezi mmoja kama wawekezaji hao hawatalipa kodi za serikali, wataingiza Watanzania wengine wazalendo ambao watalipa kodi ya serikali.

Pia ameigiza Narco ipitie upya hesabu za wawekezaji na iyaondoe maeneo ambayo hayamo kwenye shughuli zao za mifugo ili walipie kodi ambayo ni halali yao.

# Wadaiwa kutafuna mamilioni Tasaf

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

VIONGOZI wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf) wilayani Tunduru mkoani Ruvuma, wamedaiwa kutafuna mamilioni ya fedha za miradi ya kusaidia kaya zilizo katika mazingira magumu.

Taarifa kuhusu tuhuma za ufisadi huo zinadai kuwa fedha hizo zilizotafunwa kiujanja na viongozi hao, zilitolewa na serikali ya awamu ya tano Novemba, 2018, ili kulipwa kwa walengwa na badala yake zikaishia mikononi mwa wajanja wachache.

Fedha hizo, kwa mujibu wa taarifa hizo, zilipangwa kuwalipa posho wanakamati ambao walisimamia shughuli (kazi) za ajira za muda, mradi uliobuniwa na kutekelezwa na Tasaf katika kipindi cha Agosti hadi Oktoba, 2018 kwa lengo la kuboresha vipato kwa wananchi wanaonufaika na mradi huo kutoka katika kaya hizo.

Mmoja wa maofisa waliochunguza madai hayo (jina linahifadhiwa), alisema wajanja hao walikula baadhi ya fedha za malipo ya miezi yote mitatu zilizotakiwa kulipwa kwa wanakamati wa vijiji vilivyopo pembezoni ambavyo ni miongoni mwa vijiji 88 vinavyotekeleza mradi huo wilayani hapa.

Baadhi ya wanakamati waliofanyiwa ufisadi huo walidai kuwa kupitia utaratibu huo, maofisa hao wametafuna zaidi ya Sh. milioni 10.

Viongozi hao ambao walionyesha baadhi ya nyaraka kutoka ofisi ya Tasaf wilayani hamo, walithibitisha kuwa zaidi ya wanakamati 260 kutoka vijiji 67 kati 88 vyenye wanakamati 352 vinavyotekeleza mradi huo, hawajalipwa posho zao za mwezi mmoja kila mmoja wao.

Uchunguzi uliofanywa na mwandishi wa habari hizi unaonyesha kuwa ili kuwafunga midomo baadhi ya wanakamati, wajanja walilipwa wastani wa Sh. 276,000 kila mmoja wao ikiwa ni fedha ya malipo ya posho za miezi miwili kati ya mitatu waliyotakiwa kulipwa.

Aidha, kupitia uchunguzi huo pia ulionyesha kuwa wanakamati kutoka katika tarafa zilizopo maeneo ya mjini wao walemlipwa fedha za miezi mitatu yote jambo linaloonyesha kuwagawa katika matabaka ya watendaji wa Tasaf vijijini na mjini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, Gasper Balyomi, alipoulizwa kuhusu madai hayo, alisema mradi huo ulitekelezwa wakati akiwa si mkurugenzi, hivyo hajui na hana taarifa zozote.

Hata hivyo, Balyomi akamwita Mratibu wa Tasaf Wilaya ya Tunduru, Muhidin Shaibu, ambaye alikiri kutolipwa baadhi ya wanakamati hao kutokana na fedha zilizoletwa katika kipindi hicho kutotosheleza.

Alisema ili kuondoa malalamiko hayo, ofisi yake inafanya utaratibu wa kupita katika maeneo ya vijiji husika na kufanya mikutano ya kuwaarifu namna taratibu za madai yao zinavyoendelea kufanyiwa kazi ikizingatiwa uwapo wa mabadiliko ya taratibu zinazotakiwa kufuatwa kabla ya kuingiziwa fedha hizo.

HABARI KIMATAIFA

# Papa Francis asisitiza wema, upendo

**ROME,** Vatican

PAPA Francis, ameikaribisha sikukuu ya Krismasi kwa kusema kwamba Mungu anapenda kila mtu, hadi wale wabaya kati yetu.

Alikuwa akizungumza na maelfu ya watu wakati wa mkesha wa sikukuu ya Krismasi katika Kanisa la Mt. Peter Basilica, mjini Vatican.

"Mnaweza kuwa na mawazo finyu, unaweza kuwa umefanya mambo mabaya, lakini Mungu anaendelea kukupenda," alisema kiongozi huyo wa Katoliki.

**Nawapenda na nitaendelea kuwapenda kwa kuwa ninyi mna thamani kubwa mbele ya macho yangu.**

Matamshi yake huenda yakachukuliwa na wengi kama yale yanayolenga kashfa zinazokumba kanisa hilo, ikiwamo visa vya unyanyasaji wa kingono.

Katika ibada hiyo Papa Francis alisema "Krismasi inatukumbusha kwamba Mungu anaendelea kutupenda sisi sote licha ya kwamba kuna waliofanya mabaya kati yetu, anasema.

"Nawapenda na nitaendelea kuwapenda kwa kuwa ninyi mna thamani kubwa mbele ya macho yangu," aliongeza kiongozi huuyo mwenye umri wa miaka 83.

Alizidi kuwaambia waumini wa kanisa hilo kwa kusema "Mungu hakupendi kwa sababu unafikiria na kufanya kile anachotaka. Anakupenda vile ulivyo. Mapenzi yake kwenu hayana masharti na hayategemei ulivyo."

Papa pia alizungumzia kuhusu kashfa za kifedha na unyanyasaji unaokumba kanisa hilo.

"Chochote tunachokosea katika maisha yetu, ambacho hakifanyiki vyema katika kanisa, matatizo yoyote yaliopo duniani hayatatumiwa kama sababu," alisema.

Miongoni mwa wale wanaoshiriki katika ibada hiyo ni watoto waliochaguliwa kutoka mataifa kama vile Venezuela, Iraq na Uganda. **BBC**



Papa Francis akibusu sanamu ya mtoto Yesu katika kusherehekea sikukuu ya Krismasi katika Kanisa la Mt. Peter Basilica, Vatican. **PICHA: AP**

## Mashambulizi yaleta maafa

**DAMASCUS,** Syria

WATU wanane wakiwamo watoto watano, wameuawa katika mashambulizi ya Urusi Kaskazini Magharibi mwa Syria.

Hata hivyo, Ufaransa na Uturuki zimehimiza kukomesha kwa vurugu hizo zilizowalazimisha maelfu ya watu kuyahama makazi yao.

Mashambulizi makali ya ndege za Syria na Urusi yamekuwa yakiulenga mkoa wa Idlib, ambao unadhibitiwa na waasi katikati ya mwezi Desemba mwaka huu.

Vikosi vya serikali vinazidi kusonga mbele ardhini, licha ya mapatano ya kusitisha mapigano ya mwezi Agosti, na miito ya Umoja wa Mataifa kupunguza makali ya mzozo huo.

Karibu raia 80 wameuawa katika mashambulizi ya ndege na roketi katika kipindi hicho, kulingana na shirika linalofuatilia haki za binadamu nchini Syria. Linakadiria kuwa zaidi ya watu 40,000 wamepoteza makazi yao katika wiki za karibuni. **DW**

## Wanawake 31 wauawa

**OUAGADOUGOU,** Burkina Faso

WATU 35, wameuawa nchini Burkina Faso, kati yao 31 wakiwa wanawake katika shambulio lililolenga kambi moja ya kijeshi na mji nchini humo.

Maofisa wa serikali wanasema kwamba, wanajeshi saba na wapiganaji 80 waliuawa, baada ya jeshi kukabiliana na shambulio hilo la siku ya Jumanne katika mkoa wa Arbinda uliopo Kaskazini mwa Soum.

Rais Roch Marc Christian Kabore, alitangaza siku mbili za maombolezo ya kitaifa katika taifa hilo la Magharibi mwa Afrika.

Hakuna kundi ambalo limekiri kutekeleza shambulio hilo kufikia sasa.

"Shambulio hilo ambalo sio la kawaida lilichukua saa kadhaa," jeshi la Burkina Faso limesema.

Wakati walipokuwa wakitoroka wapiganaji hao waliwaua raia hao na kuwajeruhi wengine sita, alisema msemaji wa serikali Remis Dandjiou,

Mapema mwezi huu takriban watu 14 waliuawa baada ya wapiganaji kufyatua risasi ndani ya kanisa mashariki mwa taifa hilo. Mashambulio ya Wanajihad yameongezeka nchini Burkina Faso tangu 2015.

Taifa hilo ambalo lilikuwa na amani, limekumbwa na ghasia za kiwango cha juu kufuatia uvamizi wa mara kwa mara mbali na kusambaa kwa wapiganaji nchini Mali.

Mamia ya watu wameuawa mwaka huu huku mamilioni kati yao wakiachwa bila makazi. **BBC**

## Putin ajitangazia ubabe silaha za kisasa

**MOSCOW,** Urusi

RAIS wa Urusi, Vladmir Putin, amesema nchi yake iko juu kwenye orodha ya mataifa yanayounda silaha mpya za kisasa.

Akizungumza kwa kujigamba, kiongozi huyo alisema nchi yake ni pekee duniani inayotumia silaha zenye kasi kubwa kuliko sauti.

Putin alikuwa na mkutano na wakuu wake wa majeshi juzi Jumanne, alijisifu kwamba kwa mara ya kwanza katika historia Urusi inaongoza dunia katika utengenezaji wa tabaka jipya la silaha na kuishinda Marekani.

Kiongozi huyo amesema wakati wa enzi za vita baridi, Muungano wa Kisovieti ulikuwa nyuma ya Marekani katika kuunda bomu la atomiki, kutengeneza ndege za kivita na makombora ya masafa marefu.

Ameongeza kuwa hivi sasa wako katika hali ya kipekee katika historia ambapo Marekani inajaribu kuifukuzia Urusi.**DW**

# Wapiganaji vita Kagera wamwangukia waziri

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

ZAIDI ya wapiganaji 20 wa vita vya Kagera walioko wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wamemwandikia barua Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Hussein Mwinyi, kuomba fedha za mapunjo.

Kwa mujibu wa barua hiyo, mapunjo hayo ni stahiki walizopaswa kulipwa wakiwa vitani ambazo mpaka sasa bado hawajalipwa.

Wapiganaji hao walipambana katika vita vya Kagera mwaka 1978 hadi 1979 na mpaka sasa baadhi yao wameshatangulia mbele za haki bila kupata stahiki zao.

Hayo yalibainishwa jana na mmoja wa wapiganaji hao, Samson Lutende, wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake.

Lutende alisema kitendo cha kutolipwa fedha hizo kimesababisha wanajeshi hao kuishi katika mazingira mgumu.

Alisema katika barua hiyo iliyoandikwa Desemba 23, mwaka huu, wakati wa vita vya Kagera wanajeshi hao wastaafu walikuwa mastari wa mbele katika mapambano na walikuwa hawalipwi fedha vitani, huku familia zao nazo zikiwa hazilipwi fedha za kujikimu.

"Fedha tunazodai sasa tulitakiwa kupatiwa wakati tumetoka vitani mwaka 1979, lakini mpaka sasa bado hatujapatiwa na wapiganaji wengine wameshapoteza maisha. Tunamwomba waziri atusaidia kupata fedha hizo ili tumudu gharama za maisha," alisema.

Aidha, Lutende alisema familia zao ziliishi kwa shida wakati huo wakiwa vitani na kuongeza kuwa mpaka sasa bado wanaishi katika maisha magumu, huku wengine wakiwa hawatambui mwisho wa maisha yao utakuwaje kwa siku zinazoendelea.

Kwa kipindi chote cha mwaka 1978 hadi 1979, alisema walikuwa wakipigania nchi, huku akidai kuwa wao ndio wapiganaji waliojitolea kuikomboa Tanzania kwa kuyapiga majeshi ya Uganda chini ya Idi Amini Dada.

"Tunamwomba waziri kutusaidia kupata haki ambayo tulitakiwa kuipata baada ya kutoka vitani. Tumefuatilia kwa mkuu wa mkoani lakini hakuna majibu kamili," alisema.

Lutende alisema walipofuatilia kwa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainabu Tellack, aliwaeleza kuwa fedha zao ziko wilayani Kahama na changamoto wanayokutana nayo ni kusafiri mara kwa mara kuzifuatilia huku wengine wakiwa hawana uwezo wa kusafiri.



Greda la kuchonga barabara likiwa linasawazisha udongo eneo la stendi kuu ya mabasi wilayani Masasi, mkoani Mtwara, jana, kutokana na mashimo yaliyokuwapo. **PICHA: HAMISI NASRI**

# Apiga debe viongozi utalii wa ndani

**Na Daniel Sabuni,** ARUSHA

MKUU wa Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara, Noelia Myoga, ametoa wito kwa viongozi wakuu wa kitaifa na familia zao kutembelea hifadhi za taifa ili kutoa mwamko kwa wananchi wa kawaida katika jitihada za kutangaza utalii wa ndani.

Kwa kufanya hivyo, amesema kutachangia maendeleo ya taifa hasa nyakati za sikukuu za mwisho wa mwaka na wanafunzo wanapokuwa likizo.

Akizungumza na Nipashe juzi, Myoga alisema viongozi wa kitaifa na taasisi zao waonyeshe mfano kwa kutembelea hifadhi za taifa na kwa kufanya hivyo watakuwa wameonyesha mfano hai kwa wananchi na pia kuongeza mapato kama watalii wa ndani.

"Viongozi ni watu wenye hadhi kubwa kwenye jamii. Wakidumisha tabia na kuendeleza utamaduni huo, wananchi wa kawaida wataiga jambo hilo jema na kufanya utalii wa ndani na hapo lazima kasi ya utalii wa ndani itaongezeka," alisema.

Myoga alitoa mfano alipokuwa mhifadhi mkuu wa Gombe mkoani Kigoma, alipofika alikuta watalii wa ndani wanaotembelea hifadhi ni 134 na ndipo akawasiliana na ofisi ya Mkuu wa Mkoa na kuonyesha mfano kwa kufanya utalii ukasababisha kuongeza idadi hadi kufikia 1,600 mwaka 2016.

"Hili linawezekana, nilipoona mambo hayaendi kule Gombe nikaenda kumuona mkuu wa mkoa wa Kigoma wakati huo Luteni Kanali mstaafu Issa Machibya.

Tulikubaliana wakajipanga viongozi kama sita wa mkoa wakaja kutalii na kulipa viingilio. Waandishi wa habari nao wakatoa ushirikiano. Baada ya miaka minane watalii wa ndani wakafikia 1,094," alisema.

"Hapa Manyara tumeanza jitihada kama hizo za kutangaza utalii wa ndani kwenye taasisi za kiserikali, binafsi, shule, kwenye mikutano ya hadhara, makongamano na pia wakati wa kukabidhi miradi ya ujirani mwema inayotekelezwa kwenye vijiji vinavyozunguka Hifadhi ya Ziwa Manyara," aliongeza.

Myoga alitaja vivutio vilivyomo hifadhini hapo kuwa ni idadi kubwa ya tembo, nyati, swala na nyani katika eneo dogo, simba wanaopanda miti, ziwa linalovutia ndege maji hasa heroe, bata maji, bata jahazi, korongo na wengineo.

Pia mhifadhi huyo mkuu alitaja vingine kuwa ni aina nyingi za ndege, takribani 390, ukuta wa bonde la ufa, chemchem za maji ya moto zinazobubujika kutoka ardhini kati ya nyuzi 65 hadi 70, msitu wa maji ya ardhini na makundi ya viboko.

Akitoa takwimu za watalii wa ndani waliotembelea hifadhi hiyo, alisema mwaka 2012 hadi 2013 walitembelea watalii 139, 2013/14 watalii 1,132, 2014/15, watalii 1,356, 2015/16 watalii 1,508 na 2016/17 watalii 1,690.

Myoga alisema asilimia tano tu ya Watanzania ambao kwa makadirio ni milioni tano wangetembelea vivutio kwenye utalii wa ndani kwa kiingilio cha 11,800 pamoja na kodi, taifa lingeingiza zaidi ya Sh. milioni 59.

# Wasaidiwa kuepuka jembe la mkono

**Na Sabato Kasika**

VIKUNDI 20 vinavyojishughulisha na kilimo katika Jimbo la Musoma Vijijini mkoani Mara, vimepewa msaada wa majembe ya kukokotwa na ng'ombe ili kupunguza matumizi ya jembe la mkono.

Baadhi ya vikundi hivyo ni Mlandizi, Moli, Unique, Ukombozi, Umoja ni Nguvu, ambavyo vilikabidhiwa majembe hayo na mbunge wa jimbo hilo, Profesa Sospeter Muhongo.

Prof. Muhongo sasa yuko jimboni akihamasisha shughuli za maendeleo ikiwamo uchangiaji wa ujenzi wa madarasa kwa shule za sekondari.

"Plau hizo 20 zimegawiwa kwenye vituo viwili vya Chumwi na Nyasurura huku wahusika wakija kufuata na hiyo ni ishara ya kuanza rasmi kampeni ya kupunguza matumizi ya jembe la mkono jimboni mwetu," alisema.

Akizungumza na gazeti hili jana kwa njia ya simu, alisema katika kituo cha Chumwi kulikuwa na vikundi kutoka vijiji vya Bukima, Butata, Chimati, Chitare, Chumwi, Mabui Merafuru, Masinono, Mikuyu, Kaburabura, Rusoli, Suguti na Wanyere.

"Katika kituo cha pili ambacho ni cha Nyasurura, kuliwa na vikundi kutoka Vijiji vya Kamguruki, Kwibara, Maneke, Mwiringo, Nyakatende, Nyasaungu, Nyegina na Tegeruka," alisema Prof. Muhongo.

Alisema madiwani na viongozi wengine wa kata zenye vijiji vilivyopewa plau hizo aliziita kuwa ni zawadi ya Krismasi, walikuwapo kushuhudia makabidhiano hayo.

"Binafsi niliambatana na rafiki zangu wa miaka mingi toka Ujerumani, Christa Werner na Wolfgang Zils nilisoma nao Ujerumani Magharibi miaka ya 1980, walinitembelea jimboni," alisema.

Aidha, mbunge huyo alisema jana alitarajia kuendesha harambee ya kuchangia ujenzi wa shule wa sekondari mpya ya kijiji cha Nyasaungu kilichopo Kata ya Ifulifu.

Alisema wakazi wa kijiji hicho wameamua kujenga sekondari yao na wamemwalika kwa mara ya pili kuendesha harambee, ili kukamilisha ujenzi haraka na ikiwezekana ianze kuchukua wanafunzi Februari, mwaka ujao.

# Biteko akemea unyanyasaji wajasiriamali kwenye madini

**Na Asraji Mvungi,** ARUSHA

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, amesema serikali inataka kuona watendaji wa vyombo vya dola na wasimamizi wa sekta ya madini wanaacha kuwasumbua wananchi wanaofanya ujasiriamali katika maeneo yalikofunguliwa masoko ya madini.

Ameagiza kukomeshwa kwa usumbufu huo na badala yake wawajengee mazingira mazuri ya kunufaika na fursa hizo.

Biteko aliyasema juzi hayo alipokwenda kusikiliza malalamiko ya wananchi mkoani Arusha, huku akisema waathirika wakubwa ni wanawake ambao wamekuwa wakisumbuliwa na kukatazwa kufanya shughuli zao kwenye masoko ya madini.

Waziri alisema hatua ya baadhi ya wananchi, wakiwamo wanawake kukimbilia kwenye masoko ya madini kwa ajili ya kujitafutia kipato inapaswa kuwa ya kujivunia.

Aidha, akizungumza na wadau wa sekta hiyo wakiwamo viongozi wa vyombo vya dola na wa mkoa, wilaya na halmashauri, Biteko aliwataka kujielekeza zaidi katika kuwasaidia wananchi badala ya kuwasumbua tatizo ambalo liko zaidi kwa wajasiriamali hao wadogo.

Biteko alisema lengo la serikali ni kuona kila Mtanzania ananufaika na fursa zinazopatikana kwenye sekta zote za uzalishaji ikiwamo ya madini.

Kuhusu changamoto zinazolikabili soko la madini la mkoa wa Arusha, Mkuu wa Mkoa huo, Mrisho Gambo, alisema kuna tatizo kubwa la kukosekana kwa uhusiano mzuri kati ya wachimbaji wakubwa na wadogo ambao kwa kiasi kikubwa badala ya kushirikiana, wamekuwa wakichongeana suala ambalo linadhoofisha kufikiwa kwa malengo.

Baadhi ya wachimbaji na wafanyabiashara wa madini wamesema pamoja na nia nzuri ya serikali ya kuwasaidia bado kuna changamoto nyingi hasa kutoka kwa watendaji wa ngazi za kati na za chini na pia taasisi na idara za kodi.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara wa Madini Tanzania (Tamida), Sammy Mollel, alisema pamoja na wauza madini kuhakikisha wanalipa kodi zote zilizowekwa na serikali, bado kuna usumbufu na baadhi ya kodi zimeibuka na kumwomba waziri kufuatilia na kuwasaidia kwa kuwa zinaendelea kuwaumiza badala ya kuwasaidia.

Mollel alizitaja baadhi ya kodi hizo kuwa ni tozo za ukaguzi na ambazo kimsingi zinakuwa zimeshalipwa kupitia tozo zingine.

Changamoto nyingine aliyoitaja ni pamoja na kuwekewa vikwazo vya kuelekea kwenye utekelezaji wa agizo la serikali la kuhakikisha madini yote yanachakatwa nchini ambapo licha ya kuwapata wahisani wa kuwasaidia wamekuwa wakiwekewa masharti magumu ya kuingia nchini.




Mfanyabiashara ndogo akiwa anatembeza kofia za Father Krismasi eneo la Fire jijini Dar es Salaam, jana. **NA MPIGA PICHA WETU**

## Waazimia kupeleka kero kwa JPM

**Na Dege Masoli,** KILINDI

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Kilindi, kimetakiwa kuwasilisha kero tano sugu kwa Mwenyekiti wa Taifa, Rais John Magufuli zinazotokana na maazimio ya wananchi ya mkutano uliofanyika jana makao makuu ya wilaya hiyo, mjini Songe.

Wakitoa malalamiko yao kwa Mwenyekiti wa CCM Wilaya, Bakari Kingalangala, anayefanya ziara ya kukagua utekelezwaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM kwenye kata zote 21 za wilaya hiyo, wananchi walisema walidai Songe kusahaulika katika huduma muhimu za kijamii na kutoa azimio kwa chama hicho kupeleka kilio hicho kwa Rais.

Kwa mujibu wa wananchi hao, kero sugu walizotaka ziwasilishwe kuwa ni ubovu wa miundombinu ya barabara inayounganisha wilaya hiyo na za jirani, umeme, maji, uhaba wa watumishi na kukosekana kwa mtaalamu wa mashine ya vipimo katika Kituo cha Afya cha Songe.

Walisema kukosa barabara ya uhakika na umeme kunawafanya washindwe kujiendeleza kiuchumi, ongezeko la bei ya bidhaa zinazoingia wilayani humo na kukosekana kwa soko la bidhaa walizo nazo.

Pia walisema maji na uhaba wa watumishi vinahatarisha maisha yao kwa kulazimika kutumia maji yasiyo salama na tiba sahihi na kwa wakati.

Suala lingine lililoibuka kwenye mkutano huo ni hatua ya halmashauri kuchukua vyanzo vya mapato ambavyo vilikuwa vikiwezesha serikali za vijiji kujiendesha na kwamba havipati hata gawio jambo linalowafanya wenyeviti wa serikali hizo kuongoza kwenye mazingira magumu.

Wananchi hao walieleza lengo la kukitaka chama hicho kufikisha kilio chao ni kuamini kwamba mwenye mamlaka ya kuwaondolea ni Rais Magufuli.

Aidha, wananchi hao walitaka kutembelewa na kiongozi huyo wa kitaifa kwa kuwa tangu kampeni zianze hajawahi kufika wilayani humo na kwamba wanahitaji kumwona kupata maelekezo yake kama anavyofanya kwa wapigakura na wananchi wa maeneo mengine.

# Jiji lajikwamua ukosefu wa madawati

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

HALMASHAURI ya Jiji la Arusha imekabidhi madawati 1,000 kwa ofisa elimu wa sekondari wa jiji kwa ajili ya maandalizi ya wanafunzi wanaotarajiwa kujiunga na kidato cha kwanza mwakani.

Pia halmashauri hiyo inaendelea kutengeneza madawati mengine 2,500 ambayo hadi ifikapo Januari 3, mwakani, yanatarajiwa kukamilika na kusambazwa katika shule zote za sekondari zenye uhitaji wa madawati hayo.

Akizungumza wakati wa kukabidhi madawati hayo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, Dk. Maulid Madeni, alisema kulikuwa na upungufu wa madawati ndipo wakaamua kutengeneza wenyewe katika karakana yao iliyoko katika Shule ya Msingi Kaloleni.

Dk. Madeni alisema katika mchakato huo, walipanga kutengeneza madawati 3,900 kwa ajili ya shule zote za sekondari za jiji.

"Ndani ya halmashauri yetu hatutaki kuona wanafunzi wanakaa chini hawana madawati ndiyo maana tumeamua kutengeneza wenyewe madawati haya ili wanafunzi ambao wanakuja mwakani wakae vizuri na kusoma vyema.

"Kama mnavyoona madawati yetu ni imara kabisa na yametengenezwa kwa kiwango cha juu ambacho sisi wenyewe ndio tumemwelekeza fundi anayetengeneza jinsi tunavyotaka," alisema.

Alibainisha kuwa ili mwanafunzi afaulu vyema ni lazima mazingira ambayo anatumia kusomea na kufundishiwa yawe mazuri ndiyo maana wamewaandalia wanafunzi wanaoanza kidato cha kwanza mazingira mazuri ya kusomea na kuongeza kiwango cha ufaulu.

Mkurugenzi huyo alibainisha kuwa madawati yote na viti 3,900 ambayo yanatengenezwa yanagharimu Sh. milioni 100 na uamuzi huo umewasaidia sana kwa kuwa wameokoa Sh. milioni 200 iwapo wasingetengenezea katika karakana ya jiji na kumtafuta mkandarasi.

Ofisa Elimu Sekondari wa Jiji la Arusha, Valentine Makuka, akipokea madawati hayo, alimshukuru Mkurugenzi wa Jiji kwa kuwatengenezea madawati kwa kuwa yatawaondolea adha wanafunzi ambao walikuwa wanakaa chini na wale ambao walikuwa wanabanana kwenye madawati.

Alisema madawati hayo yatakidhi mahitaji ambayo yalikuwa yamepungua kwa mapokezi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza ambao wanatarajia kuwapokea Januari 6, mwakani.

Makuka alisema kwa mwaka huu wamepokea wanafunzi wa kidato cha kwanza 10,888 ambao kutokana na ujenzi wa vyumba 26, watatosha na hakuna mwanafunzi atakayebaki kwa sababu ya ukosefu wa madarasa.

# OLE ATAKIWA KUWASAJILI SANCHO, NIGUEZ




**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, ameambiwa afanye afanyavyo lakini ahakikishe anawasajili mastaa wawili, Jadon Sancho na Saul Niguez.

United inahusishwa na wachezaji wote hao wawili sambamba na mshambuliaji Erling Braut Haaland wakati Kocha Solskjaer akihitaji viungo wawili wabunifu pamoja na mshambuliaji wa kati mmoja.

Kiungo wa zamani wa United, Mbrazil Kleberson alisema kiungo wa pembeni wa Borussia Dortmund, Sancho na kiungo wa kati wa Atletico Madrid, Niguez watakuwa wachezaji muhimu sana kuongezwa kwenye kikosi hicho cha Old Trafford.

Sancho anatarajia kuigharimu United pauni milioni 100, lakini Kleberson alisema huo ni uwekezaji wenye maana kubwa.

Kocha Solskjaer amekuwa na mipango ya kuboresha kikosi chake ili kuwa cha kibabe zaidi akipanga kusajili nyota wapya Januari na kwenye dirisha lile kubwa la mwisho wa msimu.

# Yaya Toure awashangaa wanaobagua watu

**LONDON,** England

MCHEZAJI wa zamani wa Manchester City na Barcelona, Yaya Toure, anaamini kuwa ubaguzi kwenye soka umefikia hatua mbaya kwa sababu mashabiki wa sasa ni wajinga zaidi ya wale wa zamani.

Kwa miezi ya hivi karibuni, vitendo vya ubaguzi katika mpira barani Ulaya vimeongezeka kwa kasi.

Mario Balotelli na Romelu Lukaku, ni miongoni mwa wachezaji waliokumbana na ubaguzi kwenye Ligi Kuu Italia msimu huu, pamoja na hayo, yapo matukio mengi ya ubaguzi yaliyoripitiwa kwa miezi ya hivi karibuni Ulaya.

Toure amezungumza na Fifa juu ya namna ya kukomesha ubaguzi lakini akasisitiza hauwezi kuondoka haraka.

Nyota huyo wa zamani wa Ivory Coast ambaye sasa anaichezea Qingdao Huanghai ya China, alisema: "Najua itakuwa ngumu na vita hii itachukua muda mrefu.

"Mashabiki, watu, sasa wamekuwa wajinga zaidi ya zamani. Inashtua kwa sababu tupo mwaka 2019, 2020, 2025 tuna watoto wanakuja, tutafanya nini?





# AC Milan wamtaka Ibrahimovic haraka

**MILAN,** Italia

KOCHA wa AC Milan, Stefano Pioli, ameushangaa uongozi wa klabu hiyo kwa kuchelewesha usajili wa Zlatan Ibrahimovic (38), kwa sababu anaamini staa huyo wa zamani wa Manchester United anaweza kuiokoa miamba hiyo ya San Siro.

Akizungumza baada ya timu yake kukubali kichapo cha mabao 5-0 kutoka kwa Atalanta ambacho ni kikubwa zaidi katika kipindi cha miaka 21 iliyopita, Pioli alisema uongozi wa klabu hiyo ndio unatakiwa kuulizwa kwa nini haujamalizana na Ibrahimovic ambaye ni mchezaji huru kwa sasa.

Pioli aliongeza kuwa usajili wa straika huyo wa zamani wa Barcelona, utaongeza ari, kujitambua na morali kwenye timu kuanzia kwenye viwanja vya mazoezi na muhimu zaidi katika mechi na kurudisha ubabe wa Milan, Italia.

Mbali na AC Milan klabu nyingine ya Ligi Kuu England ya Everton inatajwa kumtaka staa huyo aliyemaliza mkataba wake wa kuichezea LA Galaxy. Kocha mpya wa Everton Carlo Antelotti amemfungulia milango ya kujiunga na klabu hiyo straika huyo kama atapendezwa na mpango huo.

HABARI MICHEZO

# Guardiola alalamikia ratiba ngumu EPL

**MANCHESTER ,** England

PEP Guardiola amechukua uamuzi wa kuwaandikia barua wasimamizi wa Ligi Kuu England na kuwaambia 'asante' baada ya ratiba ngumu iliyopangiwa timu yake ya Manchester City katika kipindi hiki cha Krismasi, huku wapinzani wake Liverpool akihisi wanapendelewa.

Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu England wamepewa mapumziko ya mechi kwenye "Boxing Day", lakini baada ya hapo watacheza mechi mbili kwa muda usiozidi saa 48.

Watakuwa na mechi ya jioni dhidi ya Wolves ugenini, Desemba 27, itafuatiwa na mechi ya nyumbani dhidi ya Sheffield United muda wa jioni Jumapili.

Ukiwalinganisha wapinzani hao kwenye mbio za ubingwa, Liverpool wao wana siku moja zaidi ya mapumziko baina ya mechi zake mbili dhidi ya Leicester City na Wolves.

City wanaaminika kwamba wamefanya mawasiliano na Ligi Kuu England kuzungumzia kutokuwa na furaha juu ya ratiba yao.

Guardiola alishasema wakati ratiba inatangazwa kwamba atahitaji kuwaweka kwenye jokofu wachezaji wake kwa siku mbili kutokana na mechi zinazowakabili wiki hii.

Guardiola alisema: "Nimewaandikia barua Ligi Kuu England kuwaambia asanteni.

"Tutakaa kwenye jokofu baada ya mechi dhidi ya Wolves ili kujiandaa kwa mechi dhidi ya Sheffield United."

Kitu pekee ambacho amefanyiwa Guardiola na wachezaji wake ni kwamba wao hawatakuwa na mechi kwenye siku zote za sikukuu, kwa maana ya Krismasi na Boxing Day.

Aliongeza: "Jumapili ni siku ya mapumziko, tutafanya mazoezi Jumatatu na Jumanne asubuhi. Usiku wa Jumanne ni mapumziko, Jumatano asubuhi ni mapumziko, Alhamisi mazoezini na Ijumaa ni mechi dhidi ya Wolves inayofundishwa na Kocha, Nuno Espirito Santo."

Kiungo wa timu hiyo, Kevin De Bruyne, amelalamika pia akisema wamewekewa ratiba ya mechi mbili zilizokaribiana sana jambo linalomweka kwenye wakati mgumu na wachezaji wenzake.

Staa huyo kutoka Ubelgiji mwenye umri wa miaka 28, alisema: "Mechi ya kwanza itakuwa kati ya siku tano au sita, hiyo sawa haina shida, ila sasa mechi inayofuatia, sijui tutafanyaje. Subiri tuone hali ya mambo itakavyokuwa kwa kila mtu baada ya saa 48.





# NYOTA UNITED KUTUA BARCA

**MANCHESTER,** England

HUENDA Manchester United wakaingia kwenye hatari ya kumpoteza nyota wao kinda, Angel Gomes, ambaye ana mpango wa kujiunga na kikosi cha Barcelona.

Gomez mwenye umri wa miaka 19 amesema kuwa ana mpango wa kuondoka ndani ya Old Trafford kwa ajili ya kwenda kutimiza malengo yake aliyojiwekea baada ya kushindwa kufikia makubaliano na mabosi wa United.

Kinda huyo anakipiga pia kwenye Timu ya Taifa ya vijana wa umri chini ya miaka 20 ya England (U-20), alianza kulelewa ndani ya United akiwa na miaka sita amecheza jumla ya mechi saba za wakubwa na alianza tatu pekee za kwenye Ligi ya Europa.

Habari zinaeleza kuwa mbali na Barcelona ambako anacheza mchezaji bora wa dunia, Lionel Messi, pia Juventus na Crystal Palace zimeonyesha nia ya kuwania saini ya kinda huyo.

# *Arteta aonyesha ubavu wake Arsenal*

**LONDON,** England

KOCHA wa mpya wa Arsenal, Mikel Arteta, amesema kuwa atatumia nguvu kubwa kuwashawishi wachezaji wake watumie uwezo wote walionao kupata matokeo.

Arteta ambaye aliwahi kucheza ndani ya Arsenal na alikuwa nahodha amesema kuwa anaamini wachezaji wanaweza kufanya mambo makubwa kwa ajili ya mashabiki na timu hiyo kwa ujumla.

"Nitawashawishi wachezaji kucheza kwa nguvu na kutumia uwezo wao wote walionao kupata matokeo chanya, hatua kwa hatua ninaamini kwamba tutafikia malengo yetu na mafanikio tutayaona, yatakayotutambulisha sisi katika wakati ambao tunauhitaji," alisema Arteta.

Kabla ya kutua Arsenal, Arteta alikuwa ndani ya kikosi cha mabingwa watetezi Manchester City akifanya kazi na Kocha Mkuu, Pep Guardiola.

Arteta amechukua mikoba ya Unai Emery ambaye alipigwa chini hivi karibuni baada ya kudumu kwa muda wa miezi 18, amepewa kandarasi ya miaka mitatu na nusu kukinoa kikosi hicho.

Pia kocha huyo ambaye aliwahi kucheza ndani ya Arsenal na alikuwa nahodha amesema kuwa anaamini wachezaji wanaweza kurejesha heshima ya timu hiyo kwa kuonyesha ushindani.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BARCELONA YAJIANDAA KUMRUDISHA NEYMAR

## Ni nyota ambao Arteta anatarajiwa kuwasajili mapema katika...

**BARCELONA,** Hispania

KWA mara nyingine, Barcelona itajipanga kufanya mchakato wa kumrejesha mshambuliaji Mbrazil, Neymar, katika kikosi chake kwenye majira ya joto mwakani, chanzo chetu kimeiambia ESPN.

**Mabosi wa Barcelona wanaamini kuwa Neymar ndiye mrithi halisi wa nahodha wao na mshambuliaji nyota, Lionel Messi.**

Klabu hiyo inaamini kuwa ni rahisi kumrejesha Neymar kwenye Uwanja wa Camp Nou kwa mara nyingine, na atakuwa msaada kwa timu hiyo pale Messi atakapoondoka, ikifahamika kwamba tayari mshambuliaji huyo alishawahi kucheza klabuni hapo na ni mmoja wa wachezaji waliocheza katika kiwango kizuri.

Nyota huyo anayeichezea pia Timu ya Taifa ya Brazil, ameendelea kuwa na uhusiano mzuri na Barca licha ya kuondoka na kujiunga na Paris Saint-Germain kwa dau lililoweka rekodi duniani la Euro milioni 22.

Ukurasa wa kwanza wa gazeti la Mundo Deportivo la Jumanne liliandika kuwa Barca itajipanga kumsajili mshambuliaji huyo licha ya kiwango chake kutokuwa cha kuridhisha katika kipindi cha pili cha msimu huu, huku PSG ikiendelea kupambana kuwania taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Neymar amekuwa na wakati mgumu kwa mabingwa hao wa Ufaransa, ambao walikataa kumwachia mshambuliaji huyo kujiunga na Barca katika kipindi cha majira ya joto mwaka jana licha ya kufanyika kwa jitihada kubwa za kukamilisha mchakato huo.

Wamiliki wa PSG wameendelea kuweka vikwazo kwa Barca, ambao wanajiandaa kwenda katika Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), ili kuamua ada ya uhamisho ya mchezaji huyo, ambaye ameshakaa kwenye klabu kwa muda wa miaka mitatu bila ya kuwapo kwa kipengele kinachomruhusu kuondoka.

Barcelona imekuwa ikijieleza vema kuhusiana na mvurugano uliotokea katika mchakato huo wa kumrejesha Neymar kwenye ardhi ya Catalan, na sasa ikijipanga kurudia tena zoezi hilo hapo mwakani.

Inaelezwa kuwa ili Neymar aweze kuuzwa, thamani yake ni Euro milioni 180, kiasi ambacho ni pungufu ya Euro milioni 42, ambacho Barça ilimuuza kwa PSG, usajili ambao ulionekana umeleta "kizaazaa".

Tayari Neymar ameshindwa kuitumikia klabu yake kwa muda katika msimu huu unaoendelea kufuatia kupata majeruhi ya maumivu ya nyama za paja Oktoba mwaka jana alipokuwa kwenye majukumu ya kikosi cha Timu ya Taifa ya Brazil, lakini nyota huyo mwenye umri wa miaka 27, amekuwa akifunga isipokuwa mechi mbili za Ligue 1.

## ZISIKUPITE

### WERNER ATAKIWA CHELSEA

CHELSEA inajiandaa kufanya mchakato wa kumsajili straika wa RB Leipzig na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Timo Werner (23), katika kipindi cha dirisha dogo la Januari. ***(Express)***

### POGBA AITAMANI JUVE

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Paul Pogba (26), amesema kuwa anataka kuondoka Manchester United na kurejea katika klabu yake ya zamani ya Juventus. ***(Calicomercato - in Italian)***

### NEYMAR KURUDI BARCA

VIGOGO wa Hispania, Barcelona wamesisitiza kuwa watafanya mchakato wa kumrejesha klabuni kwao mshambuliaji wa Paris St-Germain na Timu ya Taifa ya Brazil, Neymar (27), katika dirisha la majira ya joto. ***(Goal)***

### MANDZUKIC RASMI QATAR

STRAIKA Mario Mandzukic amemaliza utata kuhusu hatima yake baada ya kukamilisha uhamisho wa kujiunga na klabu ya Al-Duhail ya Qatar. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 33, raia wa Croatia, alikuwa anawindwa na Manchester United. ***(Mail)***

### HAALAND KUIKAMUA UNITED

MANCHESTER United imeweka wazi kuwa iko tayari kumlipa mshahara wa pauni 200,000 kwa wiki straika wa Timu ya Taifa ya Norway, Erling Haaland (19), endapo atakubali kutua England, kwa sasa nyota huyo anaichezea klabu ya Red Bull Salzburg. ***(Sun)***

### ALONSO ANUKIA MILAN

BEKI wa Timu ya Taifa ya Hispania na Chelsea, Marcos Alonso, ambaye ana umri wa miaka 28, ametajwa kuwindwa na Inter Milan. ***(Calciomercato)***

### DEMBELE ANUKIA ARSENAL

ARSENAL inatarajia kuuza mmoja wa washambuliaji wake ili kurahisisha mchakato wa kumsajili straika wa Lyon na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Moussa Dembele, ambaye ana umri wa miaka 23. ***(Le10Sport - in French)***

### EVERTON, ATLETICO VITANI

EVERTON na Atletico Madrid zinachuana kuwania saini ya mshambuliaji wa River Plate na Timu ya Taifa ya Colombia, Rafael Santos Borre, ambaye ana umri wa miaka 24. ***(AS)***

### SMALLING ANOGEWA ROMA

BEKI wa Manchester United, Chris Smalling (30), amesema kuwa anataka kuendelea kubakia katika klabu ya Roma, baada ya mkataba wake wa mkopo utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Roma Press)***

### ZLATAN AKARIBIA MILAN

MABOSI wa AC Milan wanaamini watafanikisha mchakato wa kumrejesha mshambuliaji raia wa Sweden, Zlatan Ibrahimovic (38), katika klabu hiyo katika usajili wa dirisha dogo la Januari. ***(Mail)***

### NUNEZ AKARIBIA ENGLAND

WEST Ham wanajiandaa kufanya mchakato wa kumsajili beki wa kati Mhispania, Unai Nunez, mwenye umri wa miaka 22, kutokea Athletic Bilbao. ***(AS in Spanish)***

# Chato Musica yaja na Hapa Kazi Tu

**Na Sabato Kasika**

BENDI mpya ya muziki wa dansi ya Chato Musica, imekamilisha kibao chake cha kwanza kiitwacho "Hapa Kazi Tu" ikiwa ni kutambua na kuunga mkono juhudi za kazi anazozifanya Rais Dk. John Magufuli, imeelezwa.

Kiongozi wa bendi hiyo, Kata Singa, alisema Chato Musica, ilianzishwa miezi miwili iliyopita na kuwa inaendelea kuandaa nyimbo kwa ajili ya kuzindua albamu yao ya kwanza.

Singa alisema hayo jana, alipofika katika ofisi za gazeti hili, Mikocheni jijini Dar es Salaam, wakati akizungumzia ujio wa wimbo huo, ambao unatarajia kubeba jina la albamu ya kwanza.

"Tumeanza na huo wimbo, kwa ajili ya kutambua kazi kubwa anayofanya Rais wetu (Magufuli), kwa ajili ya Watanzania, na lengo letu ni kuhakikisha bendi inaanza kazi rasmi mwaka ujao," alisema Singa.

Aliongeza kuwa, bendi hiyo inaundwa na wanamuziki wachache ambao hawana majina makubwa, lakini wenye uwezo wa kazi na ana uhakika italeta upinzani kwenye soko la muziki wa dansi.

"Kwa sasa bendi ina wanamuziki nane, ambao baadhi yake ni Frida Cyprian, Lily Simile, Chris Kalonji, Ngosha Simon, Easy International, ambao wote wanafanya kazi vizuri, pamoja na mimi," Singa alisema.

Naye mkurugenzi wa bendi hiyo, Abdallah Musira, alisema wamejipanga vizuri na wako tayari kukabiliana na changamoto kwenye muziki wa dansi, ambazo zimesababisha muziki huo kupoteza umaarufu.

"Sisi tunajua kwamba muziki wa dansi unakabiliwa na changamoto nyingi, lakini tumejipanga kuhakikisha tunazishinda na kuwa miongoni mwa bendi yenye jina kubwa hapa nchini," alisema Musira.

Aliongeza kuwa wanamuziki wake hawajakurupuka tu kuanzisha bendi hiyo, bali walijipanga na kufikia uamuzi huo wakiwa tayari wana mbinu za kuhakikisha wanasimama imara na kufanya kazi bila kuyumba.

"Hivyo wadau wa muziki wa dansi wasubiri mambo makubwa kutoka Chato Musica tutakapoanza kazi rasmi mwaka ujao ambao si siku nyingi tutaanza, cha msingi ni kumuomba Mungu aendelee kutupa uhai," alisema.

# YANGA YAWAONYESHA MBEYA CITY MAPENGO

**Na Isaac Kijoti,** MBEYA

BAADA ya kuanza kwa sare katika mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu Tanzania Bara akiiongoza Mbeya City, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Amri Saidi, amesema anahitaji kukiimarisha kikosi hicho kwa kukiongezea wachezaji wazoefu.

Juzi katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini hapa, Mbeya City ililazimishwa sare tasa na Yanga, huo ukiwa ni mchezo wa kwanza kwa Amri Saidi tangu aliporithi mikoba ya Juma Mwambusi aliyeachia ngazi mapema mwezi huu.

Hata hivyo, pamoja na matokeo hayo ambayo ni mwanzo mzuri wa kocha huyo, bado anaamini timu hiyo inahitaji wachezaji wazoefu kama watano au sita.

**Akizungumza na Nipashe jijini hapa baada ya mechi hiyo ambayo safu yake ya ulinzi ilionekana kucheza vizuri, Saidi alisema katika dirisha hili dogo la usajili atahitaji kuisuka zaidi timu yake.**

"Ni kweli safu ya ulinzi imecheza vizuri leo, lakini nataka kuiimarisha zaidi, eneo ambalo linahitaji kutazamwa zaidi ni safu ya ushambuliaji na kiungo.

"Kwa ujumla wachezaji wangu wamejitahidi hasa ukizingatia Yanga ni timu kubwa na ina wazoefu, ukilinganisha na sisi ambao tuna vijana wengi," alisema kocha huyo wa zamani wa Biashara United ya Mara.

Kuhusu kuambulia pointi moja nyumbani, alisema si matokeo mabaya sana kwao hasa ukizingatia hali ya uwanja haikuwa rafiki kwao kutokana na mvua iliyokuwa inanyesha.

"Tulitengeneza nafasi nyingi ila hatukuweza kuzitumia, huwezi kuwalaumu sana wachezaji hasa kutokana na hali ya uwanja iliyochangiwa na mvua," alisema.

Kwa matokeo hayo Mbeya City imefikisha pointi tisa ikiwa nafasi ya 19 baada ya mechi 13 wakati Yanga iliyoshuka dimbani mara tisa imefikisha alama 18.



Kiongozi wa bendi ya muziki wa dansi ya Chato Musica, Kata Singa (kulia), akielezea maandalizi ya albamu ya kwanza ya bendi hiyo ambayo inatarajiwa kuanza kazi rasmi mapema mwakani. Kushoto ni Mkurugenzi wa bendi hiyo, Abdallah Musira. **PICHA: SABATO KASIKA**

# *Coastal Union, Azam hapatoshi*

**Na Shufaa Lyimo**

MABINGWA wa mashindano ya Kombe la FA, Azam FC wanatarajia kuwakabili wenyeji Coastal Union, katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini, Tanga.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Idd Cheche, alisema kuwa maandalizi kwa ajili ya mchezo huo yamekamilika na kila mchezaji yupo tayari kwa ajili ya kupambana kuwania pointi tatu.

"Maandalizi kwa ajili ya mchezo wetu wa kesho (leo), yamekamilika, kila mchezaji ana morali ya ushindi," alisema Cheche.

Kocha huyo aliongeza kuwa kikosi chake kilitua mapema jijini Tanga ili kuwapa nafasi wachezaji wake kuizoea hali ya hewa pamoja na kusoma mazingira ya mchezo wao.

"Wachezaji wangu wapo vizuri kuelekea mchezo wetu dhidi ya Coastal Union, tunawaomba mashabiki wetu wajitokeze kwa wingi, hatutawaangusha,"alisema Cheche.

Aliwataka mashabiki wao kuendelea kuwapa ushirikiano ili wazidi kufanya vizuri na kupata pointi tatu ugenini.

Naye Kocha Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda, aliliambia gazeti hili kuwa mechi hiyo itakuwa ngumu kwa sababu wachezaji wake wameahidi kutopoteza mchezo wa pili mfululizo ndani ya wiki moja.

Mgunda alisema kuwa wanahitaji kulinda heshima ya klabu yao kwa kutopoteza pointi katika mechi hiyo ya ligi na kurejesha furaha baada ya kutolewa kwenye mashindano ya Kombe la FA na "watani" zao, African Sports.

"Itakuwa mechi ngumu, tumejiandaa kwa hilo, ila wachezaji wangu watatakiwa kusahau yaliyotokea katika mchezo uliopita, yale ni mashindano ya FA na sasa tunaingia kwenye Ligi Kuu, naamini tutapata ushindi," Mgunda alisema.

Ligi hiyo itakayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika mwakani, itaendelea tena kesho kwa Tanzania Prisons kuwakaribisha Yanga kwenye Uwanja wa CCM Sokoine jijini Mbeya huku keshokutwa KMC FC ikiwavaa na mabingwa watetezi, Simba kwenye Uwanja wa Uhuru.

# Michezo

Alhamisi Desemba 26, 2019

Nipashe



Barca yajiandaa kumrudisha Neymar

HABARI UK.30



Kiungo wa Simba Mzambia Clatous Chama, akijaribu kuwatoka mabeki wa Lipuli, katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini, Dar es Salaam jana. Simba ilishinda mabao 4-0. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# *Simba yanogesha Krismasi*

## ●●● Ni baada ya kuipa kichapo Lipuli FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara...

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi Simba, wamewapa furaha ya Sikukuu ya Krismasi mashabiki wao baada ya kuipa kichapo cha mabao 4-0, Lipuli FC ya Iringa katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa jana kwenye Uwanja wa Uhuru jijini, Dar es Salaam.

**Ni ushindi unaowafanya vinara hao wa Ligi Kuu Bara wafikishe pointi 28, ikiwa imecheza mechi 11, wakati Lipuli yenye pointi 20 ikibakia katika nafasi ya nne kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 20.**

Matokeo hayo yaimfanya safu ya ushambuliaji ya Kocha, Sven Vandenbroeck, kufunga mabao 10 katika mechi mbili ilizocheza ndani ya siku nne.

Kiungo Mkenya aliyesajiliwa msimu huu akitokea Gor Mahia, Francis Kahata, ndiye aliyewainua mashabiki wa Simba dakika ya 10 kwa kufunga bao la kwanza baada ya kupachika mpira ndani ya wavu, akiunganisha krosi maridadi kutoka kwa beki mzoefu, Shomari Kapombe.

Bao hilo lilidumu hadi timu hizo zilipokwenda mapumziko, licha ya wenyeji Simba kupoteza nafasi mbalimbali za kufunga kupitia Hassan Dilunga na Meddie Kagere, ambaye alikuwa anakabwa na mabeki wawili hadi watatu kwa wakati mmoja.

Kipindi cha pili Simba iliingia kwa nguvu na dakika ya 49 ilifanikiwa kufunga bao la pili kupitia kwa Kagere, ambaye alimalizia pasi kutoka kwa Clatous Chama na kuwa bao lake la tisa msimu huu huku Dilunga, akipachika goli la tatu dakika ya 56 kwa penalti iliyotokana na David Mwasa kunawa mpira kwenye eneo la hatari wakati akipambana kumzuia Chama asifunge.

Penalti hiyo ilionekana kumrudisha mchezoni Dilunga ambaye dakika ya 64 alifunga bao la nne, baada ya kupenyezewa pasi ndefu na Msudan Sharaf Shiboub.

Kabla ya kufunga magoli hayo Dilunga alikosa magoli mawili ya wazi ambayo yangeweza kuipeleka Simba mapumziko ikiwa na ushindi mzuri.

Lipuli ndio ilikuwa ya kwanza kufanya mashambulizi katika mchezo huo, ambapo dakika ya nane tu, kupitia Kenneth Masumbuko, ilifanya shambulizi la hatari kwenye lango la Simba, lakini shuti hilo lilipanguliwa na kipa, Benno Kakolanya na kuwa kona tasa.

Dakika moja baadaye, Kagere alikosa bao, baada ya "kumegewa" pasi safi kutoka kwa Chama, lakini kabla hajapiga, mabeki wa Lipuli waliuondoa mpira uliokuwa mguuni kwa Mnyarwanda huyo huku dakika ya 20 akiwa na kipa, Aghaton Antony, alitumia muda mrefu kufikiria namna ya kupiga mpira, hadi ulipookolewa ukiwa tena miguuni mwake.

Kwa kupoteza mechi hiyo, Lipuli inashuka hadi nafasi ya tisa katika msimamo wa Ligi Kuu Bara na kuipisha Yanga kwenye nafasi ya nane, kufuatia timu hizo mbili kujikusanyia pointi 18, lakini wenzao wana wastani mzuri wa magoli ya kufunga na kufungwa.

# Yanga yapania tatu za Prisons

**Na Isaac Kijoti, MBEYA**

LICHA ya matokeo ya sare tasa waliyoyapata katika mechi ya juzi dhidi ya Mbeya City, Kaimu Kocha Mkuu wa Yanga, Boniface Mkwasa, amewatoa hofu mashabiki wa timu hiyo kuelekea mchezo wao dhidi ya Tanzania Prisons.

Katika mechi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini hapa, mvua kubwa iliyonyesha kwa takribani dakika 10 baada ya mechi kuanza, ilichangia kwa kiasi kikubwa wachezaji kushindwa kuonyesha soka la kuvutia.

Yanga itashuka tena kwenye uwanja huo kesho, Ijumaa kuivaa Tanzania Prisons iliyopo nafasi ya nne katika mechi nyingine ya Ligi Kuu Bara inayotarajiwa kuwa ngumu zaidi.

Hata hivyo, Mkwasa aliliambia Nipashe kuwa ana uhakika mechi hiyo watafanya vizuri kama hali ya uwanja itakuwa rafiki.

Mkwasa, kocha wa zamani wa Ruvu Shooting na Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), alisema pamoja na hali mbaya ya uwanja iliyotokana na mvua, lakini pia aliwakosa wachezaji wake wengi wa kikosi cha kwanza.

"Mashabiki wetu wasiwe na hofu katika mechi ijayo dhidi ya Prisons, wajitokeze kwa wingi kuja kuishangilia timu, ninaamini tunaweza kufanya vizuri.

"Mechi ya leo (juzi) tuliwakosa wachezaji wetu muhimu wa kikosi cha kwanza ambao ninauhakika tutaungana nao dhidi ya Prisons," alisema Mkwasa.

Mkwasa ambaye anakaimu nafasi hiyo baada ya Mwinyi Zahera kutimuliwa, hiyo ni sare yake ya pili katika mechi tano za Ligi Kuu alizoiongoza Yanga, zingine akishinda.

Miongoni mwa wachezaji wa kikosi cha kwanza aliowakosa juzi ni pamoja na Kelvin Yondani, Feisal Salum " Fei Toto", Abdul-Aziz Makame, Mohammed Issa na golikipa, Metacha Mnata.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 9